**Kikao cha Kumi na Tatu - Tarehe 27 Machi, 2015**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa (Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Kuchunguza Upotevu wa Nyaraka):** Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani ripoti ya Kamati Teule ya Kuchunguza Upotevu wa Nyaraka za Serikali. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

**HOJA ZA KAMATI**

**Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhitibi Hesabu za Serikali na Mashirika ya Mwaka 2014/2015**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Spika:** Majadiliano yanaendelea, na jana tulianza kupokea michango ya Wajumbe mbali mbali na leo tunaendelea na michango hiyo. Wajumbe nilionao ambao kuna na safu ya mawaziri nitawaomba baadaye, hadi sasa ni Wajumbe watano pamoja na mawaziri hao ambao wataomba.

Nafikiri ni idadi ambayo si kubwa lakini pia si ndogo kufuatana na muda ulivyo. Kwa hiyo tuanze kumsikiliza kwa asubuhi hii Mhe. Abdalla Juma Abdalla, hayupo. Badala yake tumsikilize Mhe. Marina Joel Thomas.

**Mhe. Marina Joel Thomas:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kuchangia ripoti hii ya Kamati ya *PAC*. Nataka niwapongeze Kamati hii ya *PAC* kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya. Wamefanya kazi nzuri ya kuibua mambo mengi, mambo ambayo pengine hata serikali haiyatambui.

Mhe. Spika, naomba niseme kama maneno matano tu kuishauri serikali.

1. Serikali naomba ijiridhishe na ripoti hii. Kamati imefanya kazi, Kamati imetoa ushauri kwa serikali. Serikali naomba ichukue ushauri wa Kamati, lakini ijiridhishe na ripoti hii. Kwa sababu ripoti inaweza ikatolewa maamuzi pengine wengine wamo katika hatia na wengine hawamo katika hatia.

2. Itumie vyombo vyake vya uchunguzi vichunguze vione ukweli uko wapi.

3. Itoe maamuzi baada ya kuridhika na uchunguzi huo wa hali halisi ilivyo.

4. Itoe adhabu kwa wale wote waliohusika na matukio hayo mbali mbali ambayo yameelezwa katika ripoti hii.

5. Itoe adhabu kwa wahusika bila ya upendeleo wowote.

6. Ikishatoa maamuzi serikali ituletee taarifa hapa Barazani, hatua gani ambayo imechukua kutokana na ripoti hii. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Mohammed Mbwana Hamad:** Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nachukua nafasi ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia asubuhi hii kuwepo hapa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu ya kila siku; ya kuwatetea wananchi pamoja na kuisimamia serikali juu ya utendaji wake wa kazi za kila siku.

Mhe. Spika, nachukua nafasi pia kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*, na wajumbe wake kwa kazi nzuri sana ambayo wanaifanya kila mwaka juu ya kueleza zile kero, matatizo, mashaka yanayotokana na mapungufu ya utendaji kazi wa watendaji wa wizara mbali mbali za serikali. Kamati hii ya *PAC* inastahiki pongezi za makusudi kutokana na kufichua mambo ambayo yamejificha ndani ya Wizara zetu za Serikali.

Mhe. Spika, nimpongeze vile vile Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwani yeye ndiye tochi ambayo inamurika yale maovu ambayo yanatendeka katika Wizara na Taasisi zetu za serikali.

Mhe. Spika Waziri wa Fedha na yeye nimpongeze kwa uwasilishaji wa ripoti yake ambayo ameieleza pale kwa ufasaha zaidi.

Mimi mchango wangu nataka nianze kwenye ripoti ya Mhe. Waziri katika *page* ya kwanza ya ripoti yake, amesema hapa. Utendaji mzuri wa Kamati umeisaidia sana azma ya serikali ya kuimarisha usimamizi wa fedha za umma ikiwemo mapato na matumizi ya serikali.

Mhe. Spika, sentensi hii ni nzuri sana kwamba Kamati imeisaidia sana azma ya serikali ya kuimarisha usimamizi wa fedha. Nasikitika kuona kwamba makusanyo yapo lakini yanavuja. Sijui Kamati hii imeisaidia vipi serikali kuyadhibiti mapato hayo wakati ambao mapato kama tulivyoelezwa na Kamati ya *PAC,* mapato yanakuwa makubwa lakini upotevu unakuwa mkubwa zaidi.
Nimuombe Mhe,. Waziri wa Fedha atueleze sababu gani za msingi zinazopelekea kupotea kwa fedha nyingi za wavuja jasho wa nchi hii.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu katika ripoti ambayo ameieleza Mhe. Waziri wa Fedha ukurasa wa pili. Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Waziri hapa ameeleza kama ifuatavyo. Kamati katika kupitia ripoti ya ukaguzi wa hesabu kwa wizara, mashirika na taasisi za serikali ya mwaka 2011/12 iliweza kuchambua hoja 92 zilizogawanyika katika sehemu kuu tano zifuatazo. Matumizi ya Fedha za umma yasiyofuata utaratibu wa sheria za fedha na sheria za matumizi za mwaka 2005.

Mhe. Spika, kwa kweli ukiviangalia vitabu vya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, ukiangalia ripoti za *PAC* zote tokea mwaka 2011 mpaka tulipo, haya ndiyo mambo yaliyotawala. Watendaji waliopewa dhamana za fedha wanatumia fedha kinyume na taratibu. Serikali imenyamaza kimya kuwachukulia hatua wabadhirifu hawa wa mali ya umma. Wabadhirifu hawa ambao wanapoteza fedha nyingi kwa maslahi yao. Wabadhirifu hawa ambao hawana imani na wananchi wa nchi hii.

Mhe. Spika, naiomba Serikali iwe makini sana juu ya kusimamia udhibiti wa fedha. Jamani fedha zinazopatikana katika nchi hii lau kama zinatumiwa vizuri basi hapana shaka kwamba nchi hii ingekuwa ina neema za kuendelea, lakini kila siku umasikini wa watu wetu unaongezeka, utajiri wa wachache unaongezeka, mpaka lini haya?

Mhe. Spika, tunaiomba serikali, lakini sijui tunazungumza na serikali? Kwa sababu kila mwaka tunapiga makelele haya haya. Hii serikali tukisema sikivu, usikivu wake uko wapi? Usikivu wa serikali ungekuwa pale ambapo kunatokea matatizo ya ubadhirifu wa mali za watu, mali za umma, inachukua hatua za kisheria, lakini kinachotokea hapa ni majibu ya kupanga.

Kinachotokea hapa ni majibu ya usanii, kwisha! Lakini hakuna majibu ya kumuwajibisha mtendaji yeyote ambaye amefanya makosa.

Mhe. Spika, katika ripoti ya Mhe. Waziri wa Fedha ukurasa namba 3 kuhusu kasoro zilizobainishwa anasema.

"Mhe. Spika, baada ya kupitia ripoti hizo mbili kinachojitokeza ni kuwa kwa muhtasari Kamati ya *PAC* imebainisha kasoro kuu zifuatazo"

"Kasoro ya kwanza bado kuna ukiukwaji wa taratibu za matumizi ya fedha za umma kwa baadhi ya taasisi za serikali."

Jamani Kamati ya *PAC* kila mwaka inasema hivi, lakini Kamati hii iseme hivi mpaka lini. Mimi naiomba serikali iwe makini kwa sababu wananchi wanatusikiliza, wananchi wana akili, wananchi wanasoma mambo mbali mbali, wanasikiliza Mabunge mbali mbali, wanasikiliza taarifa mbali mbali.

Sisi serikali yetu itakuwa ni serikali ya kimaajabu ajabu kwamba kila siku Baraza la Wawakilishi linaibua matatizo ya watendaji mbali mbali lakini serikali imekaa kimya, inawalinda, inawaheshimu, inawatekelezea mambo yao tofauti tofauti huku wananchi wanaumia.

Mhe. Spika, kwa kweli umefika wakati wa serikali kuondoa uvivu, inasikitisha sana kwamba Mawaziri wakati mwengine wanatupa majibu ya kubabaisha. Juzi tu hapa tumeambiwa Waziri wa Elimu kuhusiana na fedha za madeski kwamba hawajapewa kutoka Wizara ya Fedha isipokuwa milioni 700 ndani ya bilioni 2 zilizochangishwa, lakini Waziri wa Fedha ametwambia amewapa Fedha zaidi ya ile asilimia iliyotarajiwa, ukweli uko wapi?

Mhe. Spika, umefika wakati wa serikali kujijua, kujiamini na kutoa maamuzi ya uhakika juu ya watendaji ambao wana nia mbaya kwa nchi na wananchi wa nchi hii. Kwa kweli inasikitisha vile vile kwamba Waziri wa Fedha katika hotuba yake hii alisema miongoni mwa changamoto zinazowakabili watendaji wetu ni kutokana na taaluma ndogo waliyonayo. Hili linatilika akilini, hivi sasa tunajua kwamba Zanzibar tuna vyuo vikuu vingi vinavyotoa taaluma ya fani mbali mbali. Hivyo Wahasibu hawa wana viwango gani vya elimu mpaka ifikie hatua ya kupoteza mabilioni ya mashilingi ya wananchi.

Mhe. Spika, kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri ikiwa watendaji wake taaluma yao ndogo, ni mpango gani aliojipangia kwa ajili ya kuwapa taaluma ya kutosha watendaji hawa ambao wanaharibu kila siku. Kuna mambo yanaharibika namna tofauti tofauti. Kuna fedha zinapotea kiholela, lakini kuna fedha zinapotea kwa kupotea risiti, kwa kupotea *documents* tofauti tofauti, ambazo zinalazimika pia zinakuwa hazionekani *documents* hizo. Huu ni ukosefu wa elimu, ni ukosefu wa uzembe au ni uzembe? (*Makofi*)

Mhe. Spika, namuomba kabisa kabisa Waziri wa Fedha aangalie vizuri watendaji wake, na aangalie vizuri safu ya watendaji wa fedha waliokuwa hawajatimiza vigezo awapeleke masomoni na awaingize ambao wametimiza vigezo katika kukidhi haja ya kudhibiti fedha.

Mhe. Spika, mimi nina imani kwamba kuna watu wengi, vijana wengi wamesoma, wana elimu kubwa, wana uwezo wa kudhibiti fedha, ikiwa waliopo hawakidhi haja hebu Wizara husika itangaze wale ambao wamefikia kiwango fulani cha elimu kwa ajili ya usimamizi wa fedha muangalie ni watu wangapi watakaokwenda. Mimi nasema kwamba serikali haijakuwa makini kwa hili, tumefanya kwamba serikali ni kama shamba la bibi tu, mjukuu, kitukuu, wote wanakwenda katika shamba lile kuchukua mali zao.

Mhe. Spika, umefika wakati wa Serikali kubadilika, tubadilike! Ili tubadilike tuondoe muhali, huyu mtoto muhali mpaka lini? Jamani Zanzibar tutakuwa na muhali mpaka lini? Naamini mtendaji yeyote anayeharibu pesa za umma kama ana duka lake na akamuachia mtu kumuendelezea duka akaliharibu hakubali anamfukuza. Itakuwaje serikali iwaachie watu, watendaji wasiokuwa na imani na wananchi waendelee kuharibu rasilimali, kuharibu mapato, kuharibu fedha za wananchi wa nchi hii.

Mhe. Spika, tutaendelea kuwatia unyonge wananchi wa nchi hii kwa sababu ya kutokuwa makini watendaji wetu wakubwa. Kwa hivyo naiomba serikali ikiwa ni sikivu iwe ni sikivu kweli kwa ajili ya wabadhirifu wa hali ya umma.

Zimeundwa Kamati Teule kadhaa, na kila Kamati Teule inayokuja hapa inakuwa na maburungutu ya matatizo. Maburungutuu ya upotevu wa fedha, lakini serikali kimya. Leo imeshaweka hati mezani hapa ya kusoma ripoti teule ya upoteaji wa nyaraka, kitakachoendelea ni kupiga kelele halafu basi.

Mhe. Spika, umefika wakati wa kubadilika, ikiwa Mhe. Hamza Hassan Juma jana alitwambia kwamba Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi amewaambia kwamba wasimfumbie macho kiongozi yeyote wa CCM ambaye anafanya ubadhirifu wa mali ya umma. Umefika wakati, na sisi *CUF* tumeambiwa hivyo hivyo na kiongozi wetu kwamba tusiwe tayari kumlinda mbadhirifu yeyote wa mali ya umma. Sasa jamani tuko wapi. Mheshimiwa tuko wapi? (*Makofi*)

Mhe. Spika, umefika wakati wa kuhakikisha kwamba wanaofanya ubadhirifu wa mali ya umma kwao, wanaofanya ubadhirifu wa mali ya umma futa, *delete,* kabisa kabisa! Jamani tutaweka watu watakaoifisidi nchi hii mpaka lini?

Mhe. Spika, uliniwashia taa muda mrefu ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii na huo ndio mchango wangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chambani naiunga mkono Ripoti ya *PAC* kwa asilimia mia moja . Ahsante.

**Mhe. Abdalla Juma Abdalla:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi nataka nikushukuru sana kwa huruma zako hizo za kuniachia angalau dakika kumi niweze kutekeleza wajibu wangu wa kuisimamia Serikali kwa maslahi ya wananchi.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze na ukurasa wa 4 wa Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali ambayo ilikuwa inachunguza au inafuatilia ukaguzi maalum wa viinua mgongo.
Kutokana na kamati hii *CAG* amefanya *something* ya kukagua Taasisi 4 katika mada hii ya uchunguzi wa viinua mgongo. Na katika taasisi 4 hiyo amekagua viinua mgongo vya wafanyakazi 60. Mhe. Spika, mambo aliyoyagundua ni haya yafutayo:

Kwanza; kuongeza kwa muda wa utumishi wa mstaafu na ujanja huo unafanywa, pili kuongeza mshahara wa mwisho ambao hutumiwa kutayarisha kiinua mgongo na huo ni ujanja mwengine ambao unafanywa na vitengo vya fedha. Lakini tatu *CAG* amegundua wastaafu kulipwa mara mbili mbili kinyume na utaratibu.

La nne ambalo hakuligundua maana huwa halipiti kwake, kuna wafanyakazi wanaostaafu wanalipwa chini ya kiwango wanachostahiki kulipwa, hili Mhe. Spika, mara nyingi huwa tunalalamikiwa sisi mtu akishanyimwa pesa zake huko anatujia sisi, bwana mimi nilikuwa nilipwe hiki lakini sikulipwa hiki ninalipwa hiki.
Sasa hii inaonesha Mhe. Spika, kuna mchezo mchafu unafanywa na Wahasibu katika taasisi za serikali, hili la kwao. Kama watakuwa wanashirikiana na uongozi wao wa taasisi sawa lakini hili la kwao, maana yake wao ndio wanao-*monitor*, wanao-*audit,* ndio wanafanya kila kitu kuhusu mafao ya wafanyakazi wanaostaafu.

Sina hakika kama wakishaongezewa halafu anarudi wanagawana na huyu sina hakika, lakini huu ni mchezo mchafu Mhe. Spika, unafanywa na kwa mujibu wa *CAG* hizo taasisi chache tu alizozikagua tayari Serikali imepata hasara ya sh. milioni 137.7

Sasa wamejitetea ukifuatilia hii ripoti wizara hizi zimekanusha kanusha sana kwamba si kweli, si kweli kulikuwa na hivi, lakini mimi nataka niseme, kwanza sijaamini kama si kweli, kwa sababu *CAG* anapokuja hizi taasisi zinakuwepo, kwa nini kama si kweli hawamwambii *CAG* kama si kweli, wanamsubiri mpaka anaandika ripoti halafu wanakuja kukanusha mbele ya Kamati maana yake nini, kipindi hiki cha katikati hapa wamejipanga wapate jawabu ya kuiambia kamati lakini huu ni ukweli, na kwa kweli kuna mambo Mhe. Spika, lazima yafanywe. Kwa sababu hizi ni taasisi chache sana katika taasisi tulizonazo katika nchi.

Ikiwa wastaafu 60 hawa zimepotea shilingi milioni 137.7 je, *CAG* kama angefanya ukaguzi wa Serikali nzima tungeona pengo kubwa sana la fedha ambazo zinapotea kupitia ustaafu tu.

Sasa naomba sana Mhe. Waziri pamoja na Serikali, hebu hawa watu waangalieni wanatutia hasara sana, wanawaumiza wananchi sana, kwa sababu hizi pesa wanazogawana kiholela hizi ni pesa za wananchi, ambazo tungezi-*save* tungepata kufanyia mambo mengi sana ya huduma za jamii.

Wahasibu wana matatizo na kama tukiendelea kuwaachia, tutaendelea kuwaonea muhali watatumaliza. Naomba sana Mhe. Waziri hili alione na tungetamani sana kuona mabadiliko makubwa katika sekta hii ya fedha.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nilisema nilitaje kwa sababu limetajwa na kamati, na mara nyingi huwa ninalitaja, kuwa miongoni mwa kazi anazozifanya *CAG* ni kukagua matumizi yanayofuata utaratibu ya fedha. Lakini kila anapotoa ripoti yake basi anatwambia kuna matumizi ambayo yanafika *this amount* ambayo hayakutumia utaratibu, na mara hii kuna bilioni 16.2 zimetumiwa bila ya utaratibu, sisemi kama zimeibiwa zote hizi, lakini inawezekana miongoni mwa hizi zimeibiwa kwa kutofuata utaratibu, na wanaofanya ni hawa hawa wahasibu.

Jengine Mhe. Spika, ametaja pia Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* kama ni malalamiko kuhusu mishahara hewa, na kwa mujibu wa taarifa tulizozipata kwa *CAG* ndani ya kila mwaka mmoja Serikali inapata hasara bilioni 1.8 kwa ajili ya kulipwa watu hewa, hakuna mtu anayeitwa hewa, isipokuwa huu ni wizi unafanywa na wahasibu.

Sasa Mhe. Hamza alisema jana kwamba sisi kazi yetu ni kulalamika basi tuendelee kulalamika, na tutaendelea kwa sababu kama hayakuchukuliwa hatua tukaona siku moja yanakomeshwa hayaendelei *CAG* akienda atayaona na akishayaona atatuletea na sisi tutayasema.

Na ninamuomba sana *CAG* asichoke hata kama hayachukuliwi hatua, aende akayafanyie ukaguzi, ayagundue atuandikie na sisi tuendelee kulalamika labda siku moja wananchi watafanya maamuzi. Maana yake Serikali inachaguliwa na wananchi bwana, kwa hivyo wenyewe wao wakifika pahali wakiona aa ishakuwa mno, watafanya maamuzi ya busara.

Mhe. Spika, nilisema juzi hapa kwamba *problem* ambayo tunayo tunaoneana muhali, wezi wote wanajulikana katika nchi hii lakini hawachukuliwi hatua kwa sababu ya muhali tu, mtoto wa fulani, mtoto wa fulani. Sasa wanaendelea kuwaumiza wananchi kwa sababu ni mtoto wa fulani anaachwa, ni udhaifu mkubwa sana, na kama hatujaweza kujirekebisha basi hata wananchi kuna siku watapoteza imani kabisa na Serikali yao.

Jambo la mwisho Mhe. Spika, kwa sababu muda sina naomba niende ukurasa wa 127 ambako kuna jambo muhimu sana ambalo Serikali bado hawajaliona wakalipa umuhimu.

Ameeleza pale kwa mujibu wa Ripoti ya *CAG* kwamba kuna ukosefu wa utunzaji na udhibiti wa maeneo ya kihistoria.

Hiki Mhe. Spika, ni chanzo chengine cha fedha, kama kitatunzwa vizuri inaweza ikaingia pale pesa nyingi sana lakini bahati mbaya Serikali hawajaliona hili. Kuna magofu yametajwa hapa ambayo kayatembelea *CAG* akaona hali yake ni mbaya na magofu ya Ras Mkumbuu, magofu ya Mkama Ndume; Pujini, magofu ya Chwaka Tumbe, magofu ya Jambangome kule Wambaa. Haya magofu yapo na yana historia kubwa na ni vivutio vikubwa kweli kweli.

Kwa mfano kama lile gofu la Mkama Ndume pale lile jumba mpaka leo lipo na hata ile *structure* yake iko kamili, tatizo ni kwamba Serikali hawajaweka pesa za kutosha ya kufukua kile kifusi halafu lile jumba likaonekana, likatunzwa watalii wakaenda wakajionea historia ili nchi yetu ikaendelea kupata matumizi.

Kwa hivyo naiomba sana Serikali kwa sababu ni chanzo cha kuingiza fedha, hebu watoe *priority* kwa haya magofu ili yaweze kutusaidia kuongeza mapato yetu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, na kwa kuheshimu muda wako, mimi naomba nikubaliane sana na ripoti ya *PAC,* na naiomba sana Serikali hebu iondoe muhali.

Mhe. Rais aondoe muhali, juzi nilisema hapa yule mzee Paul Kagame hataki muhali, na kwa sababu kaondoa muhali Serikali yake inakwenda vizuri. Sasa huwezi kuwa kiongozi watu wakawa na tabia zao za kunyofoa nyofoa halafu ukawaonea muhali mambo yakawa mazuri, haiwezekani, lazima Mhe. Rais aondoe muhali, afumbe macho *akate pua aunge wajihi* lakini tuheshimiane, tuheshimu sheria za matumizi ili tupate nchi inayosonga mbele kimaendeleo.

Mhe. Spika, baada ya maneno hayo naomba kukaa.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi ya kuchangia katika mswada huu kidogo ili na mimi nijaribu kuweka *hansard* sawa kwa baadhi ya matokeo yaliyozungumzwa juzi.

Kwa kweli Mhe. Spika, sikutaka kuchangia kwa sababu nilikutana na wenzangu nikazungumza tukafanya masahihisho mbali mbali, lakini ninasikitika sana bado michango inaendelea na bado tuhuma zinaelekezwa kwa Waziri wa Elimu, na hata msemaji aliyemaliza kusema sasa hivi ndio aliyenishawishi nikuandikie kwamba na mimi nataka kuchangia.

Kazungumza kwa ukali sana, kwa tuhuma kubwa sana, kwamba pesa nimepewa zote kwa ukamilifu, nyingi, lakini madeski hayakuchongwa. *as if* ana uhakika kwamba hayakupangwa, ana uhakika kwamba hayakugaiwa maskuli, ana uhakika kwamba hakuna tulichokifanya?

Mhe. Spika, ni muda mrefu kidogo nilitaka nionane na Mhe. Waziri wa Fedha kumuomba kwamba anisaidie kuniongezea au kunipatia kwa wakati bajeti ya *OC's* ambayo nadhani kwa Serikali hii Wizara ya Elimu ndio inayopata bajeti ndogo sana ya *OC's*.

Kama sikosei na niko tayari kusahihishwa, sidhani kama ninapata zaidi ya asilimia 32 ya *OC's*. *OC's* maana yake matumizi mengineyo.

Nilitaka nizungumze na waziri mwenzangu mapema ili tujaribu kuliangalia suala hili na mambo mengine, lakini kwa bahati mbaya sana hatukuonana isipokuwa jana tumekutana tumezungumza mengi na tumefahamiana, lakini kwa bahati mbaya kilichozungumzwa katika mkutano wa juzi imeshaandikwa kwenye *hansard*, nikaona na mimi nisipokizungumza, ukikubali ulichoambiwa kwa kunyamaza kimya maana yake umekikubali.

Umekubali kwamba pesa nimepewa za kutosha, nyingi, na madeksi sikuchonga na sikugawa wala hayapo.

Sasa mimi nasema madeski yapo, nimechonga mengi tu, nimeshayagawa na mengine naendelea kuyachonga.

Mhe. Spika, ningekusomea orodha moja moja ya skuli nilikoyapeleka madeski haya ningechukua muda mrefu sana, ila naomba upokee orodha hii nitayokukabidhi ya madeski niliyoyachonga na skuli nilizoyapeleka, ukisha kwa hisani kubwa sana kutoa *photocopy* ya waraka huu uwape Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi. Hiyo itaondosha wasiwasi kwamba mimi ni mwaminifu, nafanya kazi zangu kwa uadilifu mkubwa na situmii pesa za Serikali ovyo.

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa angalau jumla ya madeski yale yaseme ili iingie kwenye *hansard,* kwa sababu si wengi wataofuatilia ripoti hiyo na wakaijua. Sasa angalau ile jumla itasema kwamba *okay* kumbe madeski yamechongwa kwa kiasi fulani.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Nitayasema.

**Utaratibu**

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Spika, nilikuwa nataka utaratibu kidogo Mhe. Waziri leo anataka kuweka mambo sawa, na kauli aliyoitoa Mhe. Waziri wananchi wanaisikiliza kwa hamu kubwa sana.

Na kusema tu atwambie kwa jumla idadi ya madeski pia bado haisaidii sana. Mhe. Spika, umefuta maswali na majibu ili kupata muda mzuri wa kufanya hii shughuli. Mimi nafikiri kwa hili tusiwe na haraka, kwa sababu tunajua kauli za Serikali zinapogongana lazima pawe na kauli inayosafisha kila kitu.

Kwa hivyo ushauri wangu Mhe. Spika, Mhe. Waziri asione tabu, atutajie skuli fulani wamepata mangapi, skuli fulani mangapi, tusione tabu, ndio kazi yenyewe tuliyoijia hapa. Ahsante sana.

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri wa Elimu ninakupa dakika 10 ufanye kazi hiyo.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, mtoa hoja alisema nipewe muda wa kutosha ili nitaje skuli kwa skuli nilikopeleka madeski, na orodha hiyo ninayo hapa nilipo. Dakika kumi hazinitoshi, niruhusu nikusomee skuli kwa skuli nilikopeleka madeski.

**Mhe. Spika:** Endelea.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Lakini kabla sijaenda huko nataka kutoa ile takwimu ya pesa nilizozipokea za kodi ya Bandari kwa wasafiri wa Dar es Salaam kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita; mwaka 2012, 2013, 2014 na huu mwaka tulionao 2014/2015.

Mwaka 2014/2015 nilipokea shilingi 941 milioni. Mwaka 2013/2014 nilipokea shilingi 833 milioni, mwaka 2012/2013 nikapokea shilingi 563 bilioni hizi ni kodi za bandari ndizo nilizo pokea. Kwa ujumla

wa miaka mitatu si wa mwaka mmoja, miaka mitatu nimepokea shilingi bilioni 2,338,000,000 kwa muda wa miaka mitatu sio mwaka mmoja.

Mhe. Spika, na kwenye bajeti yangu ya serikali tumeendelea nayo, sasa hivi tunamaliza keshokutwa, ningesema kwamba tutakabidhiwa bilioni 2 kwa mwaka, sio kwa miaka mitatu kwa mwaka.

Sasa kwa ujumla wa suala hili nimepokea shilingi milioni 943,000,000 zilikusanywa, sio nilizopokea, samahani, zilizokusanywa na mimi nikapokea shilingi milioni 680,829,276 katika hizi ukitoa kilichokusanywa na nilichopewa utakuta kuna upungufu wa shilingi milioni 260,538,894 huo ndio upungufu ambao uliokuwa sikuupokea. Na niko tayari kusahihishwa, na kama kuna mtu anataka kuchangia kuthibitisha kwamba nimepokea zaidi ya hizo athibitishe.

Mhe. Spika, lakini baada ya kutoa taarifa yangu juzi nikashutumiwa kwamba nimemkandia Waziri wa Fedha, wala haikuwa nia yangu, maana kuna Waswahili wamesema "*ukiwepo mtoni usigombane na mamba*" atakuparura tu.

Sasa mimi sikuwa na dhamira ya kugombana na mamba, mimi nilikuwa na dhamira ya kusema ukweli nilichopewa ndio hiki. Kwa hivyo, juzi tarehe 24/03/2015 nimetiliwa katika *account* ya Wizara ya Elimu shilingi 161,000,000 juzi kishindo cha jana, nimetiliwa pesa hizo. Kwa hii hesabu niliyokupa Mheshimiwa ni ile kasoro ambayo ilikuwa sikutiliwa, baada ya kusema ikatoka kauli kwenye mkutano kwamba nitatiliwa 300,000,000 nikatiliwa 261,000,000. Hicho ndicho kilichosababisha niseme ukweli usikike na wenzangu nipate hizi pesa.
Mimi namshukuru sana Mhe. Waziri sana, sana kanipa hizi pesa ninazo, nimeshazitia katika *account* yangu ninazifanyia kazi, kulipa yale madeni machache, machache yaliyobakia yaliyokuwa wameshatengeneza madeski.

Mhe. Spika, nataka mnisikilize vizuri pamoja na Wajumbe nataka kusema kama ulivyonitaka, ulivyonishauri na alivyozungumza Mhe. Hamza nikutajie skuli moja moja niliyopeleka madeski.

Mhe. Spika, hatimaye uunde kamati iende katika hizi skuli wakachunguze, maana nimesikia kauli hapa inazungumza kwamba tunatoa kauli za kubuni kubuni, kauli za ajabu ajabu tu. Hiki nilichokusomea si ajabu ni uhakika, na tuma Kamati yako iende ipite maskuli ikachunguze haya madeski yapo au hayapo, yamepelekwa au hayakupelekwa.

Mhe. Spika, skuli ya kwanza "*mkaa na maiti haachi kulialia*" skuli ya mwanzo Donge. (*Makofi*)

Donge nimepeleka viti vya wanafunzi 90, meza 90, viti vya walimu viwili. Kidoti madeski 90, Donge sikupeleka madeski ni *secondary school* sikupeleka madeski.

Kidoti madeski 90, viti vya wanafunzi hakuna, meza hakuna, viti vya walimu viwili na meza za walimu ni mbili.

Kinyasini madeski 120, hakuna meza wala hakuna kiti, lakini meza za walimu ni 8 na viti vya walimu ni 8.

Gamba madeski 150, viti hakuna na meza hakuna; ni *primary school* hii. Kwa hiyo, meza za walimu 10 na viti vya walimu 10.

Mkokotoni madeski 70, ni *primary school* hii, hakuna viti, kuna meza 7 za walimu na viti 7 vya walimu.

Kinyasini Maandalizi hakuna madeski kuna meza za wanafunzi 45, viti vya wanafunzi 45, meza ya mwalimu 1 na kiti cha mwalimu 1.

Bumbwini Msingi madeski 100, hakuna kiti wala hakuna meza, kuna meza 9 na viti 9 vya walimu.

Kinduni Msingi kuna madeski 30, meza hakuna na kiti hakuna. Nimesema Kinduni Msingi kuna meza 2 za walimu na viti 2 vya walimu.

Kinyongele Msingi kuna madeski 30, hakuna meza wala hakuna viti, kuna viti 2 na meza 2 za mwalimu.

Mahonda Sekondari hakuna madeski, kuna meza 100 na kuna viti 100, kuna meza 5 za walimu na kuna viti 5 vya walimu.

Muyuni Msingi madeski 150, hakuna meza, hakuna kiti, kuna meza 2 za mwalimu na viti 2 vya mwalimu. Jambiani Sekondari hakuna madeski kuna meza 45, kuna viti 45 hakuna meza ya mwalimu wala hakuna kiti cha mwalimu kilichopelekwa.

Makunduchi Sekondari hakuna madeski yaliyopelekwa, kuna meza 90 na kuna viti 90, hakuna meza wala hakuna kiti cha mwalimu.

Kizigoni Maandalizi hakuna madeski, kuna meza 180, kuna viti 180 na kuna meza 3 za mwalimu na kuna viti 3 vya mwalimu vilivyopelekwa.

Dunga Sekondari hakuna madeski kuna meza 90 na kuna viti 90 na kuna meza 3 za mwalimu na kuna viti 3 vya mwalimu vimepelekwa. Kiboje Msingi, nimekosea, mbona mnacheka.

**Mhe. Spika:** Imefahamika!

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Naam!

**Mhe. Spika:** Sasa wamefahamu. (*Kicheko/Makofi*)

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Kuna madeski 45, msingi huku hakuna meza, hakuna kiti, kuna meza 3 za walimu na kuna viti 3 vya walimu vilivyopelekwa.

Bambi Sekondari hakuna madeski, kuna meza 90, viti 90, meza za walimu 3 na viti vya walimu 3.

Kiboje Sekondari hakuna madeski lakini kuna viti 135, meza 135 na hakuna kiti cha mwalimu, hakuna meza za walimu zilizopelekwa kwa sababu zipo.

Machui Msingi kuna madeski 45, hakuna meza, hakuna viti, lakini kuna viti 3 na meza 3 za mwalimu zilizopelekwa.

Machui Msingi kuna madeski 45 hakuna meza wala viti, lakini kuna meza 3 na viti 3 vya walimu.

Darajani Msingi kuna madeski 180 hakuna kiti, hakuna meza, hakuna kiti cha mwalimu, hakuna meza ya mwalimu iliyopelekwa, kuna madeski tu 180.

Kidongo Chekundu Msingi kuna madeski 150, hakuna meza hakuna kiti cha mwalimu kilichopelekwa.

Lumumba Sekondari hakuna madeski yaliyopelekwa, lakini kuna meza 90, kuna viti 90 hakuna cha mwalimu, hakuna cha mwanafunzi kilichopelekwa.

Jang'ombe Msingi kumepelekwa madeski 200, hakuna meza hakuna kiti cha mwalimu wala cha wanafunzi kilichopelekwa.

Kidongo Chekundu "B" Msingi kuna madeski 150.

*Zanzibar Commercial* kuna meza 85 na kuna viti 85, hakuna kiti cha mwalimu wala meza ya mwalimu iliyopelekwa.

Kisauni Sekondari hakuna deski lililopelekwa, kuna meza 90 na kuna viti 90. Jumla ya hizi skuli nilizozitaja hizi tumepeleka madeski 1,540…

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa mnaotoka nje tunataka kumaliza hoja hii baada ya muda mfupi, kwa hiyo tukumbuke kurudi.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Tumepeleka meza 1,230, tumepeleka viti 1,230, tumepeleka meza za walimu 69 na tumepeleka viti vya walimu 69.

Mhe. Spika, nakusomea orodha ya Pemba.

Micheweni Maandalizi tumepeleka meza 200 na viti 200.

Uondwe Msingi tumepeleka madeski 60 hatukupeleka meza wala viti, lakini tumepeleka meza 9 za walimu na viti 9 vya walimu.

Dodo Msingi madeski 105 hakuna meza, hakuna kiti, kuna meza 12 na viti 12 vya walimu.

Maziwani Msingi madeski 75, hakuna meza, hakuna kiti, kuna meza 10 na viti 10 vya walimu.

Mkote Msingi ndio wapi, naam! Ipo eeh, naambiwa ipo Mkote Msingi madeski 60, hakuna meza, hakuna kiti, kuna meza 6 na viti 6 vya walimu.

Ole Msingi madeski 60, hakuna meza, hakuna kiti, kuna meza 5 na viti 5 vya walimu. Konde Sekondari hakuna
madeski, kuna meza 150, viti 150, meza 11 za walimu na kuna viti 11 vya walimu.

Shengejuu Msingi kuna madeski 45, hakuna meza, hakuna kiti kilichopelekwa, lakini tumepeleka viti 9 na meza 9 za walimu.

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri orodha yako ni ndefu, ukiona ungekaa ukasema kwa utulivu zaidi, ruhusa ipo.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Sawa. Kisiwapanza Sekondari hakuna madeski, yamepelekwa. Kuna meza 60 na kuna viti 60, hakuna meza wala viti vya walimu vilivyopelekwa.

Mjimbini Msingi kuna madeski 90 hakuna meza wala viti vya wanafunzi vilivyopelekwa, lakini kuna viti 10 na meza 10 vya walimu.

Wawi Sekondari hakuna madeski kuna meza 135 na kuna viti 135 vya wanafunzi na meza 10 na viti 10 vya walimu.

Shidi Msingi madeski 60 hakuna meza wala kiti kilichopelekwa cha wanafunzi, lakini kuna meza 8 na viti 8 vya walimu.

Makoongwe Msingi madeski 60 hakuna meza wala kiti cha mwanafunzi, kuna viti 6 na meza 6 za walimu.

Mtuhaliwa Msingi kuna madeski 30 hakuna meza wala kiti, lakini kuna meza 6 na viti 6 vya walimu.

Chanja Mjawiri bila shaka sekondari, hapana, ni *primary* hii, kuna madeski 60 yaliyopelekwa hakuna kiti wala meza zilizopelekwa, si mwalimu wala si mwanafunzi.

*Fidel Castro* kuna viti 90 na meza 90, hakuna kiti hata kimoja wala meza hata moja ya walimu iliyopelekwa.

Jumla Pemba hiyo, madeski 705, viti 665, meza 665, meza za walimu na viti vya walimu 114 kila moja. Sasa jumla kubwa ya Pemba na Unguja madeski 2,245; viti 1,895; meza 1,895; viti vya walimu 183 na meza 183.

Pamoja na orodha hii niliyoisoma kwa ujumla wake bado nitatoa *copy* hizi Mhe. Spika hatimaye uzigawe kwa Wawakilishi wote.

Tume unayotaka kuunda tukishazigawa hawa Wajumbe wa Tume watakaoundwa wapite katika hizi skuli wakaangalie viti na meza nilizosema zipo sawa na *copy* nilizowapa?

Mhe. Spika, nafikiri inatosha kuweka mambo sawa, Mheshimiwa mimi ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Wajumbe wote wanajua kama kuna mtu anaumwa basi mimi naumwa kuona wanafunzi wangu wanasoma katika darasa zaidi ya 45 na wanakaa chini.

Mimi naumwa sana, lakini nitafanya nini, tunakwenda pole pole kuzijenga skuli na kadhalika.

Mhe. Spika, nataka nikupe hadithi ya *Milele Foundation. Milele Foundation* ni Wajumbe wa *NGO,* kamati ya *NGO* hii ni *DIASPORA* kutoka Arabuni, wametoka huko Arabuni wamekuja wakasema sisi ni Wazanzibari lakini tunaishi Arabuni.*Alhamdulillah Rabil-alamina* tumetononoka vya kutosha. Sasa huu utajiri tulionao tunataka na nyinyi wenzetu wa Zanzabar tukuleteeni kidogo nanyi mtononoke kidogo kwa skuli zenu, mnazo skuli ambazo zinahitaji kumalizwa? Tukawajibu tunazo nyingi sana, nyengine tumeshazikamilisha nyengine bado nyingi sana.

Wakanambia tupe Mkurugenzi wako mmoja au wawili tuitembee Zanzibar nzima Unguja na Pemba, tukaangalie skuli zako zilizokuwa hazikumalizika halafu sisi wenyewe tutaamua katika skuli hizo skuli 20 tutazimaliza sisi na nyumba mbili kila skuli tutazijenga. Baadae tutakaa tena tufikirie tunafanya nini, lakini hii ya mwanzo tutafanya hivyo.

Nikawapa Wakurugenzi wangu wawili wakatembelea Pemba na Unguja wakachagua skuli 20, na kazi sasa hivi inaendelea kwa kasi nzuri sana. Walitwambia chagueni skuli moja tuuzindue huu mradi tunaotaka kuufanya, wakachagua Skuli ya Mbuyutende, tukaenda Mbuyutende tukaangalia wakaanza kujenga na kukazindua rasmi kwa Unguja nzima. Jamaa hawa wanaendelea mbele.

Sasa fununu fununu zimeshatokezea kwa Wajumbe wangu wa Baraza la Wawakilishi, *duh*, jamani kuna *Milele Foundation* itatusaidia skuli, hebu twendeni tukazungumze nao, wakaja wakazungumza nao.

Kuna skuli moja, mbili wakazikubali *on condition* kwamba mimi Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali nitoe kibali kuwasaidia. Mimi nikatoa kibali kwamba kwa hawa saidieni, sina haja ya kuzitaja skuli wala sina haja ya Mwakilishi huyu katoka wapi lakini ziko.

Nataka niseme hapa kwa hivi sasa nakuombeni Wawakilishi msite kwanza kuwafuata hawa *Milele Foundation* tuwaachie wamalize skuli zetu 20, wakimaliza huru nendeni tutajitegemea wenyewe, lakini kwa sasa mkiwaendea ndio watapoona mizigo sasa inatuelemea, wataacha kutujengea skuli zetu 20 na wataacha kutujengea skuli nyengine.

Kwa hivyo, huu kwetu ni ukombozi mkubwa sana, tunamshukuru Mwenyezi Mungu na tunashukuru sana *Milele Foundation* kwa hisani zao walizotuonesha. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri nakushukuru sana kwa ufafanuzi huo, ila nataka niseme jambo moja tu. Katika kikao cha Kamati ya Uongozi tulikubaliana hakuna Kamati Teule nyengine tena, kwa hiyo kazi hiyo inaweza ikafanywa na kamati za kawaida wakafuatilia huko na wanaweza wakaleta ripoti baadae.

Lakini kama ulivyosema orodha hiyo itatolewa na Wajumbe watapata kila mmoja ya kwake. Baada ya shukurani hizo sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, nami nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana tena asubuhi ya leo, na kutuwezesha kufanya shughuli zetu kama tulivyopanga. Tunamshukuru sana *Allah* kwa uwezo huo.

Aidha, nikushukuru wewe Mhe. Spika kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu, nakupongeza sana namna ambavyo unavyoongoza Baraza letu.

Pia shukurani zangu za dhati zimuendee Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa namna ya uongozi wake wa hekima na busara anaotuongoza katika nchi yetu, na kwa uadilifu mkubwa ambao unatuletea matokeo mazuri ya maendeleo ya nchi hii.

Aidha, nichukue fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati hii ya *PAC* na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa maelekezo na muongozo wanaotupatia hasa katika utekelezaji wa matumizi ya fedha za serikali.

Mhe. Spika, nichukue pia fursa hii kumpongeza sana Waziri mwenzangu Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa maelezo yake ya ufasaha, ya kina na ambayo ameonesha mfano mzuri kwa kutoa taarifa zile zinazohitajika kutolewa. Hivyo ndivyo walivyo mawaziri wote pale wanapotakiwa kutoa taarifa watafanya hivyo kutekeleza wajibu ambao tumetumwa na wananchi.

Mhe. Spika, kwanza niseme kwamba serikali na Baraza la Wawakilishi lengo lake moja, serikali kazi yake ni kutumikia wananchi na Baraza la Wawakilishi kazi yake ni kuwatetea wananchi. Kwa hiyo, ukitizama lengo moja nia yetu sote ni kufanya mambo yaende vizuri kwa ajili ya maslahi ya wananchi wetu na Taifa letu, hilo ndilo lengo letu. Sasa kila ambalo zuri, jema, basi serikali iko tayari kulipokea na kulifanyia kazi kwa mujibu wa Katiba, sheria na taratibu tulizojiwekea. Kwa hiyo, niseme wazi kabisa, kwamba serikali yetu haina nia ya kuficha maovu yoyote yale, wala haina nia ya kuficha ubadhirifu na haitofanya hivyo. Nia yake ni kutenda mambo kwa uwazi na uadilifu, pale inapotokea kasoro ni kawaida za kibinadamu na serikali huchukua hatua kwa mujibu wa taratibu na sheria.

Mhe. Spika, nataka nimpongeze sana Mwenyekiti wetu wa Kamati ya *PAC* na Wajumbe wake kwa namna ambavyo wamewasilisha ripoti yao. Nataka niseme pia ripoti zetu hizi zilikuwa zinazungumzia

ripoti ya mwaka 2011/2012 na ripoti ya mwaka 2012/2013.

Hata ukisoma kitabu hiki cha Ripoti ya Mkaguzi Mkuu ambacho kinaelezea Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mawizara, Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka wa Fedha 2011/2012 kinaeleza jitihada zinazochukuliwa na Mkaguzi Mkuu amesema hapa. Kwa kipindi cha miaka mitatu jamii imeanza kuona mafanikio na marekebisho katika utendaji na uwajibikaji katika sekta za umma, mafanikio hayo ya kiutendaji yametokana na utekelezaji wa mapendekezo na ushauri unaotolewa katika ripoti za ukaguzi wa hesabu.

Mhe. Spika, maana yake serikali kila linalozungumzwa hapa inachukua hatua ya kurekebisha na mabadiliko yanaonekana, na hizi ripoti ambazo zinazungumzwa kama nilivyosema awali ni ripoti za 2011/2012, 2012/2013. Nina hakika kutakuwa na mabadiliko zaidi kwenye ripoti zinazofuata kama ambavyo kumekuwa na mabadiliko katika ripoti zetu hizi kila mwaka kurekebisha pale kwenye kasoro.

Kwa hiyo, nataka niseme kwamba, serikali inayasikiliza, inayafuatilia na inayatekeleza maoni yanayotolewa na Baraza letu hili Tukufu. Ni wajibu wao Waheshimiwa kusema, na sisi ni wajibu wetu kusikiliza na kutekeleza, lakini vile vile tufikie mahala Mhe. Spika tuheshimu kabisa kanuni zetu, sheria zetu ili tutende haki.

Mhe. Spika, wakati mwengine tunawazungumza wenzetu walio nje ya Baraza hili na ambao pengine hawakutajwa hata katika ripoti hii, kwa kweli tunakuwa hatuwatendei haki. Maana tunapozungumza jambo hapa lazima tuwe na ushahidi kamili, nia yetu sote iwe kutenda haki.

Sisi ni viongozi tuliochaguliwa, na wananchi wetu tunapofanya aina yoyote ya kuwasema wananchi wetu ama watendaji wetu ambao wametukabidhi mamlaka ya kuongoza nchi yetu, inasikitisha tunapokwenda kinyume na taratibu na kanuni. Kwa sababu wao wanahisi ni Baraza hili litawatetea na ni Baraza hili linalosema ndio ngome ya wananchi. Sasa tunapokuja tukakiuka mipaka tukawagonga kuwahujumu wakati katika ripoti hizi hawakuzungumzwa tunakwenda kinyume na taratibu na vile ambavyo tunatakiwa.
Kwa hiyo, niwaombe sote kwa pamoja, kila mmoja ana haki ya kutoa hekima yake, si kosa hata kidogo linapoonekana kosa ukalithibitisha ukaja kulizungumza, lakini pale ambapo huna ushahidi wa kutosha ripoti haikuletwa kumzungumza ukamzungumza mtu, kwa kweli inasikitisha, inasononesha, na wanatupigia simu wenyewe wahusika kutusikitikia kama serikali ina wajibu wa kutetea.

Mhe. Spika, pia kumezuka mtindo wa kumzungumza Rais katika Baraza kama kwamba Kanuni hatuzifahamu. Kanuni zetu, Katiba yetu na sheria zinatuongoza vizuri katika kumsema Rais wetu.

Haturuhusiwi kumsema, kumkejeli, kumdhihaki, ile ndiyo *symbol* ya nchi yetu, tumpe heshima yake, tumuone kiongozi wetu pale panapokuwa na kasoro patazungumzwa kwa mujibu wa kasoro za serikali, lakini tufahamu kabisa Rais wetu anafanya kazi ya kututumikia, hapati usingizi mchana na usiku, analitumikia Taifa hili kwa uadilifu mkubwa, tunapomzungumza kiwepesi wepesi hivi haitusaidii. Ni wajibu wetu kumpongeza kwa kazi kubwa anayoifanya na kumtakia kheri na mafanikio.

Mhe. Spika, serikali hii itaendelea kuchukua hatua kwa yeyote anayekwenda kinyume kwa mujibu wa sheria, lakini niseme tu, hakuna waziri mwenye haki ya kumpeleka mtu Mahakamani bila ya kufuata utaratibu wa kisheria, na utaratibu wetu uko wazi kabisa, unapitia kwa Mkurugenzi wa Mashtaka.

Anapopata usahihidi wa kutosha ndio aweze kumpeleka mtendaji au mtu mwengine yeyote aliyetenda kosa Mahakamani, na Mkurugenzi wa Mashtaka atathibitisha ushahidi wake kupitia chombo cha uchunguzi ambao ni Polisi wafanye uchunguzi kutokana na maelezo yanayotoka na ripoti zilizopo, na

pale wanapopata ushahidi unaothibitisha kumpeleka mtu mahakamani ndipo pale ambapo polisi wanapeleka ripoti hizo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka, na Mkurugenzi anachukua hatua.

Kwa hivyo, hakuna anayevumiliwa; ni utawala wa sheria ndio tunaotaka na utawala bora. Leo tumo ndani kesho tutakuwa nje, huo ndio utaratibu wa kawaida tuliojiwekea, huwezi kutumia mamlaka yako ukamuonea mwengine ama ukaenda kinyume na utaratibu.

Kwa hivyo, tunapofuata utaratibu wa sheria tupongezane, sio kuwa hatujafanya wajibu wetu. Pale ambapo lipo kosa kwa mujibu wa taratibu basi tunachukua hatua.

Mimi nataka sana sana kupitia hiki niwapongeze sana watendaji wetu wale wanaofanya wajibu wao kwa kufuata taratibu zilizopo, na wapo ni wengi sana. Kwa hivyo, tunapowachanganya wote tusiwavunje moyo Mhe. Spika, wanafanya kazi yao kwa uadilifu mkubwa sana, na katika hali ngumu sana ya vitendea kazi kimapato na kadhalika. Kwa hiyo, tusi-*categories* kwamba watendaji wote ni wachafu hawafai, hawafanyi hivi. Mimi nataka nichukue fursa hii niwapongeze, na niwaombe waendelee kufanya wajibu wao na wale ambao wanakwenda kinyume na taratibu basi sheria zitachukua mkondo wake.

Pia niwapongeze mawaziri kwa ustahamilivu mkubwa, wanabeba maneno makali Mhe. Spika, yanatoka humu lakini ndio wajibu wa uongozi.

Waheshimiwa Mawaziri wenzangu tupokee, tustahamili, lakini Wajumbe wa Baraza muone pia na yale mazuri tunayoyafanya muyaseme, muyapongeze.

Mhe. Ali Juma Shamuhuna katoa mfano hapa lakini sikusikia kofi, hapa nimepiga peke yangu na kazi ameifanya. Kwa hiyo, zuri lisemwe na baya lisemwe ndio utaratibu. Kwa hiyo, sote lengo letu ni moja, sote ni kutumikia wananchi wa nchi hii.

Mhe. Spika, limezungumzwa sana suala la mishahara hewa. Nataka niwahakikishie Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi wote kwa jumla. Tathmini kubwa sana imefanywa na serikali kutafuta na kuchunguza, ili kuona kila upungufu kwenye suala la mishahara hewa, kurekebisha pale ambapo panapaswa kurekebishwa, na hatua mbali mbali Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe zimechukuliwa katika kurekebisha jambo hili, na zitaendelea kuchukuliwa kurekebisha jambo hili. Hakuna anayefurahia, wala hakuna anayetaka suala la mzaha kweli, na pale inapothibitika hatua za nidhamu na kisheria huchukuliwa kwa wale wahusika.

Kwa hivyo, hakuna atakayefichwa kwenye suala la mishahara hewa, na kazi zinafanywa, na hii kuwa na Tume ya Utumishi Serikalini moja katika wajibu mkubwa inaufanya ni katika kuziba mianya hiyo ya kuwatafuta hao ambao watapata fedha za umma kinyume na utaratibu.

Kwa kweli Tume yetu ya Utumishi Serikalini, Tume yetu ya Utumishi wa Umma imefanya kazi kubwa katika kuchambua na katika kuweka mifumo na taratibu nzuri, na sote tunaona matokeo sasa yanaanza kupiga hatua kwenye suala zima la *promotion* kwenye suala la mishahara, taratibu za kazi, na nia yetu kufanya vizuri zaidi.

Mhe. Spika, kwa hiyo pale jema linapotokea pia napo tuambiwe, isiwe serikali hii chafu hakuna linalofanyika, hakuna umakini. Hayo Mhe. Spika, yapo mazuri, umakini upo na kazi zinafanyika. Suala la

serikali ni sawa sawa na mbio za kijiti, leo tupo sisi tunafanya wajibu wetu na kesho watakuja wengine watafanya wajibu wao huo ndio utaratibu.

Mhe. Spika, imezungumza hapa kwamba tumezila pesa za *MV Spice Islander II,* tumezitafuna fedha zote. Kusema ukweli *ulimi hauna mfupa*, maana katika eneo ambalo tumesimamia kwa ukaribu sana Mhe. Spika, tena nataka nijisifu, kwa ukaribu wa hali ya juu, kuhakikisha fedha hizi zimetumika vizuri, tumefanya kazi hiyo vizuri sana Mhe. Spika.

Tulikusanya shilingi bilioni moja nukta mbili (bilioni 1.2), zilizosaidiwa na wafadhili na wahisani mbali mbali ili kuwapa wale waliokutwa na ajali hii Mwenyezi Mugu wale waliotangulia mbele ya haki awaweke mahali pema peponi, na wale walioathirika kwa njia moja au nyengine awape subira, awape uzima, awaongoze katika mambo yao.

Mhe. Spika, tulikubaliana kwamba waliokolewa walikuwa watu mia tisa na arubaini na moja (941), waliofariki walikuwa watu alfu moja mia tano na ishirini na sita (1526).

Na katika serikali katika kiwango kile cha fedha tukakubaliana kwamba waliookolewa wapate laki nne na elfu kumi na mbili na mia tano (412,500), na wale waliofariki wapate laki tano na elfu hamsini (550,000).

Na utaratibu huu ukafanywa na fedha zikatoka karibu bilioni moja milioni sabini na tisa mia tano na kumi na mbili na mia tano (1,079,512,500). Zilizobakia zilikuwa milioni mia moja sabini na saba (177), na kila hatua ilikuwa inakuwa *reported* katika kikao cha *cabinet* kuonesha hatua zilizofikia na zilizobaki.

Fedha zilizobaki zikatolewa idhini milioni mia moja (100,000,000) twende tukajengee ukuta ule wa fensi kwenye makaburi yale ambayo walizikwa wale waathirika wa *MV Spice Islander II,* na fedha nyengine zilikuwa zinatolewa kwa kufuata utaratibu wa idhini ya serikali.

Kuna maafa yaliyotokea Maziwa Ng'ombe zilitolewa shilingi milioni ishirini na nne (24,000,000), moto uliotokea Jozani zilitolewa milioni sita (6,000,000).

Maafa ya upepo mkali Pemba zilitolewa milioni kumi na nane (18,000,000), ajali ile ya Kilimanjaro II zilitolewa milioni saba (7,000,000), na pesa zilizobaki ni milioni ishirini na tatu (23,000,000), hakuna mtu atakayezigusa au atakayezitumia vyengine bila ya idhini ya serikali na kwa utaratibu wake.

Kwenye ajali ile Mhe. Spika, pesa zote za *operation* zilitolewa na serikali karibu shilingi milioni mia moja (100,000,000) zilitolewa na juu ya hapo zilitolewa pesa za ubani milioni mia moja na hamsini na sita (156,000,000) waliopewa viongozi wetu wa kitaifa kuwapelekea wananchi.

Kwa hiyo, hatuwezi kula fedha za wafiwa, fedha za watu ambao walikusudiwa, wapewe uadilifu huo upo.

Na kama alivyosema Mhe. Ali Juma Shamuhuna, na mimi nataka ku-*challenge* ionekane wapi tumekula pesa hizo. Maana maneno mengine Mhe. Spika, tunatukanwa bure, lazima tufike pahala tuheshimiane, hatukatai kupokea mawazo, wala hatuwi wakali katika kupokea mawazo, lakini tunafanya kwa nia safi.

Tatizo letu tunachanganya siasa hata kwenye mambo ya msingi, ndio tatizo. Akishaonekana hapa Makamu wa Pili wa Rais, basi kuna watani wake watamfuata watamjibu hivi na hivi, hayo mambo tuyaseme kwenye viriri vya kisiasa, kwa sababu tukichanganya siasa kwenye jukwaa hili maisha tutawagombanisha wananchi wetu.

Ni lazima tukae vizuri, tujenge umoja wetu, tushirikiane tujenge nchi yetu kwa pamoja, ili manufaa wayapate wananchi wetu na sote kwa pamoja.

Mhe. Spika, nimalizie kwa sababu ya muda kuna suala hili la Sheria ya Utawala wa Baraza.

Mhe. Spika, nataka nikwambie kabisa kabisa serikali sio leo iliitaka sheria hii jana, na iko tayari kabisa kuhakikisha kwamba sheria hii inafanya kazi, na tuko tayari sheria hii wakati wowote tuilete hapa, lakini muafaka wa pande mbili ufikiwe kati ya Serikali na Baraza la Wawakilishi, kwa nia ya kuwa na sheria itakayoweza kutekelezeka; sheria itakayotenda haki kwa pande zote, na sheria isiyotoa mwanya wowote utakaoleta matatizo mbele katika kufanya kazi zetu.

Kwa hivyo, hakuna anayekataa katika kufanya hivyo Mhe. Spika, wala isiwepo dhana hiyo, inavyotakiwa tuwe na sheria itakayokidhi matakwa na uwezo wa nchi yetu.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, mimi kwa moyo mkunjufu kabisa naunga mkono ripoti zilizowasilishwa hapa Barazani. Ahsante sana. (*Makofi*).

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi angalu kusema machache juu ya hoja ambayo imewekwa mezani.

Kwanza na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake ambazo ametujaalia na leo hii tumekutana hapa.

Lakini la pili kama ambavyo wamesema Waheshima Wajumbe wote na mimi nichukue fursa hii kuzipongeza kamati zote za Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri ambazo wamekuwa wakifanya kwa kipindi chote hiki cha miaka mitano.

Ushahidi wa ripoti hizi ambazo zimekuwa zikiwasilishwa hapa zinaonesha jinsi gani Mhe. Spika, kamati hizi zimekuwa zikifanya kazi nzuri na wizara zao husika.

Ombi langu kwa kamati zote kwamba waendelee na kazi nzuri hizi ambazo wamekuwa wakizifanya ili ule wimbo ambao unaimbwa kila siku wa kuisimamia serikali upate kutimizwa vizuri. (*Makofi*).

Pili Mhe. Spika, naomba niongee kwenye maeneo mawili ambayo yamekuwa yamezungumzwa hapa moja ni hili alilomalizia Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuhusiana na Sheria ya Utawala wa Baraza, na kama alivyosema serikali haina *interest* uwezo wa kuzuia kwa mswada ule kuleta Barazani.

Jengine mwenye mamlaka ya kuingiza orodha zote zinazotakiwa kufikishwa Barazani ni Mhe. Spika, kwa mujibu wa kanuni, lakini tujiulize kwa nini mpaka leo haikuletwa.

Mimi nadhani hilo ndio suala la msingi kwa sababu mengi yamekuwa yanazungumzwa, lakini nadhani Wajumbe wengi hawana taarifa ya kwamba kwa nini mpaka leo Mswada ule haukuwasilishwa Barazani.

Na sababu yake Mhe. Spika, pamoja na kwamba tumekuwa tukizungumza kwa muda mrefu kwenye vikao vya Kamati ya Uongozi, lakini inaonesha hizi taarifa nyingi hazifiki kwa Waheshimiwa Wajumbe. Sasa ile dhana imejengeka kwamba serikali imekuwa haina nia ya kuleta mswada ule.

Mimi naomba Mhe. Spika, niwaambie Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa masharti yaliyomo ndani ya mswada ule haitowezekana kuuwasilishwa mswada ule ndani ya Baraza hili, na kwa sababu gani nasema hivi.

Kwa sababu Mhe. Spika, mswada unapendekeza vifungu ambavyo vinakwenda kinyume na masharti ya Katiba. Sasa unaposoma kifungu cha nne (4) cha Katiba inaeleza wazi kama katiba iwe sheria kuu na hilo nadhani sote tunalijua na halina haja ya kulitolea ufafanuzi, na sheria yoyote itakayotungwa itakwenda kinyume na masharti ya Katiba sheria hiyo itakuwa batili.

Sasa kwa nini chombo hiki kilete sheria ambayo ina- *propose* vifungu ambavyo vinakwenda kinyume na masharti ya Katiba baadae ipitishwe, hilo haliwezekani.

Sasa nini tumekuwa tunafanya Mhe. Spika, muda wote na tokea mimi nipewe dhamana hii kazi moja ambayo nimeikuta mezani ni hii ya Sheria ya  Utawala wa Baraza.

Nashukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma na Wenyeviti wote wamekuwa wakali kwenye jambo hili na Mwenyezi Mungu amrehemu Mhe. Salmin Awadh na yeye ni miongoni mwa Wajumbe ambao wamekuwa wakali kwenye jambo hili.

Lakini tumefika pahali tukakubaliana kama ilivyo haitowezekana kuileta humu ndani. Sasa jambo ambalo hatukukubaliana ni jinsi gani sasa ya kuleta vifungu ambavyo mwenye hoja Mhe. Hamza Hassan Juma, na serikali tutakubaliana kama vifungu hivi ambavyo tutavileta havitakuwa vinakwenda kinyume na masharti ya Katiba. Hiyo ndiyo kazi ambayo tunaifanya Mhe. Spika.

Mhe. Spika, Mhe. Hamza Hassan Juma nimemsikia sana hapa anasema anataka kuileta, vile ilivyo haitowezekana kabisa Mhe. Spika, nadhani yeye analitambua na wewe hilo unalitambua Mhe. Spika, asubiri tukubaliane tufanye hiyo kazi ambayo tumepewa tujiridhishe na baadaye tuilete.

Mhe. Waziri amehakikisha kwamba serikali wala haina nia ya kuzuia mswada huu, kama ni jambo ambalo tumesisitizwa tulifanyie kazi basi mojawapo ni hili kuhakikisha kwamba tunaileta.

Sasa tunaomba Waheshimiwa Wajumbe waelewe hilo, kama hiyo sheria mswada ule wala haukukaliwa na serikali, lakini ulivyo una vifungu ambavyo inabidi vifanyiwe kazi kwanza ili baadaye sasa uletwe humu ndani.

Pili Mhe. Spika, hili ambalo lilikuwa likizungumzwa la kutimiza masharti ya kifungu cha 112 cha Katiba.

Wengi wamezungumza na kila mtu katoa ufafanuzi wake kwa namna ambavyo yeye anaona ndivyo ilivyo, na sisi kama serikali tuna wajibu wetu na sisi wa kutoa ufafanuzi wetu wa jinsi ya kifungu cha 112 kilivyokusudiwa.

Mhe. Spika, huwezi ukasoma kifungu cha 112 kabla ya kusoma kifungu cha 105 na 106 cha Katiba, huo ndio msingi. Kwamba serikali ili ipate kutumia lazima iwe na fedha ambazo zinaidhinishwa na Baraza, hapo ndipo inapopatikana sasa ile *checks and balances*, moja anatumia na akishatumia anakaguliwa.

Sasa kifugu cha 105 na 106 cha Katiba ndio kinaelezea huo utaratibu wa kisheria wa kuwasilisha hayo makadirio na matumizi ya serikali kwa mwaka wa fedha ukishapata ruhusa, maana yake unaambiwa

kuwa wewe sasa utumie na unatumia kwa kipindi cha miezi 12 kinachoanza Julai 1 na kumalizika tarehe 30 Juni.

Unapomaliza kutumia sheria zinakwambia ufunge mahesabu isipite miezi 3, na ripoti yako uiwasilishe kwa *CAG* na ukishaiwasilisha kwa *CAG,* na *CAG* sasa kazi yake ndio hii sasa imeelezwa katika kifungu cha 112 kama yeye sasa anatakiwa kwenda kukagua hesabu zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa na Baraza kwa mwaka wa fedha uliomalizika, na akishamaliza kazi hiyo kifungu cha 112(5) kinamtaka sasa ile ripoti yake aipeleke kwa Mhe. Rais na nadhani kwenye kikao cha Januari Mhe. Rais ametimiza masharti ya Katiba, amemuagiza Waziri wake wa Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora kuwasilisha ripoti hiyo ndani ya Baraza, nadhani imewasilishwa na sote tumeipokea.

Sasa haya mengine yaliyobaki Mhe. Spika, ambayo Wajumbe wengi wamekuwa wanayazungumza, kuna ripoti nyengine Mhe. Hamza Hassan Juma jana ameelekeza hata utaratibu wa kufanywa.

Mimi nasema kama kuna utaratibu mwengine ambao serikali haikuufuata kwa mujibu wa kifungu cha 112(5) basi aliyokuwa nayo hiyo ripoti ailete, maana ripoti hii ni ya *CAG,* na *CAG* ndie yeye anaipeleka kwa Mhe. Rais, na Mhe. Rais anampa Waziri wake ailete Barazani. Sasa kama ripoti iliyoletwa siyo kuna ripoti nyengine ambayo inatakiwa iletwe kwa mujibu wa kifungu hiki, basi iletwe.

Kama masharti ya kifungu hiki hayakutimizwa iletwe, lakini masharti ya kifungu cha Katiba yameshatimizwa, kwa sababu ripoti iliyotakiwa kuletwa imeshaletwa mezani.

Sasa hizi nyengine ambazo Waheshimiwa Wajumbe wanazizungumza utaratibu wake usimezwe kwenye kifungu hichi. Baraza pia limepewa uwezo wa kuidhinisha (*special audit*). Kama kuna jambo ambalo wanaona halikufanyiwa kazi sawa sawa waidhinishe mambo hayo Mhe. Spika, *CAG* akafanye hiyo kazi na akimaliza hiyo ripoti wala haipelekwi kwa Mhe. Rais, kwa sababu siye aliyemtuma. Ataileta hapa hapa Barazani kwa sababu Baraza ndilo lililomtuma. (*Makofi*)

Mhe. Spika, lakini masharti ya Kifungu cha 112 (5) lazima tukubaliane sote kama tayari yameshatimizwa wakati wa kikao cha Januari, ripoti hiyo tumeipokea. Kwa hivyo ile dhana ya kwamba haikuletwa ripoti hiyo, mimi ninadhani tungeiondoa na utaratibu huo ndivyo ulivyo. Unapotumia lazima ukaguliwe na unapokaguliwa ndiyo utaratibu huu wa kisheria ulivyo.

Sasa lazima vifungu hivi tunavyovisoma tuvisome vyote. Huwezi ukasoma kifungu cha 112 (5) ukaacha kifungu cha 112 (3) (a) na (b). Kwa sababu haya ndiyo yote yanaelezea utaratibu huo. Sasa niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe kama wakati wanapotafsiri vifungu hivi vya Katiba basi wawe waangalifu, kwa sababu inapotoka tafsiri siyo sahihi, inawezekana sasa ikazuia mjadala mwengine.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naomba kurudia kuunga mkono hoja hii ya *PAC* kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, ninakushukuru. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Mhe. Hamza Hassan Juma wacha tuendelee na mtiririko. Sasa na mengine Mhe. Hamza tuliitana jana ofisini pale wala haina haja ya kuleta maelezo mengine.

Tunatafuta *the way forward,* jana tulikubaliana na hayo mengine pia nayo niliyatafutia *the way forward* mapema hata kabla ya Mhe. Mwanasheria Mkuu. Ninakushukuru sana Mhe. Hamza.

Sasa ni zamu yake Mhe. Waziri wa Fedha.

**Mhe.Waziri wa Fedha:** Mhe.Spika, kwanza kabisa ninataka nichukue nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe na Wajumbe wa Baraza lako kwa kuchangia kwa ufasaha kabisa ripoti ya *PAC* pamoja na taarifa niliyoiwasilisha. Lakini kabla sijaenda katika kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja, ninataka niseme mambo ya utangulizi.

La kwanza, ninamshukuru sana Mhe. Ali Juma Shamuhuna. Ninamshukuru kwa dhati kwa sababu hoja hii iliibuliwa, Wizarani tunatayarisha kodi lakini hatuwapi wanaohusika na ikatajwa *specific* kuwa tunawatolesha wananchi kodi za bandari kwa utengenezaji wa madawati, lakini hatuwapi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kutengeneza madawati. *(Makofi)*

Ndipo na mimi nilipotoa takwimu zangu nikasema kwamba, "*nendeni mukaiulize Wizara ya Elimu wamezifanyia nini hizo pesa".* Ninamshukuru sana Mhe. Shamuhuna imedhihirika kwamba Serikali haina mzaha pale inapoamua kufanya jambo lake, hatuna mzaha. *(Makofi)*

Jana nilimwambia Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kuwa lengo la Serikali ya Mapinduzi, miaka mitano tuondokane na tatizo la madawati. Na laiti mungenikubalia na Pemba nako niongeze kodi ile, leo kwa idadi hii anayoeleza Mhe. Shamuhuna tungekuwa tupo mbali sana. *(Makofi)*

Ninataka niseme siyo hili tu. Kodi yoyote tutakayoiweka kama Serikali na kusema hii *specific* itakwenda kwa jambo fulani tutapeleka huko. Ninamshukuru sana Mhe. Shamuhuna, ninawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri na ninataka Mawaziri wengine wote itakapokuja dhana kama hii watoe ufafanuzi ili wananchi wasikie na Wajumbe wako waweze kufahamu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, la pili kuwa sina desturi ya kuwachezea, kuwagusagusa, kuwapapasa Waheshimiwa Wajumbe wako, sina desturi hiyo. Lakini kuna baadhi ya Wajumbe wana tabia ya kuwagusa gusa Mawaziri, kuwanyofoanyofoa, wao ukiwagusa wananyanyuka, wanasema utaratibu, taarifa. Leo nitawagusa baadhi yao na nitawagusa kwa sababu ninataka nitoe ufafanuzi wafahamu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi nilidhania kwamba Baraza lako tukufu, Mawaziri tunaposoma wanatusikiliza lakini baadhi yao kumbe hawasikilizi kitu, wanakuwa wapo mbali kabisa. Jana nimeshangazwa sana na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na leo kakimbia hapa. Anaulizwa machungwa manne jumlisha na maembe sita anajibu kumi, haiwezekani. Machungwa na maembe huwezi ukayajumlisha. Mimi ninasoma ripoti aliyoiwasilisha mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* mwaka jana, ninatoa taarifa za mwaka jana na Mwenyekiti wa *PAC* anatoa taarifa za mwaka huu. Huwezi ukajumlisha vitu kama hivyo, hatupo skuli hapa, mimi hata *marks* akinipa moja, mbili, *zero, I don't care*. Mimi nimeshamaliza *master* yangu ya *university*, tena *university* ambazo zinazojulikana duniani. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ninataka Wajumbe tusikilize tunalolisema. Kosa halikuanza kwa Waziri wa Fedha, kosa limeanza kwenye Kanuni yenu hii muliyoitayarisha. Naomba Mhe. Spika, niisome halafu tutairekebisha. Kifungu cha 108 (15), ninasoma,

> "Kila Wizara itapaswa kuwasilisha mbele ya Baraza ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Baraza na ripoti za Kamati hizo kuhusiana na Wizara husika mara moja kwa mwaka katika mkutano wa mwezi Machi isipokuwa ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika itawasilishwa na Waziri anayehusika na fedha".

Halafu bajeti za Wizara munapitisha wenyewe Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, fungu hili litasimamiwa na Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha.

Mimi nilitarajia nije niwasilishe yale ya ujumla lakini yale ambayo yapo *specific* Mawizara wenyewe ndiyo waje wayaelezee hapa. Suala la *Spice Islander* analijua Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, halihusiani kabisa na Wizara ya Fedha na kalitolea ufafanuzi hapa. Hii Kanuni irekebishwe. Waziri wa Fedha aje awasilishe ya jumla halafu Wizara ziende *specific, page 160*. Watendaji wangu wanahangaika, wanaingia ngazi kwa ngazi wanatafutwa kutoka Wizara tofauti, kwa sababu Kanuni yetu imekaa vibaya. Mimi sasa hivi niko huku sasa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimesema katika ripoti ile ambayo Mhe. Omar Ali Shehe aliiwasilisha mwaka jana, nikasema alichunguza ripoti mbili tu. Nimesema katika taarifa yangu. Kwanza aligundua kwamba kuna hoja nimezitaja hapa, kuna hoja ambazo Mhe. Omar Ali Shehe tisini na mbili (92) katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alizigundua.

Katika ripoti ya pili aliyoichunguza aligundua kuna hoja kumi na nane(14). Hoja mia moja na kumi (110), munanitarajia mimi nije nikae hapa dakika kumi na tano nijibu hoja. Nilichokifanya nimezi-*group* zile hoja. Ndiyo nikasema kwamba hoja hizi nimezi-*group* katika makundi haya na nikasema kwamba kwa *detail* zipo katika *document*.

Matarajio yangu Mhe. Spika, kwamba hii Kanuni tutairekebishwa. Ninakumbuka mwaka juzi tulifanya vizuri sana. Kila Waziri mwaka juzi alikuja kueleza *specific* tumefanya nini katika hoja ambazo zipo chini ya Wizara yake.

Kwa hivyo Mhe. Spika, ninataka niwakumbushe tu Waheshimiwa Wajumbe kwamba Mawaziri tunaeleza utekelezaji wa ripoti zilizowasilishwa mwaka jana. Mwenyekiti wa Kamati anapokuja anawasilisha ripoti ambayo sisi tutakuja kujibu mwaka kesho. Ripoti aliyowasilisha Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*, panapomajaaliwa inshaallah itakuja kujibiwa na Waziri wa Fedha atayekuwepo baada ya uchaguzi. Inshaallah nitakuwa mimi Omar Yussuf Mzee na nitakuja kuijibu kwa ufasaha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba baada ya utangulizi huo, sasa nijibu hoja zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wajumbe; zaidi zilizoibuliwa kwenye Kamati ya *PAC* zitakuja kujibiwa muda wake ukifika, lakini nitazitolea ufafanuzi kwa baadhi ya hoja.

Ninataka nikuhakikishie Mhe. Spika, kuna *improvement* kubwa sana ndani ya Serikali. Katika matumizi ya fedha za maendeleo na za kawaida. Tumeingia ndani ya Serikali sisi Serikali ya Umoja wa Kitaifa, tumeanza kuzichambua ripoti za Serikali iliyopita awamu iliyopita na hapa tumechambua *audit report* zilizopita.

Leo ukiisoma ripoti ya *auditor*, kuna *a lot of improvements*. Kama hatuyaoni haya, yale aliyosema Mhe. Waziri Mohammed Aboud Mohammed tunataka kufanya siasa ndani ya Baraza hili. Mimi sitaki kufanya siasa ndani ya Baraza hili. Ninataka nieleze yale ambayo watawasaidia wananchi. Tuna nafasi zetu huko nje, tunaviringe vyetu huko nje vya kufanyia siasa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, Wajumbe wamezungumzia kuhusu habari ya hoja ya marekebisho ya sheria. Nimeeleza kuna sheria nne sasa hivi tumeshazifanyia marekebisho. Lakini kiutaratibu munakwenda nyinyi kama Wizara mukishirikiana na Mwanasheria wa ndani wa Wizara, munapitia ile sheria, munakusanya maoni kutoka kwa wananchi mbali mbali nini kinachotakiwa kurekebishwa ndani ya ile sheria. Baadae inakwenda kwa Kamati ya Uongozi wa Wizara, baadae inakwenda kwa Kamati ya Makatibu Wakuu, baadae inakwenda kwenye Baraza la Mapinduzi, baadae ndiyo inakuja kwenye Baraza la Wawakilishi.

Kuna *process* lakini tayari suala la marekebisho ya sheria tunaliona kweli. Sheria ya Fedha, Sheria ya Manunuzi, kweli zinahitajika kufanyiwa marekebisho. Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii zote hizo tayari tumezipitisha katika uongozi wa Wizara, sasa zinakwenda katika Makatibu Wakuu na baadae kwenye Baraza la Mapinduzi.

Tatizo ni kwamba kikao cha Juni *unless* iwe sheria *emergency* ndiyo tunapitisha sheria, kikao cha mwezi wa sita kinakuwa ni kikao cha bajeti, *otherwise* ninadhani sheria hizi zote zingeweza hata kuja kwenye kipindi hicho. Lakini ni imani yangu tutakaporudi tena katika Baraza lijalo baada ya uchaguzi na inshaallah tutarudi sote humu ndani, sheria hizi tutazileta ili ziweze kufanyiwa mapitio. *(Makofi)*

Suala la madeni kwa taasisi Mhe. Spika, kamati ilitutaka madeni yaliyokuwa hayalipiki tuyafute ili taasisi ziwe na hesabu zake vizuri. Tumepitia madeni haya, siyo suala la kuwa na deni ukalifuta tu, tumepitia deni kwa deni. Kuna madeni mengine wanadaiwa watu binafsi, tumepitia deni kwa deni. Sasa hivi tayari tuna orodha kamili ya madeni ambayo tunataka tuyafute. Nitakuomba sana Mhe. Spika, katika kikao cha bajeti unipe muda niyafute haya madeni kabla hatujaingia kwenye uchaguzi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kudhibiti magendo ya mafuta. Waheshimiwa Wajumbe tumepiga kelele kubwa sana kwenye eneo hili. Lakini ninataka nikuhakikishieni juhudi kubwa sana zinafanywa na watu wangu wa *TRA*. Tunakamata mafuta, tunakamata magari au vyombo walivyobebea mafuta kushirikiana na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. Lakini leo kama mtu anakuja ananyanyuka anasema anauliza tumefanikiwa kudhibiti magendo ya karafuu, kwa nini tushindwe magendo ya mafuta, hatutashindwa. Lakini mwanadamu huyu huyu kila wewe ukimzibia huku, yeye anazibuwa huku. Mpaka leo madawa ya kulevya bado yanaingia humu ndani yanatoka lakini Serikali inajitahidi.

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wanajitahidi. Tuna uchafuzi wa mazingira humu ndani, mwananchi huyo huyo ndiye anayechafua mazingira. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wanajitahidi, lakini mwananchi anachafua mazingira. Tuna usafishaji wa mji Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum SMZ wanajitahidi, lakini mwananchi huyo huyo anachafua miji na huo ndiyo ukweli. Sisi *TRA*, *ZRB* tutaendelea kuwakamata wale wote ambao wanaofanya magendo ya mafuta. *(Makofi)*

Kuna watu walifanya magendo ya mafuta hapa yenye thamani ya Dola tisini elfu. Wakanipigia simu mimi nipo Pemba, "Mhe. Waziri mafuta yangu yamekamatwa", nikamwambia kayakamata nani? *ZRB*, kwa nini kayakamata, mbona yaliopo kwenye vituo vya *GAPCO* hawakamati, aah! maana yake wamenionea tu, walidhania magendo. Nikamwambia unataka mimi nikufanye nini, kwani mimi ndiye niliyekukamata?

Alipomaliza tu simu yake nikawapigia *ZRB*, nikawaambia nikiyaona mafuta hayo vimetoka vichwa vyenu. *Effort* tunazifanya jamani na pale ambapo tunataka kuisifia Serikali, tuisifie na tuipongezeni. Hii ndiyo Serikali yenu, hakuna Serikali nyengine. Mhe. Spika, kwa hivyo suala hili ninasema Wajumbe tushirikiane ili kuweza kukamata zaidi hawa wasafirishaji wa mafuta ya magendo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, iliibuka hoja ya mahoteli kutokulipa kodi ya ardhi kwa baadhi ya mahoteli. Ninataka nikwambieni ndugu zangu, ninashukuruni sana kwa hoja hii na wala haya mahoteli siyo mengi yaliopo Zanzibar. *Hotels and guest houses* tulizonazo Zanzibar karibu mia mbili na kidogo hivi. Nitamuomba sana Mhe. Waziri mwenzangu, Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati tufanye kazi ya kupitia moja baada ya moja watupe na stakabadhi zao za kulipia ardhi, tutafanyakazi hiyo na watendaji wetu. Nataka niseme hapa kwenye chombo chako Mhe. Spika, nikimkamata mwenye hoteli halipii ardhi na hana barua ya waziri kwamba amepewa msamaha wa miaka fulani tutampandisha mahakamani. Hili hatutanii kabisa, tutampandisha mahakamani na kazi hiyo tutaifanya mimi na waziri mwenzangu, kwa sababu ni wajibu wetu.

Mhe. Spika, jengine ambalo liliibuliwa ni ubadhirifu katika matumizi; hapa na mimi nataka niseme kidogo. Mhe Spika, with *due respect*, nawaheshimu wana Wajumbe wa Baraza lako tukufu kama ripoti zetu hazijamtaja mtu basi sisi tusimtaje, tulinde ile *the human right* haki ya mwanadamu tuilinde, isiwe sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ndio tunavunja haki ya mwanadamu.

Kama ripoti imewataja watendaji fulani na fulani wacha tu watu waseme. Kama ripoti haijamtaja mimi naona tabu sana sisi kuweza kumtaja. Inawezekana kafanya vitendo hivyo na inawezekana hajafanya vitendo hivyo. Lakini sisi tunamtangaza kwa wananchi, ule uhuru wake tunaupoteza, ile amani yake tunaipoteza. Mimi naomba sana Mhe. Spika, tusifanye hivyo, tutazingatia suala la ubadhirifu ili kila Katibu Mkuu aliyepewa dhamana ya kusimamia ubadhirifu, basi aisaidie Wizara ya Fedha. Katibu Mkuu kapewa dhamana ya kusimamia matumiziya fungu lile atusaidie sana.

Ripoti ya mishahara hewa, nadhani hili sina haja ya kulielezea, Mhe. Mahammed Aboud kalitolea ufafanuzi sana na Mhe. Mwanasheria Mkuu amejaribu kulielezea kwa mujibu wa katiba. *CAG* nyinyi mnaweza mkamtuma, lakini nimeshangaa sana wajumbe tumesimama hapa hatujamtuma *CAG* atuchunguzie matumizi ya mfuko wa jimbo, hatujamtuma, tunatuma huko kwengine tu. Wengine hapa mnakwenda mnatumia hamrejeshi, wengine mnarejesha risiti hewa. *CAG* sasa nitamtuma mimi achunguze matumizi ya mfuko wa jimbo. *(Makofi)*

Nitamwandikia *official CAG* achunguze matumzi ya mfuko wa jimbo. Isiwe sisi watunga sheria hatuchunguzwi, hatuna mamlaka hayo kwenye katiba na sisi tunatakiwa kuchunguzwa. Nitamwandikia mwenyewe *CAG* achunguze mifuko hii ya majimbo, halafu aniletee taarifa na mimi kwa kila jimbo. Tutakuja kuiweka wazi hapa ili wananchi wasikie.*(Makofi)*

Mhe. Spika, limekuja wazo hapa watendaji wasiokuwa na elimu wapatiwe mafunzo, nimelipokea na hasa wale wa *ZRB* na taasisi nyengine vile vile. Lengo letu ni kuwapa mafunzo watendaji wetu, ili kila mtendaji aweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, maeneo ya historia tumeambiwa tuyatunze, ili yaweze kutusaidia kutupatia mapato. Wazo sio baya ni zuri, kila lililokuwa zuri Mhe. Spika, nimelichukua na tutajitahidi sana na mimi nitawashawishi wenzangu waweke bajeti angalau tuweze kufufua moja baada ya moja, hata kama hayatupatii mapato. Wenzetu wanaotoka nje tunaowaita watalii, wanapoingia ndani kuja kuona historia yetu inatusaidia sisi kututangaza nje. Nitawashawishi wenzangu sana tuweke bajeti katika maeneo haya, licha ya kuwa hali yetu sio nzuri, tuweze kufufua moja baada ya moja awamu kwa awamu.

Mhe. Spika, kabla ya kumalizia lilielezwa vile vile uhaulishaji wa fedha. Nataka niseme uhaulishaji wa fedha una daraja mbili. Daraja la kwanza ni wizara yenyewe wanapoona kwamba mahitaji ya fungu hili au fungu hili linahitajika pesa na huku ziko za kutosha nihaulshe nitumie huku. Baada ya kuridhika wanampelekea waziri wao ili waziri naye aridhika, ananiandikia mimi, na mimi Waziri wa Fedha naruhusu uhaulishaji huo ufanyike.

Mhe. Spika, mimi namtarajia waziri zaidi atafahamu uhaulishaji ule kwa nini zinahitajika, kuliko hata kunitarajia mimi, kwa sababu yeye yuko karibu na mfuko wake, karibu na watendaji wake, anaweza akawauliza na anaweza akapata majibu kwa ufasaha zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka niseme na mimi nitajitahidi sana katika eneo hili, kabla sijatia saini nitawapigia mawaziri wenzangu, ili niwaulize kama wameridhika na huo uhaulishaji kabla hatujahaulisha. Lakini sambamba na hili, nataka niwaambie zile taasisi ambazo wanafunga hesabu wakabakisha pesa wakaziweka katika *account* nyengine, badala ya kuzirejesha, hilo ni kosa. Nawaomba sana wasifanye hivyo.*(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka nimalizie kwa kusema moja sasa. Mhe. Spika, wenzangu walisema juzi, nilizungumza na wakanipongeza sana, lakini jana walivunjika moyo. Msivunjike moyo. Juzi nilichokuwa nakifanya nawasilisha taarifa ya wizara yangu, ni taarifa ambazo nazijua kwa ukamilifu na nilichokuwa nakifanya juzi nawasilisha utoaji wa fedha, kitu ambacho nakijua kwa ukamilifu nani kapata nini na nani hakupata nini, ndicho nilichokuwa nakiwasilisha na nilichokuwa nina uhakika nacho. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jana mlinipa kazi ya kuzungumza mapotevu na matumizi ya taasisi tofauti. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba mawaziri wanaohusika na sekta zao walikuwa na nafasi na uwezo mzuri zaidi wa kuzungumzia upotevu kama upo katika sekta yake kuliko hata mimi. Ndio maana nasisitiza tubadilisheni kanuni, ili tutowe nafasi kwa kila waziri tutamjua, huyu waziri anasimamia kweli upotevu ndani ya taasisi yake au hasimamii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakuomba sana tena nakuomba sana Baraza lijalo tuwe tuna kanuni mpya, yamo mengi humu ndani yanatakiwa kurekebishwa, ili tuweze kuwa- *accommodate* mawaziri wenzangu. Mimi kama Waziri wa Fedha nije nitowe ya jumla, yale ambayo tuliyoyaona serikalini, lakini yale *specific* tutowe nafasi kwa mawaziri wa sekta. *(Makofi)*

Nataka nikuombe tena Mhe. Spika, wakati tunawasilisha hizi taarifa za kamati, tutowe muda mzuri zaidi, tungejitahidi sana kupunguza miswada ya sheria, tukatoa muda mzuri kwa kamati ili na serikali nayo isikike imetekeleza nini. Hivi unavyonipa mimi dakika 30 au dakika 15. Kwa kweli na sisi huwa hamtutendei haki. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima nataka niseme tu kwamba nimeyapokea yale yote ambayo Waheshimiwa Wawakilishi wameyaazungumzia, na tutayafanyia kazi. Nimemuona Shemegi yangu Mhe. Makame Mshimba hapa ameingia, lakini amekwepa matope na yeye na kuna mvua huko. Tutayafanyia kazi kwa uadilifu mkubwa sana. Lengo letu ni kuona kwamba hakutakuwa na upotevu wa aina yoyote ndani ya serikali.

Lakini *with new recruit*, wafanyakazi wetu wana maadili tofauti, wafanyakazi wetu wanatamaa tofauti na wewe kila mwaka *as a Government* una *recruit* wafanyakazi wapya, unawaingiza, wengine wanatoka. Kwa hivyo, hili zoezi litakuwa ni endelevu, *it is continuous*. *(Makofi)*

Nataka niwaambieni Mhe. Spika, na wajumbe tumepiga *progress* nzuri sana hata ripoti tulipokuja tukazipitia, sisi huwa tunazilinganisha na mwaka jana na mwaka uliopita, lakini tutajitahidi sana. Wenzangu wameelezea hapa *process* za kumshtaki mtu, Waziri wa Fedha hana mamlaka ya kumshtaki mtu. Hakuna pahala hata pamoja katika sheria zetu. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk jana alisema, angefurahi angesikia kwamba Waziri wa Fedha kampeleka mtu mahakamani, sina mamlaka hayo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu nimemuuliza hapa mimi toka jana, anioneshe sheria moja inayosema kwamba Waziri wa Fedha ana mamlaka ya kumshtaki mtu, hana hata moja. Lakini mimi mamlaka yangu ni kuhakikisha kwamba ninatoa taaluma kila siku kwa wahasibu na watendaji wetu, wapunguze na hatimaye kuondokana kabisa na ubadhirifu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi naamini sana *the day will come*, hili suala la ubadhirifu litakuwa ni historia. Kila mmoja ataweka risiti zake kwa uangalifu na hakutakuwa kwamba amekwenda *CAG* hajakuta risiti, baadaye inakwenda kamati risiti zipo. Hiyo sio *ethic* ya Uhasibu, *once* uki- *purchase one item* unatakiwa uweke *documentation* zako *in a proper place*. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimesema sana, nia yangu ni kwamba chombo chako hiki kiwe more *educative*, kielimishe zaidi kuliko kuwa ni chombo cha siasa. Najua mwaka huu wa uchaguzi, CCM tunataka kuendelea kukaa ndani na *CUF* wanataka kututoa nje. Kama wavuta kamba, huyu anataka kumvuta ndani na huyu anataka

kumtoa nje. Ni imani yangu kwamba tuwaachie wananchi wenyewe, sisi humu ndani tusifanye siasa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kuwasilisha na ninawashukuru tena wajumbe wote. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri wa Fedha tunakushukuru sana. Nilitaka niseme jambo moja tu kabla sijamkaribisha Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*. Waheshimiwa Wajumbe, kanuni zetu ni kitu ambacho kina uhai, kwa maana tunaweza tukarekebisha kila pale tutakapoona pana haja ya kurekebisha.

Hivi tunavyozungumza kuna mradi maalum wa kupitia kanuni hii, ili turekebishe. Hili ambalo Mhe. Waziri wa Fedha ameniomba sana, nimeshaelekeza mapema kwamba kila waziri abebe mzigo wake. Haziwezi zikatafunwa pesa sehemu nyengine na tukamtaka atowe maelezo huyu hapa, wakati mtafunaji yupo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, yule aliyetafuna ndiye atakayeeleza ametafuna vipi. Hilo Waheshimiwa Wajumbe wangu linafanyiwa kazi, ili kurekebisha hilo, kwa sababu na mimi nililiona nikasema hii sio halali, kwamba ubadhirifu umefanyika kwengine, ajibu mtu mwengine, basi atajibu mwenyewe.

Baada ya machache hayo sasa nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya PAC. *(Makofi)*

**Mhe. Omar Ali Shehe: (Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*):** Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena naomba nikushukuru kwa kunipa wasaa huu wa kuweza kusimama mbele ya Baraza lako hili, kwa lengo la kufanya majumuisho juu ya hoja zile zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe, tangu jana wakati tulipoanza kujadili ripoti hii ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika.

Mhe. Spika, baada ya kukushukuru naomba sasa niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote ambao walichangia hoja hii na ambao walisikiliza kwa makini hoja hii lakini hawakupata fursa ya kuchangia. Naamini wako wengi walitamani sana kuchangia, lakini kwa tatizo lile lile la muda, ambalo hata Mhe. Waziri wa Fedha kapendekeza kwamba tupate muda zaidi, ni jambo muafaka sana, kwa sababu katiba yetu inalitaka Baraza kusimamia serikali. Pahala ambapo tunaweza tukasimamia serikali ni katika utendaji wa shughuli za serikali na ambao ni kupitia ripoti zetu za kamati.

Kwa hivyo, mimi nakubali na naafiki kabisa kwamba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wapate muda zaidi wa kujadili ripoti za kamati kwa sababu ndio pahala pekee unapoweza kupata kipimo cha utendaji wa serikali kwa mwaka mmoja.

Mhe. Spika, naomba niwatambuwe wale waliochangia, ambapo kama kawaida alianza;

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk;
2. Mhe. Hija Hassan Hija;
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu;
4. Mhe. Fatma Mbarouk Said;
5. Mhe. Subeit Khamis Faki;
6. Mhe. Hamza Hassan Juma;
7. Mhe. Marina Joel Thomas;
8. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad;
9. Mhe. Abdalla Juma Abdalla;
10. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali;
11. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;

12. Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali na;
13. Mhe. Waziri wa Fedha.

Mhe. Spika, ukweli ni kwamba zaidi ya asilimia 80 ya michango iliyotoka, ilikuwa ni michango ya jumla ambayo wote waliungana na kamati katika kueleza masikitiko na lawama mbali mbali kwa serikali, juu ya utekelezaji wa ripoti na mapendekezo ya ripoti ya kamati yetu ya *PAC*.

Kwa hivyo, ni asilimia ndogo tu ambayo ilikuja na mchango wa maswali pamoja na kutaka ufafanuzi. Naomba nianze kujibu yale ambayo Waheshimiwa Wajumbe, ama waliuliza kama maswali au walitaka ufafanuzi.

Kwanza naomba nimjibu Mhe. Hija Hassan Hija ambaye alitaka kujua inakuwaje inatokea wizi hasa katika eneo la viinua mgongo, wakati ambapo mchakato wa kumlipa mfanyakazi aliyestaafu unahusisha taasisi kadhaa.

Ni kweli Mhe. Spika, tulisema kwamba mchakato wa kumlipa mtu aliyestaafu unapita katika sehemu tatu kubwa.

1) Taasisi aliyotokea, husika na suala zima na kutoa taarifa muhimu kuhusiana na mstaafu, kama vile tarehe ya kuajiriwa, mshahara wa nyongeza na mshahara wake wa mwisho.

2) Taasisi ya pili ni Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo inajukumu la kusahihisha na kuthibitisha juu ya uhalali wa malipo yaliyohitajika.

3) Taasisi ya tatu ni ile inayofanya malipo ambao ni Wizara ya Fedha.

Mhe. Spika, yaliyotokea ni kama nilivyosema ni niya ovu ya baadhi ya watendaji ambao sio waaminifu, hucheza mchezo na yule ambaye ni mstaafu. Hapa basi taasisi inayohusika kwanza ni taasisi yake muajiriwa ambayo ndiyo inayotoa taarifa sio sahihi. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ndiyo inayotakiwa ithibitishe. Kwa hiyo huku taasisi ya kwanza inaweza ikatoa taarifa lakini Mdhibiti katika kufanya uhakiki wake akathibitisha au akahakiki akaona hili ni kosa.

Linapotokea hivyo kwa kweli Mdhibiti hutakiwa arejeshe jalada lile kwa ofisi inayuhusika, ili kufanyawa usahihi. Sasa kosa linapotokea ni mashauriyano kati ya muajiriwa ambaye ni mstaafu pamoja na maofisa wa taasisi yake, pamoja na maofisa wa CAG, pale ndio mara nyingi mchezo unapochezwa.

Kwa hiyo ile Wizara ya Fedha huwa haihusiki sana, kwa sababu Wizara ya Fedha anachotakiwa kufanya ni kile alichoagizwa na Ofisi ya CAG kwamba lipa. Sasa akishaambiwa lipa Wizara ya Fedha kazi yake huwa amejiridhisha kwamba Mdhibiti amefanya kazi nzuri na yeye hulipa. Sasa mchezo hutokea sehemu hizo.

Kama ilivyo kwa pendekezo la Kamati tumependekeza ili kuondokana na tatizo hili basi ni vyema kuwe na *database* ya wafanyakazi ambayo kwa kweli taasisi zote zinazohusika, wizara zote zinazohusika pamoja na Ofisi ya Mdhibiti na Wizara ya Fedha watakuwa na *access* ya kuona taarifa zote zinazohusu muajiriwa. Nadhani tukifikia hatua hiyo huu mchenzo mchezo kama huu unaweza ukapungua ama ukaondoka kabisa.

Mhe. Spika, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, alitoa lawama kidogo kwamba Kamati haikuwa makini sana hasa katika kutoa mapendekezo yanayohusiana na lile lilotokea katika *treasured* ile ya MV. Spice.

Mhe. Spika, kwanza mimi nataka niseme kwamba hapa hatufanyi siasa. Kwa masikitiko sana mimi nasikitika kwamba ikiwa tutazungumza kwamba hoja za Mdhibiti na mapendekezo ya Kamati pamoja na mchangio wa Wajumbe ni siasa binafsi mimi nitasikitika sana. Kwa sababu ni sawa na kwamba sasa tunataka kupotosha umma, hatupotoshi umma.

Mhe. Spika, kinachozungumzwa hapa kwamba hiki kimeibiwa ni wajibu wa Mdhibiti aseme kwamba hapa pameibiwa au hapa pametokea hitilafu. Ni wajibu wa Kamati kufanya uchunguzi na ni wajibu wa Wajumbe waseme kwa hisia kali. Ni lazima tuseme kwa hisia kali, hatutaki ku- *politicize* mambo haya kwamba CUF tunataka iingie CCM itoke, hapana hayo ni mambo ya mchezo huko nje. Humu tunachozungumza ni pesa za walipa kodi zinatumika vipi.

Mhe. Sika, kwa hivyo hii isizungumzwe kabisa, mambo ya siasa siasa ni nje. Hapa mwizi ataitwa mwizi, mwizi hatoitwa shekhe. Hatuwezi kubadilisha jina wala hatuna taminoji nyengine ya mwizi kumwita shekhe hapa, mwizi ataitwa mwizi tu. Tukimwita mwizi hiyo siyo siasa, huo ndiyo uhalisia.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe mnatoka nje tukielewa kwamba akimaliza Mwenyekiti tu tunapitisha hoja hii. Sijui utaratibu huu unatoka wapi, tuliyokuwepo nje turudi ili tumalize hii kazi. Mheshimiwa endelea.

**Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*):** Mhe. Spika, mimi nadhani kwa kweli tusitumie hili twenda kwenye hoja mahsusi na tuseme lile lililotokea na vile ambavyo serikali inataka kujibu, ili mwisho wa siku tuone ukweli uko wapi na kodi za wananchi zinatumikaje.

Mhe. Spika, tulichokiona hapa ni kweli kwamba Mdhibiti alitoa ripoti na yeye akaeleza na Kamati ilikwenda kukagua na ikathibitisha kilichotolewa kwamba utaratibu wa malipo haukuwa sahihi. Tukiangalia ripoti tutaona mambo yako *clear* kabisa. Unapopata *list* ya malipo na ikawa wengine wanatia saini kwa madole magumba, wengine hawakutia saini au wengine wanatumia dole la siri kama ilivyoelezwa hapa katika ripoti zilizopita. Sasa hilo ni suala la uchunguzi.

Maana yake Kamati inaletewa kwamba pungufu ni hili. Kamati ya Uchunguzi maana yake sasa inatakiwa iende mbali zaidi ichunguze, kwamba hata hilo dole lilikuwa ni dole gani, kwani madole nayo yanakuwa na *detection* maalum ya kujua kwamba unaweza kwa mambo haya ya madole mtu mmoja akatia madole *list* zote.

Mhe. Spika, hayo ni mambo yanayohusiana na uchunguzi na ndiyo maana Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Mahesabu ya Serikali kama lilivyo jina lake ilitakiwa ifanye kazi zaidi ili iende mbali kwa kujiridhisha kwamba watu walioweka madole katika *list* zile ni madole sahihi na yanahusika na watu tofauti.

Mhe. Spika, labda inawezekana kwamba Kamati mapendekezo hayakuridhisha lakini bado narudia niseme kwamba Baraza hili lina nafasi ya kuweka mapendekezo. Kama ikiwa mapendekezo hayakukidhi haja, bado Baraza lina nafasi ya kutoa tena mapendekezo zaidi. Kwa sababu kitendo cha kuwaibia marehemu, kitendo cha kuwaibia watu waliojeruhiwa ni kitendo kibaya sana.

Mhe. Spika, ni jukumu la Baraza lako lione litafanyaje katika hoja ile lakini kamati imefikia katika upeo ule na kwa nafasi iliyopewa na muda uliopewa na Baraza.

Mhe. Spika, Mhe. Hamza Hassan Juma yeye alieleza hoja ya kwamba Kamati ya PAC ingelikuwa ina nafasi zaidi ya kuchukua hatua.

Mhe. Spika, Katiba yetu kifungu cha 112 kiko wazi. Mimi binafsi ninavyoamini na kwa mafunzo niliyopewa katika Kamati hii na sehemu mbali mbali nilizotembea katika kuishughulikia Kamati hii, nimepata uzoefu kwamba ripoti zote za kawaida na ripoti zote maalum ukaguzi maalum zinatakiwa ziwasilishwe Bungeni.

Mhe. Spika, hii ndio *best grates* kwa Mabunge yote, kwamba ripoti ya kawaida na ripoti ya ukaguzi maalum hupitia tu mikononi mwa Rais lakini mwisho wake huletwa Barazani au huletwa kwenye Bunge ili wananchi wakaona nini kilichotokea.

Mhe. Spika, Baraza lililopita nakumbuka Waheshimiwa Wajumbe wengi pamoja na mimi tuli-*raise* hoja hii na serikali kupitia Waziri wa Nchi, Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Dk. Mwinyi waliahidi kwamba ripoti italetwa Barazani. Mimi binafsi niliitegemea sana kwamba ripoti ingeliletwa katika Kikao hiki. Bahati mbaya kwamba haikuletwa.

Kama Mwenyekiti wa Kamati na nilitoa hoja Mhe. Spika, niliandika hoja binafsi kama Mwakilishi, kwamba ripoti ile naiyomba serikali ilete hoja. Bahati nzuri Mhe. Spika, kwa hekima zako ukanambia kwamba haitowezekana. Ulinipa sababu kwamba serikali italeta ripoti, kwa hiyo hakuna haja ya kuendeleza hoja binafsi kwa sababu serikali italeta ripoti. Lakini bahati mbaya leo ama kesho, keshokutwa tutamaliza Baraza hili ripoti haipo.

Mhe. Spika, nasema kwamba kwa mamlaka yangu kama Mwenyekiti, au kwa mamlaka yangu kama Mjumbe upeo wangu ni kuomba tu kupitia hoja binafsi na kwa sababu hilo lipo kwenye mchakato baadaye tutaona tutafanyaje. Lakini Mhe. Spika, hakuna sababu yoyote lazima ripoti iletwe. Ili kama Wawakilishi wa wananchi tuone nini kilichomo na wananchi wetu waone nini kilichomo. Hoja yangu ni ile ile kwamba serikali kupitia mishahara hewa kwa mwezi inapoteza zaidi ya bilioni 1.8 na zaidi.

Mhe. Spika, mjadala wa Wajumbe ulilenga mambo mbali mbali, lakini kuna mambo ambayo yaliguswa sana. Kutokana na majadala wa Wajumbe naomba mambo yafuatayo kwa sababu yalitawala mjadala. Kwanza ile ripoti ya ukaguzi maalum wa ZUSP ufanywe ukaguzi maalum kuhusiana na mradi wa ZUSP.

Mhe. Spika, la pili naomba ufanye Baraza lako liazimie kufanywe kwa ukaguzi katika ule mradi wa *E-Goverment*. Lakini Mhe. Spika, naomba Baraza lako vile vile liazimie kwamba ripoti ya ukaguzi wa mishahara hewa, pamoja na ile ripoti ya ukaguzi wa *ZMA* iletwe katika Baraza hili katika kikao cha bajeti. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba niseme kwamba hatupingani wala hatukinzani kuhusiana na hoja ya serikali ya kuitoa Kampuni ya *Philtex* sio hoja yetu. Hoja yetu ni fedha zilizotumika katika kipindi hicho tangu mwaka 2004, tangu ule mradi ulipoanza, ziko wapi? Naomba nirudie Mhe. Spika, hoja yetu sio namna gani serikali imempa nani, sio hoja yetu, serikali mwisho wa siku ina uwezo wa kumpa yeyote yule. Lakini hoja yetu ni fedha zilizoingia serikalini zimetumikaje katika kipindi chote kile ambacho *Philtex* ilikuwa katika *operation*. Kwa hivyo, tunaomba ripoti hiyo iletwe, ili mwisho wa siku tuone tunafanyaje.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naliomba Baraza lako hili wakati litakaporidhia kupiga kura kuipokea ripoti hii basi liridhie pia na maazimio haya matatu ambayo leo nayawasilisha katika kikao hiki.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Fedha kaeleza vizuri na pamoja na marekebisho ya kanuni, lakini naomba na mimi niseme kwamba napendekeza ripoti ya *PAC* iwe ni ripoti ya mwanzo katika mjadala na ripoti nyengine za kisekta zifuate baadaye. Katika muktadha ule ule wa kwamba tuwe na muda zaidi pamoja na marekebisho mengine kwamba na mawaziri husika na wao wajibu.

Kwa hivyo, napendekeza Mhe. Spika, ripoti ya *PAC* iwe ni ya kwanza na hii ni *best practice* kwa Mabunge yote, kwamba ripoti ya *PAC* ndio inayoeleza namna ya makusanyo na namna ya matumizi. Sasa tutakapokuwa tunazungumza ripoti ya *PAC* mwisho wakati ripoti za kisekta zimepita, tunakuwa tunaleta faida gani. Mimi nadhani tungetanguliza mwanzo ripoti ya *PAC*, baadaye ndio ripoti za kisekta kwamba tutakapozizungumza tutajua kwamba haya mambo yamekwendaje.

Mhe. Spika, naomba niseme kwamba niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe, serikali ni kodi na bila ya kodi hakuna serikali popote kule duniani. Mhe. Spika, tunaposema serikali ni kodi tunamzungumza mwananchi, mwananchi ndiye anayetoa kodi na mwananchi ndiye anayepaswa kutumia kodi, huduma za serikali ndio matumizi ya kodi kwa mwananchi, maana yake ni *circle* kwamba mwananchi hutoa kodi ika-*reverse* kuwa ni huduma kurudi kwa wananchi.

Kwa hivyo, tunapozungumza suala la kodi tunamzungumza mwananchi, na tunapozungumza kodi ni mwananchi katika kutoa na katika kupata huduma kutoka kwa serikali. Hapa ndipo maana wale wataalamu walioanzisha mifumo hii wakaliweka Bunge kama ndio msimamizi wa serikali katika masuala haya, kwamba lazima serikali isimamiwe katika kutoza kodi na lazima serikali isimamiwe katika kuhakikisha kwamba inarejesha kodi kwa wananchi, hiyo ndio mantiki yake. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wajumbe, tumekuwa tukilalamika lalamika. Hivi mwenye dhamana hasa ya kuisimamia serikali ni nani. Wenye dhamana ya kuisimamia serikali katika ku-*regulate* kodi na katika kuhakikisha kwamba serikali inarejesha kodi ni sisi wawakilishi, sasa kama tangu tunalalamika wizara haitekelezi maagizo, wizara inadharau. Wenye jukumu la kuisimamia serikali ni sisi, serikali popote duniani ina kawaida ya kuwa na kibri, kwa sababu serikali ina majeshi, serikali ina polisi na kila kitu na ndio maana kukawekwa Mabunge ili kusimamia serikali ili iondokane na vitu kama hivyo. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Spika, kama serikali hai-*perform* vizuri, mimi nadhani wa kulaumiwa ni hili Baraza letu. Kama serikali ina kibri wa kulaumiwa ni Baraza letu, kama serikali inajibu majibu ya ovyo wa kulaumiwa ni sisi wawakilishi, kwamba tumeshindwa kuisimamia serikali na tumeshindwa kutekeleza majukumu yetu. Kipimo kiko wapi wananchi wenyewe mwisho wa siku ndio watakaosema kwamba wewe rudi, wewe usirudi na wewe rudi, wewe usirudi kwa sababu kipimo ni wananchi.

Mhe. Spika, naomba tena niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe, kwamba sisi wajumbe tuna wajibu pamoja na yote. Lakini tuna wajibu wa kuona fedha zimetumika kama tunavyofanya, kwamba fedha zimetumika kwa hiki na hiki, lakini hatutakiwi tuishie hapo tu, tunatakiwa tujuwe fedha zimetumikaje. Hili neno zimetumikaje ndio neno la msingi sana kwa upande wetu Mhe. Spika. Lakini si hilo tu, tunatakiwa tujuwe je, taratibu zimefuatwa. Hizo ndio hoja za msingi, fedha zimetumikaje na je, taratibu zimefuatwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nikitoa mfano kwa hii hii Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Jana Mhe. Waziri wa Fedha alituambia kwamba kwa mujibu wa takwimu alizotupa ni kwamba fedha zilizokwishatolewa katika mradi huu wa madeski, ambao tulikubali kwamba watu wapate tabu katika kukatwa wakati wanaposafiri, ni jumla bilioni 4,393,000,000, kwa mujibu wa idadi aliyotupa Mhe. Waziri wa Fedha. Sasa kama hivyo ndivyo kama ni bilioni 4,393,000,000 zimetumika, namshukuru Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali leo katupa taarifa.

Mhe. Spika, katika taarifa yote ile aliyotupa ununuzi wa viti, meza na ma-*desk*, kama tutapiga hesabu kwa vitu vyote kwa skuli zote alizotupa, tuchukuwe kwamba kati ya vitu vile chenye gharama kubwa zaidi ni kipi. Mimi nasema ni *desk* tulipata *item* alizozitoa ni shilingi 6,401/= vyote vile na kilichotumika ni bilioni 4,393,000,000, sasa niwarejeshe kwenye hoja je, zimetumikaje. Ukigawa hapo utapata kila *item* imetumia shilingi 6,086,000 kwa kila *item* moja kwa hesabu iliyotolewa, maana yake ikiwa kama ni meza

au *desk*. Tuchukuwe desk, kati ya hesabu hiyo tutapata kwamba kila *item* imetumia shilingi 600,000 kila desk moja limechongwa kwa shilingi 6,086,439/= hiyo ni haki au hiyo ni sawa.

Sasa Waheshimiwa Wajumbe tunasema kwa vyovyote vile hapa panajengeka wingu la shaka. Tunataka sasa tujiridhishe na hili Mhe. Spika, kwa hivyo kama ulivyoagiza kwamba muhimu tujuwe fedha iliyotumika ni hii na je, taratibu zimefuatwa au hazikufuatwa. Taratibu za ukandarasi zimetolewa vizuri, zimetolewa kwa mujibu wa sheria na kadhalika.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nataka niseme neno moja tu la kumalizia. Mhe. Spika, Zanzibar ni nchi ndogo sana na uchumi wetu ni mdogo sana kwa kweli, nchi yetu kwa namna hiyo Mhe. Spika, haimudu hata siku moja kutokea ubadhirifu na wizi kama huu. Wenzetu wanavyozungumza bilioni 6 na bilioni 200 wao inawezekana uchumi wao hautingishiki, lakini sisi tunaposema kila mwezi zinapotea bilioni 1.8 kwa kupitia *item* moja tu ya mishahara Mhe. Spika hii *is a big chaos* katika nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja, nakushukuru. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana kuna taarifa. Mhe. Waziri wa Fedha.

**TAARIFA**

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, nataka nitowe taarifa ndogo tu. Hili suala la madawati lisimsakame Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Wajumbe warudi nyuma wafahamu. Kulikuwa kuna kodi unalipia shilingi elfu moja, nikaomba niongezee shilingi elfu moja ili niipeleke kwenye madawati. Kodi sasa hivi ni shilingi elfu mbili kutoka Zanzibar kwenda Dar-es-Salaam, lakini katika hizo shilingi elfu moja tu ndiyo inayokwenda kwenye madawati.

Mhe. Spika, alichokizungumza Mhe. Ali Juma Shamhuna na alichokizungumza Mhe. Omar Ali Shehe ile ni nusu yake ndiyo inayotakiwa kwenda kwa Mhe. Ali Juma Shamhuna, wasimzonge bure Mhe. Ali Juma Shamhuna. Lakini waende wakafatilie kama mwenyewe Mhe. Ali Juma Shamhuna alivyokuwa amesema.

**Mhe. Spika:** Asante sana kwa taarifa.

**TAARIFA**

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, nakubaliana na hoja ya kaka angu Mhe. Waziri wa Fedha. Lakini juzi baada tu ya kaka angu kutoa elimu kubwa ya kodi na mapato yaliyopatikana nilitafuta *Hansard* ya Mhe. Waziri wa Fedha na ninayo hapa na ndio maana tunatumia *Hansard*.

Mimi binafsi kama Mjumbe wa Kamati ya Fedha naamini yale ya juzi aliyozungumza Waziri wa Fedha ni sahihi. Namuamini yeye ni mtaalamu na ana uwezo mkubwa na Wizara yake ina uwezo mkubwa.

Paragrafu moja ya Mhe. Waziri wa Fedha alisema hivi: ‘’Kodi iliyopangwa iliyokusudiwa kutolewa ni bilioni 2.2454. Lakini hadi mwezi uliopita nimewapa zaidi ya bilioni 2.5539 sawa na asilimia 113’’, paragrafu ya kwanza.

Paragrafu ya pili akasema mwaka huu kodi iliyokusudiwa ni bilioni 2.84, Wizara ya Elimu nimeshawapa bilioni 1.84 hadi mwazi Februari 2015. Kwa hiyo 2.5539 + 1,84 = 4.39 bilion. Kwa hoja hiyo madawati ambayo Waziri amechongesha hata kama yote ni madawati ni 6401 maana yake nini. Maana yake 4.34 bilion ukigawa kwa dawati moja tusiseme viti, dawati moja ndiyo gharama kubwa, ni laki 686 ndio tunasema *valume for money* ipo.

## TAARIFA

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, namshukuru sana ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija, hiyo taarifa si niliitoa miye na miye ndiye niliyesahihisha kusema nusu ya hizo. Kwa sababu ya shilingi elfu moja ndiyo za kwao, pale kuna neno nusu ndio limekosekana. Kwa hivyo asimsakame Mhe. Waziri kwa madawati. Hiyo taarifa kama niliitoa miye, miye ndiye ninayesahihisha.

**Mhe. Spika:** Niwashukuru wote kwa taarifa hizo, hiyo ndiyo ina maana ya ile kamati inayohusika sasa ifatilie huo ukweli. iwe ni sehemu ya kazi ya kwaida ili kuona uhalisia wa *value for money*, kutokana na hizi taarifa na masahihisho ya taarifa iliyotolewa.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo basi sasa niwahoji wale wanaokubali na kupokea taarifa ya utekelezaji wa Wizara ya Fedha pamoja na Ripoti ya Kuchunguza hesabu za serikali ya mwaka 2014/2015 wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja imetolea iamuliwe)*
*(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Spika:** Taarifa ya utekelezaji imepokelewa na ripoti ya Kamati imepokelewa kwa ajili ya kufanyiwa kazi na serikali.

Wahishimiwa Wajumbe nichukue nafasi kuwashukuru tena, zimebakia dakika kumi na tano kazi iliyopo mbele yetu tulizungumza na Mwenyekiti mapema kasema inahitaji si chini ya saa moja na nusu katika kuwasilisha. Ni dhahiri kwamba dakika kumi na tano hazitoshi kuifanya kazi hiyo. Kwa hiyo nichukue nafasi hii kusitisha shughuli zetu kutoka hapa, hivi sasa niahirishe kikao hiki basi hadi saa 11:00 jioni leo, ambapo Kamati Teule itakuja kuwasilisha ripoti yake.

*(Baraza limeahirishwa saa 5:43 mpaka jioni saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)*

## RIPOTI YA KAMATI TEULE YA KUCHUNGUZA UPOTEVU WA NYARAKA

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa (Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Kuchunguza Upotevu wa Nyaraka):** Kwanza sina budi kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi kwa kuweza kutuwezesha siku hii ya leo kwa mara nyengine tena kufika hapa kuendelea na utaratibu wetu ambao tulikuwa tumejipangia.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, nikushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuja kuwasilisha Ripoti Kamati Teule ya Kuchunguza Upotevu wa Nyaraka uliotokea katika Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa Zanzibar.

Pia niwashukuru wajumbe wenzangu ambao nilikuwa nao katika kamati tulishirikiana vizuri na hatimaye kwa imani yao leo kuniwezesha mimi kuweza kusimama hapa na kuweza kuwasilisha ripoti hii, na mwisho kabisa ninawashukuru sana wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi kwa matayarisho yaliyotokea hatimaye nikaweza kuwasilisha ripoti hii.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwa utangulizi kwa kusema kwamba Kamati Teule ya Kuchunguza Upotevu wa Nyaraka imeundwa na Baraza la Wawakilishi katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Baraza la Nane ambao ulikuwa mahususi kwa ajili ya kujadili Ripoti za Serikali na Hoja za Kamati za Kudumu za Baraza

la Wawakilishi. Kamati hiyo imeundwa kwa mamlaka iliyonayo Baraza ambayo ni kwa mujibu wa Kanuni ya 120 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2012.

**Chimbuko la Kamati Teule**

Kamati Teule ya Kuchunguza Upotevu wa Nyaraka imeasisiwa na hoja ya Mhe. Ussi Jecha Simai ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi aliyoitowa mnamo tarehe 28/01/2014 wakati akiwasilisha muhtasari wa Ripoti ya Kamati hiyo kuhusu Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma.

Wakati wa Kuwasilisha ripoti hiyo Mwenyekiti aliliomba Baraza kufanya maamuzi ya kuunda Kamati Teule ambayo itafanya kazi ya kwenda kuchunguza masuala ya upotevu wa nyaraka za Serikali uliotokea katika Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa iliyopo Kilimani. Mhe. Ussi alieleza kama ifuatavyo:

> "Mhe. Spika, tunataka tutumie kanuni ya 120 ya Kanuni zetu, kwamba na sisi tuna Mamlaka na uwezo wa kuunda Kamati Teule kwa ajili ya uchunguzi. Serikali watachunguza Kwa upande wao na sisi Kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao tunawabeba wananchi, mimi nahisi tuna wajibu wa kwenda kuangalia katika eneo hili. Kwa hivyo, Mhe Spika, nakuomba ukubaliane na wazo letu la kuundwa kwa Kamati Teule ili tuisaidie kazi Serikali…"

Hoja hii imeungwa mkono na kuchangiwa na wajumbe mbali mbali kama ifuatavyo:

- **Mhe. Hamza Hassan Juma**

Anaomba Kamati Teule iundwe ili kuchunguza kadhia hii na maneno yake yalikuwa kama ifuatavyo:-

> "Mhe. Spika, hii kadhia imefanywa na watendaji wa Wizara, tukisema tuiachie Serikali ikachunguze tuna tabia ya kufumbiana macho. Mimi nadhani chombo chako hiki kwa kutumia Kanuni hii ya 120 nimeisoma hapa basi Baraza lako tukufu Mhe. Spika, liunde Kamati Teule tukachunguze kadhia ile na tukachunguze ni sababu gani."

- **Mhe. Ismail Jussa Ladhu**

Naye aliendelea kuunga mkono hoja ya kuundwa Kamati Teule na katika mchango wake alisema:-

> "Mheshimiwa Spika, katika suala hili mimi hata nikisimama kuunga mkono hoja ya kuundwa Kamati Teule mara nyingi huwa nishatafakari sana na ningetegemea katika hali ya kawaida nisingelisema tuiachie Kamati ya Kisekta. Lakini Kamati yenyewe ya sekta inasemaje, kwa hili iundwe Kamati Teule ikachunguze. Sasa mimi naliunga mkono kwanza pendekezo hili."

- **Mhe. Salmin Awadh Salmin**

Wakati akichangia hoja hiyo kama Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, anakubaliana na hoja iliyotolewa na Mwenyekiti huyo kuundwa Kamati Teule ikachunguze na alisema yafuatayo:-

> "Nakubaliana na hoja ya Mwenyekiti wa Kamati na wajumbe wote kuunda Kamati Teule itakayoweza kuchunguza jambo lile. Kwa sababu pale nyaraka haziibiwi bali zinachukuliwa."

**Muundo wa Kamati Teule ya Nyaraka**

Katika Mkutano huo wa Kumi na Tano kikao cha tano cha Baraza la Wawakilishi ambapo baada ya Baraza kuridhia, Mhe. Spika, aliteua wajumbe watano kuunda Kamati hiyo kama ifuatavyo:

i. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
ii. Mhe. Ussi Jecha Simai
iii. Mhe. Ashura Sharif Ali
iv. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
v. Mhe. Mohammed Haji Khalid

Kwa mujibu wa kanuni ya 122(6) Katibu wa Baraza aliteua makatibu wa Kamati wawili kutoka miongoni mwa watumishi wa Baraza ambao ni waratibu wa shughuli za Kamati, makatibu hao ni:

i. Ndg. Khamis Hamad Haji; na
ii. Ndg. Latifa Saleh Suleiman

Katika kutekeleza matakwa ya Kanuni ya 120(4), inayotaka wajumbe wa Kamati kuchagua Mwenyekiti katika mkutano wao wa kwanza, hivyo basi katika mukutano wa kwanza wa mwezi Febuari, 2014, wajumbe wote kwa kauli moja walimchagua Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa kuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo.

**Hadidu Rejea za Kamati Teule**

Kamati Teule ya Kuchunguza Upotevu wa Nyaraka imepewa hadidu rejea mbili za kufanyia kazi ambazo ni:-

i. Kuchunguza suala zima la upotevu wa Nyaraka katika Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa iliyopo Kilimani, Zanzibar; na

ii. Kuchunguza na hatimae kupendekeza njia mbali mbali muafaka ambazo Nyaraka nyengine zitakuwa salama.

**Utaratibu wa kazi za Kamati Teule**

**Muda wa kazi**

Uzoefu umeonesha kuwa Kamati Teule mbali mbali zilizoundwa na Baraza hili la Nane kwa kawaida, zimekuwa zikiwasilisha ripoti zake katika Mkutano unaofuata baada ya ule Mkutano ambao Kamati hiyo imeundwa.

Itakumbukwa kwamba wakati Kamati hii inaundwa ilipangiwa muda wa siku saba (7) tu kukamilisha kazi yake kuwasilisha ripoti Barazani.

Hata hivyo, kazi hiyo haikuweza kuanza kwa wakati uliopangwa kwa vile muda huo wajumbe wote wa Baraza walikuwa katika maandalizi ya mwisho ya kuhudhuria katika Bunge Maalum la Katiba lililoanza mnamo mwezi Febuari, 2014 na kuahirishwa mwishoni mwa mwezi April, 2014.

Katika mwezi wa Ogasti, mpaka Oktoba, 2014 Bunge Maalumu la Katiba liliendelea na kazi zake hivyo bado haikuwezekana Kamati kufanya kazi yake katika nyakati hizo.

Kamati ilianza kazi rasmi siku ya tarehe 29/12/2014 kwa kuanzia muda wa siku saba zilizopangwa awali.

Hata hivyo, katika kipindi hicho kifupi, Kamati ilifanya shughuli ya uchunguzi na kukusanya ushahidi wa maelezo na vielelezo kwa hatua mbali mbali ambapo shughuli hizo zilikuwa kubwa kuliko siku zilivyotolewa.

Mhe. Spika kwa busara kubwa, alikubali ombi la Kamati la kuongezewa muda wa kumaliza kazi zake katika hatua zilizobakia. Kamati kwa ujumla imefanya kazi hii ya uchunguzi kwa muda wa wiki sita.

**Njia zilizotumika kukamilisha kazi**

Njia mbali mbali zilitumiwa na Kamati katika kukamilisha kazi ya uchunguzi na hatimae kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa ili kudhibiti wizi na upotevu huo usitokee tena, njia hizo ni kama zifuatavyo:-

i. Kuchambua Sheria mbali mbali zinazohusiana na kadhia hii, kwa mfano Sheria ya Utumishi wa Umma namb. 2 ya mwaka 2011, Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa, Nam. 3 ya mwaka 2008, Sheria ya Kinga, Fursa za Kidiplomasia na Kikonsula Namba 5 ya 1986 ya Jamhuri ya Muungano Tanzania;

ii. Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2014;

iii. Kufanya mahojiano na watu mbali mbali ambao Kamati iliamini kwamba wanaweza kusaidia katika uchunguzi huo;

iv. Kufanya ukaguzi wa nyaraka mbali mbali katika Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa;

v. Kuchambua vielelezo vilivyowasilishwa mbele ya Kamati; na

vi. Kufanya ziara katika maeneo mahususi yanayohusina na uchunguzi.

Pia Kamati ilikusudia kufanya ziara ili kukagua sehemu mbali zinazowekwa kumbukumbu za nchi yetu, hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda Kamati ilifanya ziara ya kwenda kukagua nyaraka za sauti za matukio ya Mapinduzi ya mwaka 1964, zilizopo katika Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) mjini Rahaleo.

## SEHEMU YA PILI

## MAUDHUI

### HADIDU REJEA ZA KAMATI NA NAMNA KAMATI ILIVYOZIFANYIA KAZI

Katika kueleza jinsi Kamati ilivyozifanyia kazi hadidu rejea ilizopewa na Baraza hili tukufu, Kamati ingependa kueleza historia fupi inayohusu Nyaraka hapa Zanzibar.

Jumba la uhifadhi wa nyaraka Kilimani lilifunguliwa rasmi katika mwaka wa 1963 na Nyaraka za Serikali zikaanza kuhamishiwa katika jengo hilo kuanzia mwaka huo. Nyaraka za mwanzo kuhamishiwa katika jengo hilo zilikuwa ni zile za *Consular General* na *British Resident* ambazo zilikuwa katika jengo la *British Resident* au Ikulu kwa sasa. Nyaraka hizo zimeitwa kwa majina haya kutokana na aina mbili za mifumo ya utawala wa Kingereza zilizokuwepo hapa kabla, ambayo ni ile ya *Consular General* na ya pili ni ile ya *British Resident.*

Ofisi hizi ndizo za mwanzo kuzalisha nyaraka na ndizo zenye nyaraka za zamani zaidi katika jumba la nyaraka.

Nyaraka hizi zina thamani kubwa sana katika dunia kwa kuwa zina ushahidi wa asili kuhusu matokeo mbali mbali ya nchi hii, pia maandishi yake mengi ni ya mkono yakiwa katika lugha ya Kiarabu na Kiengereza, hii inatokana na kuwepo kwa tawala mbili zilizotawala Zanzibar, moja ya Kiengereza na nyengine ya Kisultani kwa wakati huo.

Hivyo basi, utawala wa Sultan ulipokuwa ukifanya mawasiliano rasmi na Serikali ya Oman na kwengineko, kumbukumbu zake zilihifadhiwa katika kumbukumbu za *Consular General* kwa vile ndiye aliyekuwa Mtendaji Mkuu wa Serikali. Nyaraka nyingi katika kundi hili ni zile za mawasiliano kati ya Zanzibar na Uingereza pamoja na Oman.

Baada ya Uingereza kufanya mabadiliko ya Tawala nafasi ya *Consul General* ilibadilishwa na kuitwa *British Resident* na kufunguliwa Ofisi mpya ya *Chief Secretary* na kuundwa kwa Idara za Serikali kama vile za Kilimo, Elimu, Tiba, Manunuzi na Mauzaji, pamoja na Wakfu.

Hivyo basi, uzalishaji wa Nyaraka ukaanza kukuwa na kuwa na makundi mengine mapya ya nyaraka ambayo ni ya *British Resident Records*, *Secretariat Records* kutoka kwa afisi ya *Chief Secretary*, ambazo ni nyaraka za Idara ya Kilimo, Nyaraka za Idara ya Elimu, Nyaraka za Idara ya Afya, Nyaraka za Idara ya Mauzaji na Manunuzi pamoja na Mirathi.

Makundi mengine ya Nyaraka zilizopo katika jumba la Nyaraka ni *Arabic Manuscripts*, hivi ni vitabu ambavyo vilichukuliwa kutoka katika Kasri la Mfalme ambavyo ni vya zamani na vyenye thamani kubwa sana, takriban Wafalme wengi waliopita wa Zanzibar walikuwa wakivitumia vitabu hivi kwa ajili ya kufanyia dawa na mambo mengine yanayohusiana na familia zao. Mfano mzuri ni ule wa Sultan Sayyid Said alipotaka kuwasiliana na Serikali ya Oman kwa kumfunga njiwa barua na kumrusha kupeleka ujumbe Oman, mnamo miaka ya 1840.

Mbali na nyaraka hizi zipo nyaraka za picha, ramani, michoro na machapisho ya kale pamoja na kumbukumbu za utawala wa Kijerumani ambazo pia yalihamishiwa hapo katika kipindi kifupi baada ya kufunguliwa jumba la uhifadhi wa nyaraka Kilimani, na hadi kufikia Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 takriban nyaraka zote muhimu zilikuwa zimeshahamishiwa katika jumba hilo.

Kwa bahati nzuri baada ya Mapinduzi Nyaraka hizo hazikuwa zikitumika sana zaidi ya kuhifadhiwa katika chumba maalum cha Uhifadhi nyaraka *(repository room).* Hali hii iliendelea hadi mwaka 1981 wakati Wajerumani walipokuja kuzichukuwa nyaraka zao yaani *German Records* kwa ajili ya kwenda kuzifanyia ukarabati, maombi yao yalikubaliwa na kupewa nyaraka zote za Kijerumani kwa ajili ya kwenda kuzifanyia ukarabati baadae zilirejeshwa na kuhifadhiwa kwenye chumba cha uhifadhi *(repository room)*, jambo hilo kidogo lilikuwa ni kosa kwa vile hakuna uhakika kama nyaraka hizo zilizorejeshwa zilikuwa za asili au ni kopi.

Katika mwaka 1983 walikuja wataalamu kutoka katika nchi za Jumuiya ya Madola *(Common Wealth)* na kuiomba Serikali kuruhusiwa kusaidia kuzipitia na kuzipanga upya nyaraka hizo ili baadae nyaraka hizo ziweze kutumiwa na wasomi watakapohitaji, ombi hili lilikubaliwa na Serikali, na hapa ndipo yalipofanyika mabadiliko makubwa katika jumba la nyaraka.

Nyaraka zote zilizokuwepo katika jumba la nyaraka zilipangwa upya na kufanyiwa faharisi *(indexing system)*, baada ya kumalizika kazi hii ndipo hapo kazi ya kuitangaza Zanzibar na hazina yake ya nyaraka ilipoanza kwa njia ya radio pamoja na magazeti ya ndani na nje.

Watu mbali mbali walikuja katika jengo la nyaraka kwa madhumuni tofauti, wengine kwa ajili ya kusoma, utafiti, kuangalia na wengine ni kwa ajili ya wizi wa hazina hiyo.

Mbali na nyaraka hizo za kale Jumba la nyaraka pia linahifadhi sehemu kubwa ya nyaraka ambazo zimezalishwa na Wizara mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, zilizoundwa baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964. Hata hivyo, uhifadhi wa kumbukumbu baada ya 1964 sio wa kuridhisha.

**MATOKEO YALIYOPATIWA UFUMBUZI KUTOKANA NA KUWEPO NYUMBA YA KUHIFADHI NYARAKA ZA TAIFA**

Umuhimu wa nyaraka na kumbukumbu za kitaifa siyo kwa ajili ya kuhifadhi na kusoma tu bali pia unalinda historia na kumbukumbu muhimu za matukio ya nchi ambayo ushahidi wa matokeo yake unahuishwa kwa uwepo wa nyaraka hizo.

Ripoti hii inakumbusha baadhi ya matukio muhimu yaliyowahi kutokea katika nchi hii na kukosa ufumbuzi wa haraka isipokuwa ufumbuzi wake ulipatikana kutokana na Nyumba ya Nyaraka na kumbukumbu za kitaifa, matukio ambayo ni kama ifuatavyo:-

i. Mkataba wa Ujenzi wa gati ya Zanzibar kuhusu malipo ya fidia kutoka kampuni ya *Cogefer*. Katika mkataba huo kulikuwa na kipengele cha fidia iwapo gati hiyo ingepata athari kwa kipindi fulani, ilipotokezea athari hiyo mkataba huo ulikuwapo katika nyumba ya Nyaraka na fidia hiyo ikalipwa;

ii. Umiliki wa mnara wa mawasiliano wa ‘wireless’ Kikwajuni, mnara huo, Kampuni ya mawasiliano ya TTCL ilikodishwa na SMZ na baadaye kudai kuwa mnara huo ni wao, wakitaka kuuvunja na kujenga mwengine, nyumba ya nyaraka ilithibitisha kwa kutoa nyaraka za umiliki wa mnara huo kwa SMZ;

iii. Umiliki wa jengo la Posta, Kijangwani ambalo liliwahi kudaiwa na Shirika la Posta Tanzania kwa madai kuwa lilijengwa kwa fedha za EAC, hata hivyo, Kumbukumbu kutoka Nyumba ya Nyaraka zilikuja kuonyesha kuwa SMZ ilijenga jengo hilo kwa fedha zake, hivyo ni mali ya SMZ;

iv. Nyumba ya Wakf iliyonunuliwa na Serikali ya Zanzibar nchini Saudia Arabia, mjini Makka kwa ajili ya kuweka wakf ya watu masikini wa Makka, wakati huo nchi ya Saudi Arabia ikiwa masikini na Zanzibar ikisaidia, kumbukumbu zinazohusu nyumba hiyo zilithibitishwa kutoka nyumba ya Nyaraka;

v. Umiliki wa Kisiwa cha Mombasa na hivi karibuni kisiwa cha Lamu (Fungu Mbaraka) kumbukumbu zake zipo nyumba ya Nyaraka na zinathibitisha umiliki wake kwa Zanzibar;

vi. Ushahidi wa Umiliki wa majengo, ardhi na mashamba kwa Serikali na watu binafsi, umekuwa ukithibitishwa kutoka na nyaraka ambazo zipo katika nyumba ya Nyaraka;

vii. Kumbukumbu za kesi za watu mbali mbali za mirathi na ugawaji wake ulivyofanyika zinahifadhiwa katika nyumba ya Nyaraka; na

viii. Kuwapo kwa hifadhi ya vitabu mbali mbali vya asili ikiwemo Msahafu wa kale uliopatikana Makunduchi na baadaye kupelekwa Tumbatu na hatimaye kupelekwa pale na Mhe. Dr. Salmin Amour Juma.

Matukio haya na mengine mengi yana ushahidi ambao ni Nyumba ya Nyaraka ni Kumbukumbu pekee inayoweza kuyaweka kwa usahihi kutokana na kumbukumbu zake kuhifadhiwa hapo kwa dahari. Kamati imeamuwa kuweka mifano hii kwa nia ya kutoa taarifa kwa chombo hiki cha wananchi kujuwa ni kitu gani Taifa hili kinapoteza pale inapotokea nyaraka za Taifa zimepotea au kuibiwa.

Kumbukumbu zilizooredheshwa hapo juu zimehifadhiwa katika nchi hii miaka mingi nyuma na kizazi cha sasa kimeweza kuzitumia kutatuwa matatizo ambayo hayafahamiki na kuyapatia ufumbuzi.

Kamati inajiuliza iwapo yumba ya nyaraka itahujumiwa na watu wa ndani na nje, je, kizazi kijacho kitawezaje kutatua changamoto za nchi hii kama kizazi cha leo kilivyoweza kwa kutumia kumbukumbu zilizohifadhiwa na waliopita.

Kwa kuongezea, kamati ilipata kufahamu pia kuwa Nyumba ya Nyaraka imekuwa sehemu muhimu katika ujenzi wa Taifa hili, kwani wapo viongozi wa Kitaifa ambao wameitumia sana nyumba hiyo wakati wakifanya utafiti katika masomo yao ya elimu ya juu kama vile Makamu wa Kwanza Rais Maalim Seif Shariff Hamad na Rais wa awamu ya Tano wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dkt. Salmin Amour Juma ambapo wakati akifanya utafiti katika masomo yake ya Shahada ya Uzamivu (*PhD*) alitumia sana Nyumba ya Nyaraka, Kilimani.

Vile vile, katika kipindi cha utawala wake aliiweka taasisi hiyo chini ya Afisi ya Rais na kuipa uangalizi wa karibu, kamati imefahamishwa kuwa Dkt. Salmin Amour alikuwa mstari wa mbele katika kuihuisha Nyumba ya Nyaraka kwani mara kadhaa mpaka akiwa madarakani amekuwa akipeleka mwenyewe nyaraka kwa ajili ya kuhifadhiwa.

Kamati inaeleza mifano hii muhimu kwa madhumuni ya kufahamisha kuwa umuhimu wa Nyumba ya Nyaraka katika ujenzi wa taifa letu sio wa kupuuzwa hata kidogo.

## HADIDU REJEA YA KWANZA

Baada ya ufafanuzi huo mfupi kuhusu historia fupi ya nyaraka na uanzishwaji wa Nyumba ya Nyaraka Zanzibar na umuhimu wake kwa Taifa, yafuatayo ni maelezo ya uchambuzi wa hadidu rejea za Kamati Teule kama ifuatavyo:-

### Kuchunguza Suala Zima la Upotevu wa Nyaraka katika Afisi ya Nyaraka iliyopo Kilimani, Zanzibar

Katika kuifanyia kazi hadidu rejea Nam. 1, kamati imetazama mambo mbali mbali yaliyojumuisha kadhia iliyotokea, uchambuzi wa hadidu rejea hiyo imeifanya kamati kutazama mambo yafuatayo:-

a. Upotevu wa nyaraka ulivyo katika Taasisi ya Nyaraka;
b. Mazingira ya wizi na upotevu wa nyaraka;
c. Maslahi ya nchi yamezingatiwaje katika kushughulikia kadhia ya wizi wa nyaraka;
d. Mambo yaliyopelekea au yaliyorahisisha suala la wizi au upotevu wa nyaraka katika Taasisi ya Nyaraka.

### Upotevu wa Nyaraka ulivyo katika Taasisi ya Nyaraka

Katika zoezi la ukaguzi wa nyaraka wa kubaini suala zima la upotevu wa nyaraka lilivyo katika Taasisi ya Nyaraka, kamati ilifanya kazi ya kuchunguza nyaraka kwa mtindo wa maeneo maalumu (*sampling*) kwa sababu ya ufinyu wa muda na wingi wa nyaraka zilizopo katika Nyumba ya Nyaraka, Kilimani.

Katika maelezo ya awali yaliyopatikana na kamati ni kuwa kuna ukaguzi uliofanywa na wafanyakazi mara baada ya tukio la wizi la upotevu wa nyaraka na mabadiliko ya wafanyakazi katika chumba cha hifadhi. Ukaguzi ambao uligunduwa baadhi ya maeneo ambayo nyaraka hizo zimepotea. Hatua hiyo ya uchunguzi haikuendelea kwa kile kamati ilichoelezwa kuwa Mkurugenzi alisitisha zoezi hilo lisiendelee. Rejea kiambatanisho Nam. 1 kuhusu nakala ya taarifa ya uchunguzi iliyofanywa na wafanyakazi waliokabidhiwa chumba cha hifadhi ya nyaraka.

Kamati ilipomuhoji Mkurugenzi wa Nyaraka kwa nini alisitisha zoezi la ukaguzi, alisema kuwa alisitisha kwa sababu alihofia nyaraka zilizokuwemo ni za muda mrefu na hakumuachia kila mtu kufungua na kuzishika kungeliweza kuleta athari kwa nyaraka hizo. Kamati imeona kwamba haikuwa busara ukaguzi huo kusitishwa katika hatua hiyo ambayo kama ungeliendelea mapungufu mengi yangelioneka, ikizingatiwa kuwa waliokuwa wakifanya ukaguzi huo ni wafanyakazi waliokabidhiwa dhamana na wanajua umuhimu wake.

Kamati pia ilipitia uchunguzi wa polisi ambao ulifanyika mwezi Febuari, 2014 ambapo uligundua maeneo kadhaa kuwa na mapungufu na baadhi ya maboksi ya kuhifadhia nyaraka hizo yakiwa matupu. Rejea ukurasa wa 2 wa kiambatanisho Nam. 2 kuhusu barua ya polisi iliyoainisha maeneo ya uchunguzi na matokeo yake.

Kamati ilitumia taarifa hizo kama mwelekeo tu wa uchunguzi wake na mnamo tarehe 15/02/2015, iliamua kuingia katika chumba cha uhifadhi wa nyaraka kwa muda wa wiki moja. Katika uchunguzi huo kamati imegundua nyaraka ziafuatazo:-

**NYARAKA ZA MAANDISHI YA KIARABU *(ZA-ARABIC MANUSCRIPTS)***

i. Nyaraka za maandishi ya Kiarabu na vitabu vyengine *(ZA1, Arabic Manuscripts-Holy Qur-an and Suras)* ambazo zipo kuanzia kundi la *ZA1* mpaka *ZA* 13, ambapo kila boksi moja kati ya maboksi hayo 13 uchache wake ni nyaraka 10 na wingi wake ni nyaraka 130. Katika uchunguzi huo kamati imegundua kuwa kundi la nyaraka za *ZA1*, ambazo idadi yake ni nyaraka 105, nyaraka ambazo zimepotea ni mbili (2), mbazo zimeorodheshwa katika kiambatanisho Nam. 3, kuhusu orodha ya nyaraka za *ZA1* zilizopotea;

ii. Nyaraka za maandishi ya Kiarabu za vitabu vya tiba *(ZA2 Arabic Manuscripts- Diseases, treatments, local medicine and witchcraft)* idadi ya nyaraka hizo ni kuanzia 1-30 na kamati imebaini nyaraka tisa (9) hazimo kama zilivyoorodheshwa katika kiambatanisho Nam. 4 kuhusu orodha ya nyaraka za *ZA2* zilizopotea;

iii. Nyaraka za maandishi ya Kiarabu za vitabu vya historia *(ZA3 Arabic Manuscripts-History General)* idadi yake ni kuanzia 1-55. Kamati imebaini nyaraka kumi (10) hazipo kama ilivyooneshwa katika kiambatanisho Nam. 5 kuhusu orodha ya nyaraka za *ZA3* zilizopotea;

iv. Nyaraka za maandishi ya Kiarabu za vitabu vya lugha *(ZA4 Arabic Manuscripts-Series and languages)* ambazo idadi yake ni 1-27. Kamati imebaini nyaraka tano (5) hazipo na nyengine zimehamishiwa pahala pengine ambapo pia hazipo, rejea kiambatanisho Nam. 6, kuhusu orodha ya nyaraka za *ZA4* zilizopotea;

v. Nyaraka za maandishi ya kiarabu kuhusu Sheria za Kiislamu *(ZA5 Arabic Manuscripts-series Islamic Laws)*, idadi ya nyaraka ni kuanzia 1-139. Kamati imebaini nyaraka kumi na mbili (12) hazipo, rejea kiambatanisho Nam. 7, kuhusu orodha ya nyaraka za *ZA5* zilizopotea**;**

vi. Nyaraka za maandishi ya Kiarabu za vitabu vya hadithi na simulizi *(ZA6 Arabic Manuscripts-Novels and Stories)* idadi yake ni kuanzia 1-12. Kamati imebaini nyaraka mbili (2) hazipo, rejea kiambatanisho namba KTN 8, orodha ya nyaraka za *ZA6* zilizopotea;

vii. Nyaraka za maandishi ya Kiarabu za vitabu vya kumbukumbu *(ZA7 Arabic Manuscripts-Diaries&Records books)* ambazo idadi yake ni kuanzia 1-26. Kamati imebaini nyaraka moja (1) haipo, rejea kiambatanisho namba KTN 9, kuhusu orodha ya nyaraka za *ZA7* zilizopotea;

viii. Nyaraka za maandishi ya Kiarabu zinazohusu kidini kwa ujumla *(ZA8 Arabic Manuscripts-Religion general)* ambazo idadi yake ni kuanzia 1-60. Kamati imebaini kuwa nyaraka mbili (2) hazipo kama zinavyooneshwa katika rejea kiambatanisho namba KTN 10 kuhusu orodha ya nyaraka za *ZA8* zilizopotea;

ix. Nyaraka za maandishi ya Kiarabu zinazohusu mkusanyiko wa majarida ya kihistoria *(ZA11 Arabic Manuscripts-Collection of Historical Magazine)*, ambazo idadi yake ni kuanzia 1-15. Kamati imebaini nyaraka moja (1) imepotea, rejea kiambatanisho namba KTN 11 kuhusu orodha ya nyaraka za *ZA11* zilizopotea; na

x. Nyaraka za maandishi ya Kiarabu zinazohusu mambo ya kilimo kwa ujumla *(ZA12 Arabic Manuscripts-Agricultural general)* ambazo idadi yake ni kuanzia 1-8. Kamati imebaini nyaraka moja (1) imepotea, rejea kiambatanisho namba 12, kuhusu orodha ya nyaraka za ZA12 zilizopotea.

**NYARAKA ZA MAWASILIANO YA BARUA *(AA5/ ARABIC CORRESPONDENCE)***

Nyaraka hizi zinahusu maandishi ya lugha ya Kiarabu yanayohusu mawasiliano ya barua zilizoingia na kutoka *(AA5 Arabic Correspondent-inward and outward letters).*

Nyaraka za sehemu hii ndizo zilizoathiriwa na tukio la wiz. Katika ukaguzi huu maboksi sita yaliathirika kwa nyaraka nyingi zikiwa zimeibiwa na boksi moja likiwa tupu. Nyaraka hizi za barua ni nyingi na katika kila boksi zimewekwa kwa *'volumes'* ambazo ndani yake zimo barua nyingi.

Tatizo kubwa kamati imegundua kuwa barua hizo hazina nambari maalumu ya kuzitambua kwa hiyo iwapo zinaibiwa au kupotea sio rahisi kujua idadi gani ya barua hizo zilizopotea au kuibiwa. Miongoni mwa nyaraka ambazo kamati imezikagua na kubaini mapungufu hayo kwa pamoja zinajumuishwa katika kiambatanisho KTN 13:-

i. Nyaraka za barua za mawasiliano yaliyoingia na kutoka (*AA5 Arabic Correspondents-inward and out wards letter)* ambazo idadi yake ni kuanzia 1-26. Kamati imebaini kuwa nyaraka kumi na tano (15) hazipo**;**

ii. Nyaraka za barua za kumbukumbu za Mahakama *(AA7 Arabic Correspondents-Courts records)* ambazo idadi yake ni kuanzia 1-6. Kamati imebaini nyaraka moja (1) haipo; na

iii. Nyaraka za barua *consular (AA8 Arabic Correspondents-Consular and Agents records)* ambazo idadi yake ni kuanzia 1-7. Kamati imebaini nyaraka moja (1) haipo.

**NYARAKA ZA AFISI YA ARDHI *(AE LAND OFFICE-HOUSING SERIES)***

Nyaraka hizi zinahusu masuala ya ardhi, mashamba na nyumba. Kamati imezipitia na kugundua yafuatayo:-

i. Nyaraka za ardhi *(AE1 Land Office)* ambazo idadi yake ni kuanzia 1-1059. Kamati kutokana na ufinyu wa muda na wingi wa nyaraka hizi, imeweza kukagua maboksi 54 tu na kubaini nyaraka tano (5) hazipo. Rejea kiambatanisho namba KTN 14, kuhusu nyaraka za AE1 zilizopotea. Kamati inaamini kuwa uchunguzi zaidi ukifanyika kuna uwezekano wa kubaini nyaraka nyengine nyingi zaidi zilizopotea.

**NYARAKA ZA BARUA NA MAWASILIANO ZA SULTANI NA MAMBO MBALI MBALI *(ARC 1-5)***

Nyaraka hizi zinahusu mawasiliano ya barua za Sultani na maeneo mengine, taarifa za watembezi na Wamishionari *(Explorers and Missionaries)*, makubaliano na mikataba, mawasiliano ya *Lord Mathew* na maelezo mbali mbali ya taarifa ndogo ndogo za maandishi (*memos*). Katika ripoti hii nyaraka hizo zimewekwa kwenye kiambatanisho cha pamoja namba KTN 15, zinazohusu orodha ya nyaraka za *ARC* zilizopotea. Kamati imekagua makundi matano ya nyaraka hizo kama ifuatavyo:-

i. Nyaraka za barua na mawasiliano ya Sultani *(ARC1 Sultanate Letters and Correspondents)* ambazo idadi yake ni kuanzia 1-219. Kamati imebaini kuwa nyaraka kumi na sita (16) hazimo**;**

ii. Nyaraka za watembezi na Wamishionari *(ARC2 Explorers and Missionaries),* ambazo idadi zake ni kuanzia 1-54. Kamati imebaini nyaraka moja (1) haipo;

iii. Nyaraka za mikataba na makubaliano *(ARC3 Treaties and Agreements)* ambazo idadi yake ni kuanzia 1-43. Kamati imebaini kuwa nyaraka tano (5) hazipo;

iv. Nyaraka za Mawasiliano ya *Lord Mathew (ARC/4),* ambazo idadi yake ni kuanzia 1-36. Kamati imebaini nyaraka moja (1) haipo; na

v. Nyaraka za mambo mbali mbali *(ARC/5 Miscellaneous)* ambazo idadi yake ni kuanzia 1-130. Kamati imekuta nyaraka zote hizi zipo.

**NYARAKA ZA MAANDISHI KUTOKA KASRI YA SULTANI *(AQ 1 ARABIC SCRIPT FROM SULTAN PALACE)***

Nyaraka hizo ni kama ifuatavyo:-

i. Nyaraka za *AQ 1* ambazo idadi yake ni kuanzia 1-4, kamati imebaini nyaraka mbili (2) hazipo, rejea kiambatanisho namba KTN 16.

**NYARAKA ZA MIRATHI *(HC1 PROBATE AND ADMINISTRATION)***

Nyaraka hizi idadi yake ni 4,948 ambapo kamati ilipata muda wa kukagua nyaraka 685 na kugundua nyaraka thelathini (30) hazipo rejea kiambatanisho namba KTN 17.

**KUMBUKUMBU ZA KIJERUMANI *(AL 1 & AL 2 GERMAN RECORDS)***

Nyaraka hizi za *(AL 1)* zipo kuanzia 1-15, ambapo katika ukaguzi kamati imebaini nyaraka 1 haipo. Katika nyaraka za (*AL 2)* ambazo idadi yake ni kuanzia 1-111, kamati imebaini nyaraka moja (1) haipo. Rejea kiambatanisho namba KTN 18.

**NYARAKA ZA USAJILI WA HATI *(AM GENERAL DEEDS REGISTERS)***

Nyaraka hizi zinahusu usajili wa hati za mauziano, wakfu na uwekaji rahani. Kamati katika uchunguzi wake imekagua na kubaini mapungu katika nyaraka zifuatazo:-

i. Nyaraka za usajili wa hati kwa ujumla *(AM1 General Deeds Register)* ambazo idadi yake ni kuanzia 1-18, kamati imebaini nyaraka mbili (2) hazipo;

ii. Nyaraka za usajili wa hati katika Afisi ya *Consular (AM 2 General Deeds Register at Consular General Office)*, ambazo zipo kuanzia 1-24, kamati imebaini kuwa nyaraka mbili (2) hazipo;

iii. Nyaraka za Usajili wa Hati za Mauziano na Wakf *(AM 7 Deeds of sales, Wakf Servant Employment)*, idadi yake ni 26 ambapo nyaraka moja (1) haipo;

iv. Nyaraka za usajili wa hati za mauziano na rahani *(AM 8 Deeds of sales and Mortgage)* idadi yake ni 12 ambapo nyaraka mbili (2) hazipo;

v. Nyaraka za usajili wa hati za mauziano *(AM 10 Deeds of Sales Optional Mortgage)* idadi yake ni 1-29 ambapo nyaraka moja (1) haipo;

vi. Nyaraka za usajili wa hati kwa lugha ya Kiarabu *(AM 11 Arabic Deeds Register)* idadi yake 1-23 ambapo nyaraka mbili (2) hazipo; na

vii. Nyaraka za usajili wa hati Pemba *(AM 13 General Deeds Vol. from Pemba)* idadi yake ni 103 ambazo nyaraka moja (1) haipo.

Nyaraka zote za kundi la *AM 1-13* zimeorodheshwa katika kiambatanisho namba KTN 19, kilichoambatanishwa pamoja na ripoti hii.

**Mazingira ya Wizi na Upotevu wa Nyaraka**

Kamati ilichunguza kwa mazingatio makubwa eneo hili na kwa kuwa hoja hii inataka umakini kuifanyika kazi kwa sababu tayari pamekuwa na mjadala wa wizi uliotokea katika Taasisi ya Nyaraka. Wala hapakuwa na mjadala kuwa hatua zilichukuliwa kwa wanaodaiwa kuhusika na tukio hilo kama ilivyothibitishwa na serikali katika Baraza hili. Rejea ukurasa wa 10 kiambatanisho namba KTN 20, kuhusu maelezo ya *hansard* ya Mhe. Haji Omar Kheir yaliyowekwa kwenye *matrix*.

Kwa hivyo, kazi ya kamati hapa haikuwa kwenda kujua kama wizi umetokea au hapana, kwa vile hilo limethibitishwa katika hatua ya awali ya uchunguzi kuwa wizi umetokea. Maana yake ni kuwa wezi walioiba pia walikuwapo. Kamati hakuwa na haja ya kutafuta mwizi nani na ushahidi upi unamfunga kwa kuwa kazi hiyo inahusu vyombo vyengine nje ya muhimili huu.

Kamati ilichotaka kubaini hapa ni mazingira ya wizi yalikuwaje na uhusika wa wanaodaiwa ukoje. Sababu kubwa ya kutaka kujua mambo hayo mawili ni kuwa, kamati imepewa jukumu la kushauri njia za kuzuia taukio hilo lisitokeze tena, hivyo ni vyema kwanza mazingira haya wizi yajulikane.

Pili, kamati inahitaji kupendekeza hatua za kulikamilisha kadhia hii kwa vyombo husika kuchukua hatua zaidi, hivyo uhusika wa wanaodaiwa unabainishwa na kama kuna pahala panapokwama taarifa hii iweze kusaidia. Kamati imeangalia eneo la upotevu na maeneo mengine na kwa mujibu wa taarifa ilizopata katika mahojiano na wafanyakazi mbali mbali wa Taasisi ya Nyaraka, pamoja na vielelezo kadhaa ilivyopokea, imebainika kuwa wizi huo usingelitokea isipokuwa maeneo mawili yalihusika kikamilifu kufanikisha wizi huo, ambayo ni:-

1. Baadhi ya wafanyakazi wa ndani wa Taasisi ya Nyaraka.
2. Na muhusika kutoka nje ya Afisi ya Taasisi ya Nyaraka.

Katika sehemu ya kwanza kamati ilibaini kuwa chumba maalumu cha kuhifadhia nyaraka kilikuwa katika hali hatarishi ya kuweza kufanyika jambo la hatari dhidi ya vitu vilivyohifadhiwa. Kwa kuwa chumba cha uhifadhi nyaraka *'repository'* kilikuwa ndiyo shabaha ya wahalifu ilikuwa dhahiri kuwa uwezekano wa kufanikisha uhalifu huo usingekuwapo kama wafanyakazi wa ndani ya chumba hicho wasingelitumika au kutumiwa katika tukio hilo la uhalifu.

Wakati Kamati ikimuhoji Mkurugenzi wa Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Kitaifa ndugu Hamad Hassan Omar pamoja na watendaji wake kadhaa walifahamisha Kamati kuwa kwa mara ya kwanza tukio la wizi lilianza kubainika baina ya mwezi Julai, Ogasti, Septemba na Oktoba 2013, baada ya baadhi ya wafanyakazi kuanza kutilia shaka nyenendo zisizoeleweka za baadhi ya wafanyakazi wenzao hususani waliokuwa wakifanyakazi katika chumba cha uhifadhi nyaraka.

Kamati ilipodadisi kuhusu hizo nyenendo zisizoelewaka ilielezwa kuwa baadhi ya wafanyakazi walikuwa wakikiuka kwa makusudi taratibu za utendaji kazi zinazohusu chumba cha uhifadhi ambazo hazikuruhusu mfanyakazi kutumia muda mrefu ndani ya chumba hicho bila ya kazi, jambo ambalo linadaiwa kufanyika na wahusika wa uhalifu huo.
Mbali na ukiukwaji huo, Kamati ilielezwa na wafanyakazi hao wakati wa mahojiano kuwa wafanyakazi wa chumba hicho ambao wanatuhumiwa kuhusika na wizi huo walikuwa wakiingia na mikoba na kutoka na vitu.

Aidha, Kamati ilielezwa na kupata ushahidi kuwa wafanyakazi waliohusika walikuwa wakifanyaka mawasiliano na mtu wa nje ya Afisi ya Nyaraka ambae Kamati katika uchunguzi wake imebaini alikuwa wakiwatumia kufanikisha mpango wa wizi ambapo mtu huyo alikuwa akipatiwa nyaraka hizo baada ya kuibiwa kutoka chumba cha uhifadhi, rejea Kiambatanisho namba KTN 21, kuhusu kilelezo cha mawasiliano ya simu za watuhumiwa.

Mtu huyo kama itakavyofafanuliwa kwenye sehemu ya pili, alitumia nafasi yake uongozi kinyume na sheria na nafasi ya kujulikana kwake na baadhi ya wakubwa wa baadhi ya Taasisi za Serikalini ikiwemo ya Nyaraka, kuwashawishi na hatimaye kufanikisha mpango wa kuiba nyaraka za urithi wa Zanzibar.

Katika sehemu ya pili, Kamati ilibaini mazingira ya wizi pia yalikuwa na mhusika kutoka nje ya Taasisi ya nyaraka. Katika sehemu hii Kamati ilianza kwenda kwa undani, kwanza kwa kupitia taarifa za waheshimiwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakati wakichangia hotuba ya ripoti ya Mwenyekti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi, tarehe 28/1/2014 ambayo ndiyo iliyoibuwa kadhia hii na hatimaye kuundwa kwa Kamati Teule.

Katika michango yao baadhi ya wajumbe ambao walikuwa na baadhi ya taarifa za watu waliohusika na uhusika wa mtu mmoja ambaye anafanyakazi katika ubalozi mdogo wa moja ya nchi rafiki na Zanzibar ambapo wajumbe hao walichelea kumtaja jina kwa hofu ya kuharibu uhusiano na nchi hiyo.

Kamati ilipata maelezo ya kina kabisa kama itakavyoelezwa hapo chini kwa kirefu kuwa mtu huyu alikuwa muhimu katika kufanikisha mipango ya wizi wa nyaraka za Zanzibar ambazo ni urithi wa Taifa hili wa leo, kesho na milele.
Katika maelezo yake ya majumuisho ya bajeti ya Afisi ya Rais, Kazi na Utawala Bora, Mhe. Haroun Ali Suleiman aligusia uhusika wa mtu huyu ambaye mheshimiwa Waziri alisema kuwa kijana huyo alimwita na kumuuliza lakini alikataa.

Mheshimiwa aliliambia Baraza kuwa kijana huyo hakuwa mfanyakazi wa ubalozi wa Oman isipokuwa alikuja kwa kazi za ukarabati wa Beit el Ajab na akipita katika ubalozi huo mdogo kama nyumbani, aidha kama wafanyavyo Watanzania wanapokuwa nje ya nchi katika balozi zao, rejea ukurasa wa 12-13 wa Kiambatanisho namba KTN **20,** kuhusu taarifa za hansard ya Mhe. Haroun Ali Suleiman kwenye *matrix*.

**KUHUSISHWA KWA NDUGU HUMOUD ABDULLA AL RASHIDY**

Katika uchunguzi wake Kamati imepitia maelezo na vielelezo mbali mbali vinavyonesha kuwa Humoud alikuwa ni mshukiwa muhimu katika kadhia hii ya wizi, Kamati ilipomtaka Mkurugenzi wa Nyaraka aeleze hatua gani alichukuwa mara baada ya kubainika tukio la wizi, alisema aliripoti tukio hilo Polisi, rejea Kiambatanisho namba KTN 22, kuhusu barua ya Mkurugenzi kwa Polisi ambao walifungua jalada na kuanza uchunguzi.
Hata hivyo, uchunguzi huo ulichukuwa muda mrefu bila ya kukamilika, ambapo Naibu Katibu Mkuu wa Afisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma alifuatilia na kupata maelezo kutoka kwa Kamishna wa Polisi kuhusu hatua ya uchunguzi wa Polisi ilipofikia, rejea Kiambatanisho namba KTN 23, kuhusu barua ya Kamishna wa Polisi kwa Katibu Mkuu Afisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma ambayo pia imewekwa anuani kwa Katibu wa Rais.

Katika maelezo hayo, Polisi ilibainisha hatua za uchunguzi ilizofanya kupitia jopo maalumu la Uchunguzi lilioundwa na Kamishna wa Polisi Zanzibar, aidha ilibainika kuwa katika kadhia yote hiyo pamoja na kuhusika kwa baadhi ya wafanyakazi wa Taasisi ya Nyaraka ambao hatua za kisheria zimeshachukuliwa dhidi yao, mshukiwa mwengine muhimu katika uhalifu huu alikuwa ni Humoud ambaye Polisi katika uchunguzi wao walibaini kuwa alikuwa ni mfanyakazi wa ubalozi mdogo wa Oman Zanzibar.

Aidha, Polisi waliambia kamati kuwa mtu huyo pia ameshawahi kukaimu nafasi ya balozi mdogo wa nchi hiyo, kwa hivyo, alikuwa na kinga ya kibalozi ya kutoshitakiwa na kuhojiwa na vyombo ya kiusalama vya Tanzania kutokana na kinga hiyo aliyo nayo.

Kwa kuthibitisha hilo, Kamati ilimwita kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, ndugu Mkadam Khamis Mkadam, ambaye pia Msaidizi Kamishna, na alithibitisha mbele ya Kamati maelezo hayo na kuwa walipokea barua kutoka Wizara Mambo ya Nje na Ushirikano wa Kimatatifa kupitia Afisi ya Mambo ya Nje, Zanzibar ikielezea kuwa Humoud alikuwa ni mwanadiplomasia aliyekuwa mwambata wa balozi mdogo wa Oman Zanzibar, hivyo alikuwa na kinga ya kutoshitakiwa, rejea Kimbatanisho namba KTN 24, ya Idara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwenda kwa Kamishna wa Polisi Zanzibar.

Kwa kuwa Kamati ilikuwa katika njia panda ya kuamini kauli ipi ni sahihi, kati ya ile ya serikali iliyotolewa Barazani na Mhe. Haroun Ali Suleiman kuwa Humoud hakuwa mfanyakazi wa Ubalozi au ile ya uchunguzi wa Polisi kuwa Humoud ni mfanyakazi wa Ubalozi wa Oman, Kamati nayo iliamuwa kutaka ukweli kwanza kwa kumwita Mhe. Haroun mnamo tarehe 02 Januari, 2015 atoe maelezo yake pamoja na mengine aseme kama kauli yake inabakia vile vile au la, na Mhe. Haroun aliijibu Kamati kuwa maelezo yake yanabakia vile vile.

Katika hatua nyengine, Kamati ilifanya jitihada ya kuthibitisha maelezo ya uchunguzi wa Polisi kwa kuiandikia Idara ya Mambo ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa barua ya tarehe 20/01/2015 ikitaka maelezo ya wasfu wa Humoud na mnamo tarehe 23/01/2015 Idara hiyo iliijibu Kamati kupitia kwa Katibu wa Baraza kuwa Humoud alikuwa ni mfanyakazi wa Ubalozi mdogo wa Oman ambaye aliingia Tanzania mnamo tarehe 26/04/2012 na kuondoka mwezi Disemba, 2014 baada ya kumaliza muda wake.

Kamati ilipochambuwa taarifa hizo mbili ilibaini kuwa maelezo ya Polisi ya uchunguzi yalikuwa ni sahihi. Hivyo Kamati imeona kuwa maelezo ya Mhe. Haroun Ali Suleiman, alipokuwa akisema Barazani kwa niaba ya Serikali, hayaendi sambamba na masharti ya kanuni 59 (3) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2012, ambazo zinakataza mjumbe yeyote kutoa maelezo yasiyo sahihi ya kubuni au kubahatisha.

Katika uhusika wa Humoud, Jeshi la Polisi katika uchunguzi wake lilishauri kitaalamu kuwa kwa kuwa kuna ushahidi wa kimazingira unaomuhusisha Humoud na wizi wa nyaraka basi taratibu halali za kisheria zitumike kuwezesha kupatikana kwake ili ahojiwe na hatimaye hatua stahiki zichukuliwe dhidi yake.

Jeshi la Polisi lilishauri kuwa Serikali ipeleke ombi la kuvuliwa kinga ya kidiplomasia ya Humoud na kuwezesha kujibu tuhuma za wizi wa nyaraka za Serikali, shauri ambalo halijafanyiwa kazi kwa uzito unaostahiki mpaka hivi sasa, rejea Kimbatanisho namba KTN 24.

### c. Maslahi ya nchi yamezingatiwaje katika kushughulikia kadhia ya wizi wa nyaraka

Kadhia nzima ya tukio la wizi wa nyaraka limekuwa pana na katika kulishughulikia hasa kutokana na kuhusika kwa mtendaji wa ubalozi mdogo wa nchi ya Oman hapa Zanzibar, ambayo bila ya shaka yoyote ni moja ya nchi zenye mahusiano mazuri na Zanzibar kwa karne nyingi sasa.

Hakuna anayebisha kuwa mahusiano haya ni muhimu na yanahitaji kuendelezwa na kudumishwa kwa hali yoyote ile. Wala hakuna anayekataa kuwa nchi hizi mbili zina maingiliano ya kidamu baina ya watu wake kutokana na historia yake.

Kila mtu atakubali kuwa uhusiano huu baina ya nchi mbili hizi siku zote umekuwa katika misingi ya uadilifu, haki na kuheshimiana bila ya kujali uwezo, ukubwa na hadhi za nchi zetu, na katika misingi hiyo ndiyo uhusiano huu umekuwa imara na mzuri kwa miaka yote. Kamati inaamini kuwa kuchezewa misingi hii ya uhusiano wetu na Oman ni kuhatarisha mahusiano yenyewe, ni maoni ya Kamati kuwa hili lisiachiwe litokee kwa kuwa Zanzibar na Oman zinahitajiana kila mmoja, aidha ni maoni ya Kamati kuwa watendaji wa nchi zetu wasiachiwe waiharibu misingi hii ya mahusiano kwa maslahi yao binafsi.

Tunaamini kuwa kitendo kinachodaiwa kufanywa na Humoud cha kuwarubuni watendaji wa Taasisi ya nyaraka kuibia nyaraka za Serikali ni kitendo chake binafsi hakina Baraka yoyote ya nchi ya Oman.

Siku zote Taifa la Oman limekuwa likiendesha mahusiano baina yetu kwa misingi tuliyoitaja hapo juu ya uadilifu, haki na kuheshimiana, Humoud kwa kushirikiana na baadhi ya watendaji wa Taasisi ya nyaraka, amejitokeza kutaka kuichafua misingi hiyo.

Kamati inaona kuwa si Oman wala Zanzibar iliache suala hili liende anavyotaka Humoud na wenzake kwa kuichafua misingi mizuri ya mahusiano yetu.

Kamati inaamini kuwa maslahi ya nchi zetu lazima yalindwe dhidi ya ukorofi wa watendaji wetu bila ya kuona haya wala kuoneana muhali, ikitokezea mtu wetu kutoka Zanzibar amefanya uharibifu Oman kwa

jina na cheo chake hatua stahiki zichukuliwe kwa mujibu wa sheria, kadhalika na wenzetu wa Oman wafanye hivyo hivyo kwa upande wa Zanzibar.

Wakati wa kufanya uchunguzi Kamati ilitumia muda mwingi kupambanuwa hoja zifuatazo:-

i. Humoud ni nani?;
ii. Kwanini ametajwa kuhusika katika kadhia ya wizi wa nyaraka za Zanzibar;
iii. Hatua za uchunguzi wa tuhuma za wizi dhidi yake zimefikia wapi;
iv. Kama Humoud alikuwa ni Mwanadiplomasia, alifanyaka kazi yake kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Kinga za Mabalozi na Konsula ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Namba ya mwaka 1986 pamoja na Mkataba wa Vienna wa Kinga za Kikonsula wa mwaka 1963;
v. Kama masharti ya Mikataba ya Kimataifa inayoratibu shughuli za mahusiano ya kibalozi imevunjwa nini shufaa ya nchi iliyoathirika na kuvunjwa kwa masharti hayo; na
vi. Inawezekana kuchukuliwa hatua za kisheria kwa mujibu wa sheria bila ya hofu ya kuharibika uhusiano wa kidiplomasia baina ya Oman na Zanzibar (Tanzania) kama nayo ni hoja.

Katika kujibu hoja ya kwanza, Kamati iliridhika kuwa Humoud alikuwa ni mfanyakazi wa ubalozi mdogo wa nchi ya Oman hapa Zanzibar kuanzia 26/04/2012 mpaka mwezi Disemba 2014 kama ilivyothibitishwa na Idara ya mambo ya Nje, Afisi ya Zanzibar na kinyume na maelezo ya Mhe. Haroun Ali Suleiman alipoliambia Baraza hili kuwa kijana huyu (Humoud) hakua mfanyakazi wa ubalozi mdogo wa Oman isipokuwa ameletwa na Serikali yake kwa kazi za kushughulikia ukarabati wa Beit el ajab.

Kamati imetaka kujua pia wasfu wa Humoud na katika kutafuta huko imebaini kuwa kabla ya mwaka 2012 mwaka ambao Humoud alikuja kama afisa balozi, alishawahi kuja Zanzibar kwa awamu mbili na awamu ya tatu akaja kupitia ubalozini vile vile.

Katika awamu ya kwanza Humoud aliletwa Zanzibar na Serikali ya Oman mnamo tarehe 15/7/2005, kutoka Wizara ya Mila na Utamaduni ya Oman, kwa ajili ya kuendeleza kazi za udhibiti na uhifadhi wa nyaraka zinazohusu historia ya Oman. Katika barua hiyo pia ilielezwa kuwa Wizara hiyo ya Utamaduni ya Oman itatoa baadhi ya vifaa vya kuendeleza uhifadhi huo kama zawadi kupitia kwa Humoud, rejea Kiambatanisho namba KTN 25, katika barua ya Ubalozi Mdogo wa Oman kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Katika mahojino na wafanyakazi wa Taasisi ya Nyaraka, walieleza Kamati kuwa walimfahamu Humoud muda tokea mapema katika miaka ya 2005 na 2006, katika kipindi hicho Humoud alikuwa akija katika Taasisi ya Nyaraka na kuomba kupatiwa nakala kivuli za nyaraka mbali mbali ambazo alipatiwa.

Baada ya kipindi hicho Humoud aliondoka na kuja tena katika kipindi cha baina ya mwaka 2007 na 2008, Kamati ilielezwa na watendaji wa nyaraka ambao wakimfahamu vizuri, kuwa katika kipindi hicho cha awamu ya pili Humoud alitaka tena kupatiwa nakala kivuli za nyaraka kama ilivyokuwa katika awamu ya mwanzo, hata hivyo hakufanikiwa kupatiwa kwa kile Kamati ilichoelezwa kutofautiana na Mkurugenzi wa Taasisi ya Nyaraka.

Kamati ilipomuhoji Mkurugenzi alisema hamfahamu Humuoud, isipokuwa anamtambua kwa kuwa alikuwa akiambatana na ujumbe wa Oman ulipotembelea Taasisi ya Nyaraka na mara kadhaa alimuona Wizarani.

Katika awamu ya tatu ya mwaka 2012 Humoud alikuja kwa mlango wa ubalozi kama ilivyotangulia kuelezwa. Kamati ilielezwa kuwa Humoud alikuwa na mahusiano makubwa na Mkurugenzi wa Taasisi ya Nyaraka na baadhi ya watendaji wengi wa nyaraka, ingawa Mkurugenzi wa Nyaraka alikanusha kuwa na mahusiano hayo na Humoud.

Baadhi ya wafanyakazi hao waliambia Kamati kuwa mahusiano hayo yalikuwa makubwa kiasi ambacho Humoud mara kadhaa akija na zawadi ndogo ndogo na kuwapatia baadhi ya wafanyakazi hao kama vitambaa, tende nk.

Kamati pia ilielezwa na mmoja ya wafanyakazi aliyefuatwa na Humoud na alimpa ahadi kwamba iwapo atafanikisha kuiba nyaraka na kumpatia angeliyabadilisha maisha yake kama ilivyo kwa mabosi wake. Kamati ilipomuuliza ni mabosi wepi aliokusudia Humoud, mfanyakazi huyo alisema ni wakuu wa Taasisi yake ya Nyaraka.
Kamati ilipokuwa inachanganuwa taarifa hizi ilibaini yafuatayo:-

i. Katika awamu zote alizokuja, Humuod alikuja kwa kazi inayofanana kuhusu nyaraka zilizopo katika nyumba ya nyaraka kilimani;
ii. Katika awamu zote alizokuja, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inataarifa ya ujaji wake wa awamu ya kwanza tu ya 2005, pale ubalozi mdogo wa Omani ulipoleta taarifa rasmi na madhumuni ya kuja kwake, rejea Kiambatanisho namba KTN 25;
iii. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haikuwa na taarifa ya ipi hasa hadhi ya Humoud katika awamu ya tatu aliyokuja, rejea maelezo ya Waziri Haroun katika Kiambatanisho namba KTN 20;
iv. Huenda Humoud alifanyakazi za kiuchunguzi kwa vile aliweza kupata fursa kubwa ya kuijuwa Taasisi ya Nyaraka, ambapo imesaidia kufanikisha wizi wa nyaraka zenyewe;
v. Kwa fursa aliyopata ya kuifikia Taasisi ya Nyaraka na kujuana na Wakuu na watendaji wa Taasisi hiyo, Humoud aliweza kuifahamu Taasisi hiyo na watendaji wake kwa kina sana;
vi. Humoud alikuwa na uhuru wa kuifikia Taasisi ya Nyaraka anavyopenda; na
vii. Kutokana na tuhuma za wizi kuibuka katika kipindi cha karibuni upo uwezekano mkubwa kuwa Humoud amekuwa akijihusisha na tabia hizo katika awamu zote alizokuja.

Katika hoja ya pili, Kamati ilitaka kujuwa kwanini Humoud amehusishwa na tuhuma za wizi wa nyaraka. Katika kujibu hoja hii Kamati imetafakari vizuri uchunguzi uliofanywa na Jeshi la Polisi ambao umethibitisha kuwa Humoud ametajwa na watendaji wa Nyaraka waliohusika katika wizi huo rejea Kimbatanisho namba **KTN 23**.

Katika taarifa hiyo ushahidi wa kimazingira unaoungwa mkono na kauli za watendaji wanaodaiwa kushirikiana naye unaonyesha wazi kuwa alikuwa ni mmoja ya watuhumiwa muhimu katika wizi wa Nyaraka ndani ya taasisi hiyo.
Kamati imepitia taarifa mbali mbali na vielelezo ambavyo bila shaka yoyote vinamhusisha Humoud na tukio hilo, katika kipindi hicho cha mwezi wa Julai , Agosti na Septemba, 2013, matendo ya Humoud katika Taasisi ya Nyaraka yalikwenda sambamba na matokeo ya wizi wa nyaraka zenyewe hapo baadaye.

Katika kipindi cha mwezi wa Julai 2013, Humuod aliongoza ujumbe wa Oman kupitia Ubalozi ambao ulifika katika Taasisi ya Nyaraka na Kukagua maeneo mbali mbali katika chumba cha Hifadhi yaani kile chumba kikubwa cha kuhifadhi nyaraka. Kamati iliambiwa na wafanyakazi wa Nyaraka kuwa wizi wa nyaraka ulitokezea katika maeneo yale yale ambayo ujumbe huo ulikaguzwa na Humoud akiwemo.

Ujumbe huo ulioneshwa nyaraka mbali mbali zikiwamo nyaraka za tawala za kisultani husani katika kipindi cha utawala wa Sayyid Barghash bin Said na Masultani wengine. Madhumuni ya ujumbe huo yalikuwa katika mwenendo wa utekelezaji wa makubaliano ya ushirikiano wa kutunza na kuhifadhi nyaraka (*MoU*) yaliyokusidiwa kusainiwa baina ya Serikali ya Zanzibar na Oman.

Kamati iliarifiwa kuwa awali kulikuwa na makubaliano ya aina hiyo baina ya Serikali ya Oman na Serikali ya Zanzibar ambayo yalisainiwa mnamo tarehe 17/08/2010 wakati huo Taasisi ya Nyaraka ikiwa

chini ya Wizara ya Elimu, Utamaduni na Michezo. Rejea Kiambatanisho namba KTN 26, kuhusu mkataba wa makubaliano ya Zanzibar na Oman '*MoU*'.

Mara kadhaa ubalozi mdogo wa Oman umekuwa ukikumbusha na kuhimiza uwekaji saini mkataba huo. Rejea Kiambatanisho namba KTN 27, kuhusu barua ya ukumbusho wa kusainiuwa makubaliano hayo kutoka Ubalozi Mdogo wa Oman ya tarehe 22/2/2007.

Kamati ilielezwa kuwa makubaliano ya mwaka 2010 yalifanyiwa marekebisho baadae wakati Taasisi ya Nyaraka ikiwa chini ya Wizara ya Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, nyongeza hiyo ya marekebisho ya makubaliano hayo hayakusainiwa kwa kuwa uongozi wa Wizara wa wakati huo haukuafiki baadhi ya vipengele vya nyongeza hiyo, vilivyonekana kwenda kinyume na maslahi ya nchi.

Mnamo tarehe 5/01/2015, Kamati ilimwita na kumhoji aliyekuwa Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Haji Omar Kheir ambaye alieleza Kamati kuwa katika kipindi hicho, nyongeza ya makubaliano ya mkataba huo hayakusainiwa kutokana na kuwamo kipengele kilichoweka sharti kwamba katika kubadilishana nyaraka upande wa pili (Oman) upate fursa ya kupatiwa nyaraka bila ya kuwapo taratibu za kawaida.

Mhe. Haji Omar Kheir, aliambia Kamati kuwa hilo hawakuwa tayari kufanya na walitaka kifanyiwe marekebisho ambayo hayakuwahi kufanyika baada ya kutokea mabadiliko ya Baraza la Mawaziri mwezi Ogasti, 2013 na yeye kuondoka katika Wizara hiyo, huku makubaliano hayo yakiachwa kwa ajili ya ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Rejea Kimbatanisho namba KTN 28, kuhusu nakala ya makubaliano hayo ambayo hayajawekwa saini.

Kutokana na kuchelewa kusainiwa nyongeza hiyo ya makubaliano, Ubalozi mdogo wa Oman umekuwa ukikumbusha mara kwa mara kuhusu kusaniwa makubaliano hayo. Hata hivyo, baada ya tukio la wizi wa nyaraka kutokea si Ubalozi mdogo wa Oman wala Humoud aliyekumbushia tena kusaniwa makubaliano hayo. Kama hiyo haitoshi, kipindi kifupi tu baada ya kadhia hiyo Humoud aliondoka nchini.

Kamati iliambiwa katika kipindi hicho, kuwa wakati utiaji saini wa makubaliano hayo unasubiriwa, Humoud alijichomoza tena kwa kuwatafuta watendaji wa Afisi ya Nyaraka na kuwashawishi waibe nyaraka hizo na kumpatia yeye kwa malipo ya fedha nyingi.

Ndugu Omar Shehe Khamis ambaye ni Afisa Mwandamizi katika Taasisi ya Nyaraka aliiambia Kamati kuwa alipigiwa simu na Humoud ambaye anamfahamu lakini hakupokea simu hiyo mara kadhaa alipopigiwa, alifafanuwa kuwa baadae alikutana na Humoud akiwa Beit-el-Ajab alipokwenda kwa shughuli zake za kujistarehesha jioni na familia yake na Humoud alilalamika kwa ndugu Omar kuwa amekuwa akimpuuza na hakuwa akipokea simu zake.

Kamati ilipomuhoji ndugu Omar kwa nini hakupokea simu za Humoud, alisema kuwa amekuwa na mashaka na Humoud na hakutaka kushughulika naye kwa vile alihofu angelimtumia vibaya kwa maslahi yake.

Humoud hakutosheka na hapo lakini pia alimtafuta ndugu Fuad Abdalla ambaye nae pia anafanyakazi *'search room'* katika Taasisi ya nyaraka, ndugu Fuad Abdalla alieleza Kamati kuwa alipigiwa simu na mtu asiyemfahamu akimtaka wakutane naye kwa kuwa anashida naye muhimu. Ndugu Fuad Abdalla aliongeza kuwa alimtaka mtu huyo wakutane eneo la Kilimani karibu na Afisi ya Nyaraka majira ya asubuhi saa 4:00 na walipokutana na mtu huyo alikuwa kwenye gari aina ya Prado na alijitambulisha kuwa yeye ni Humoud ana mazungumzo muhimu na yeye (Fuad Abdalla).

Ndugu Fuad Abdalla aliendelea kuifahamisha Kamati kuwa alipakiwa kwenye gari mpaka kwenye mkahawa mmoja hapo Kiembe Samaki na wakiwa Mkahawani hapo, Humoud alimtaka Fuad Abdalla ampatie nyaraka kutoka Taasisi ya Nyaraka na kwa kufanya hivyo angelifaidika kwa kumpa fedha nyingi ambazo zingelibadilisha maisha yake kama ilivyo kwa mabosi wake, ndugu Fuad Abdalla alisema kuwa alimwitikia Humoud ambaye alimsisitiza akubali na alipoondoka, Humoud alimpatia Fuad Abdalla shilingi elfu ishirini (20,000/=).

Katika maelezo yake mbele ya Kamati ndugu Fuad Abdalla alisema alishindwa kutekeleza ombi la Humoud kwa kuwa hakuona kama kitu cha busara kufanya kitendo hicho na kuhatarisha kazi yake ambayo ameajiriwa siyo miaka mingi. Ndugu Fuad Abdalla alieleza kuwa alikata mawasiliano na Humoud kwa kuifunga (*block*) namba yake ya simu ya mkononi na akawa hawasiliani naye tena.

Mfanyakazi mwengine ambaye Humoud aliwasiliana naye ni ndugu Khadija Idd Mohamed ambaye naye anafanyakazi katika '*search room'* katika Taasisi ya Kuhifadhi Nyaraka Kilimani.

Ndugu Khadija Idd Mohamed aliambia Kamati kwamba katika kipindi cha karibu na tukio la wizi wa nyaraka alipigiwa simu na mtu asiyemfahamu nyakati za usiku mtu huyo alijitambulisha kuwa yupo maeneo ya Kiembe Samaki na alimtaka wakutane ana shida muhimu, Khadija Idd Mohamed alisema kuwa hakukubaliana na wito huo kwa vile yeye ni mtu mwenye familia na asingeliweza kutoka katika nyakati hizo za usiku kufuata wito wa mtu asiyemjua.

Alipowasimulia baadhi ya wafanyakazi wenzake mmoja wao alimwambia Khadija Idd Mohamed kuwa huyo huenda ni Humoud na bora asishughulike naye kwa kuwa anaweza kumsababishia matatizo. Wakati lilipobainika tukio la wizi na kujulikana kuwa Humoud alishawishi matokeo yake, ndugu Khadija Idd Mohamed alitoa taarifa kwa uongozi wa Taasisi kuhusu yeye kupigiwa simu na mtu asiyemfahamu akitaka kukutana naye Kiembe Samaki.

Ndugu Khadija Idd Mohamed alionesha namba ya simu hiyo aliyopigiwa na ilipoangaliwa iligundulika kuwa ni namba hiyo hiyo waliyopigiwa wafanyakazi wengine kushawishiwa kuiba nyaraka na namba hiyo ilikuwa ikitumiwa na Humoud Abdulla Al Rashidy.

Mbali na mazingira hayo ambayo yanaashiria vya kutosha ushawishi wa Humoud katika tukio hilo la wizi wa nyaraka hakuishia kwa watendaji hao alifanya mawasiliano kwa mfanyakazi mwengine wa chumba cha uhifadhi nyaraka aitwaye ndugu Mwanakombo Ali Haji.

Mfanyakazi huyu ni miongoni mwa watuhumiwa katika kadhia ya wizi wa nyaraka ambaye katika maelezo na vielelezo mbali mbali vinaonyesha kuwa alikuwa akiwasiliana na Humoud mara kadhaa na kufanikisha wizi wa nyaraka hizo.
Katika mahojiano na ndugu Moza Zahran Mohamed ambaye ni Afisa Mwandamizi katika Taasisi hiyo ya Nyaraka aliambia Kamati kuwa katika nafasi yake katika chumba cha uhifadhi Ndugu Mwanakombo alikiuka taratibu za kazi zinazohusika katika chumba hicho kwa kuwa alikuwa akiingia na mikoba na akitumia muda mwingi katika chumba hicho bila ya kazi maalumu.

Kamati pia imegundua wakati wa uchunguzi wa tukio hilo kuwa Humoud alifanya mawasiliano ya simu na ndugu Mwanakombo Ali Haji ambayo katika kipindi hicho cha miezi mitatu yalikuwa kwa kiwango kikubwa, ambapo inadaiwa wamewasiliana katika maeneo tofauti mara zaidi ya 127. Rejea Kiambatanisho namba KTN 21, nakala ya kumbukumbu ya mawasilano ya simu baina ya Mwanakombo na Humoud.

Kwa maelezo hayo, Kamati imeona kwamba kuna mazingira tofauti yanayomuhusisha Humoud na tukio la wizi wa nyaraka.

Katika kujibu hoja ya tatu ya hatua za uchunguzi dhidi ya Humoud zilipofikia, Kamati iliridhika kuwa Humoud kwa kiasi kikubwa amejihusisha na matukio ya wizi wa nyaraka.

Kamati imepata kumuhoji Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai wa Mkoa wa Mjini/Magharibi (*RCO*) na alithibitisha mbele ya Kamati kuwa uchunguzi wao umebaini kuwa Humoud alihusika na kama kinga aliyonayo ingeondolewa wangeliweza kumuhoji na kumshitaki pamoja na wahusika wengine.

Aidha, *RCO* alieleza kuwa Polisi wangeliweza kufika mbali zaidi katika uchunguzi wao iwapo wangelipata fursa ya kumuhoji Humoud na kutokana uchunguzi wao walikuwa na hakika na uhusika wa Humoud ndiyo maana walishauri Serikali imuondolee kinga ya kibalozi ili wapate kumuhoji na hatua stahiki zichukuliwe dhidi yake.

Akitoa maelezo hayo mbele ya Kamati, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mjini Magharibi (*RPC*) kamishna msaidizi ndugu Mkadam Khamis Mkadam alisema Jeshi la Polisi lilitaka ushauri kutoka Idara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ya Zanzibar wa kujua hadhi ya Humoud na Idara hiyo ilijibu Jeshi la Polisi mnamo tarehe 11/02/2014.

Katika jibu hilo Idara hiyo ilieleza Jeshi la Polisi kuwa suala la Humoud lilifikishwa Makao Makuu ya Wizara ya Mambo ya Nje, Dar es Salaam ambao walieleza kuwa Humoud alikuwa ni Afisa wa Ubalozi mdogo wa Oman na kwa sasa hawezi kushitakiwa au kuhojiwa na Polisi au vyombo vya ulinzi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu ya kinga aliyonayo akiwa ni mwanadiplomasia wa kigeni kwa mujibu wa Makubaliano ya Vienna juu ya Mahusiano ya Kidiplomasia ya mwaka 1961, *(Vienna Convention on Diplomatic Realations of 1961)* na sheria ya Kinga na Fursa za Kidiplomasia na Kikonsula Na.5 ya 1986 *(Diplomatic and Consular Immunities and Privileges Act No.5 of 1986)*

Aidha, barua hiyo ilieleza kuwa kama Polisi wanataka kumkamata na kumuhoji Humoud, lazima wakusanye ushahidi wenye nguvu na kuwasilisha Wizara ya Mambo ya Nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ndiyo itakayoandaa ombi kwa Serikali ya Oman la kumuondolea kinga Humoud.

Katika hatua ya uchunguzi wa taarifa mbali mbali kuhusu Humoud Kamati imebaini kuwa:-

i. Waziri Haroun Ali Suleiman alipitikiwa sana kumuhoji ndugu Humoud kienyeji kwa vile Polisi ndiyo ilikuwa ifanye kazi hiyo kitaalamu na kwa mujibu wa sheria. Kauli ya Waziri Haroun Ali Suleiman kuwa alimuhoji kijana huyo na kukataa kuhusika haikuwa sawa kwa kuwa angalisaidiana na Jeshi la Polisi kufanikisha azma yao ya Kumuhoji kwa kusaidia taratibu za kuondolewa Kinga yake. Rejea Kiambatanisho namba KTN 20.

ii. Ushauri wa Jeshi la Polisi ambalo limefanyakazi kubwa ya upelelezi wa suala hili na kutaka Humoud aondolewe kinga ya kibalozi, haukufanyiwa kazi inavyostahiki.

iii. Licha ya Kamati kuelezwa na Mhe. Haroun kuwa suala hili limeshafikishwa Wizara ya mambo ya Nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, bado hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa mpaka sasa na Kamati imepata taarifa kuwa Humoud amekuwa akija na kuondoka Zanzibar mara kadhaa na hakuna chochote kinachoendelea dhidi yake*,* vile vile, majibu ya Idara ya Mambo ya Nje, Afisi ya Zanzibar hayaonyeshi kuwa kuna hatua za maana zinazochukuliwa dhidi ya Humoud.

iv. Idara ya Mambo ya Nje kutaka upatikane ushahidi wenye nguvu inatia shaka na utayari wa kushughulikiwa suala lenyewe, kwa vile mpaka hatua iliyofikiwa ushahidi wa kimazingira ulitosha kwanza kukamatwa Humoud kwa mahojiano ambayo ndiyo yangewezesha kutilia nguvu

ushahidi wa kimazingira, ikiaminika kuwa Polisi wangelikwenda mbali zaidi ya kumuhoji na kumfanyia upekuzi.

Kamati bado ina imani na hatua ya uchunguzi wa Jeshi la Polisi kwa vile ulikuwa unapahala pa kuanzia na walihitaji kumaliza vile vile. Imani ya Kamati kwa Jeshi la Polisi inakuja kwa kuwa Jeshi la Polisi limefanyakazi hiyo kwa umakini na timu ya uchunguzi ilikuwa imehusisha vyombo muhimu vya haki na jinai na kuja na hitimisho la kuwapata watuhumiwa wa uhalifu wa tukio hilo akiwamo Humoud.

Ni masikitiko yetu kuwa nguvu na weledi wa Jeshi la Polisi umebezwa kwa kutofuatwa ushauri wao baada ya uchunguzi wa muda mrefu kuhusu kadhia hii.

Aidha, Kamati imegunduwa kuwa kuna hali ya shaka au hofu kwa baadhi ya viongozi wa Serikali kutekeleza wajibu wao katika kulishughulikia suala hili kwa mfano, mnamo tarehe 02/01/2015, Kamati ilimwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Mohamed Aboud Mohamed na kutaka kujuwa taarifa ya uchunguzi na hatua zilizochukuliwa baada ya uchunguzi wa Polisi na Mamlaka ya Rushwa na Mhe. Mohammed Aboud Mohammed alisema kuwa suala hili halifahamu na hajawahi kusikia katika ngazi za juu ya Serikali, alisema na kuonesha wazi wazi kuwa suala hili linaweza likaharibu uhusiano baina ya nchi yetu na Oman kama halitashughulikiwa kwa uangalifu.(*Makofi*)

Kamati ilishtushwa kuona kuwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambayo inaratibu mambo ya Muungano ikiwemo na vyombo vyake haina taarifa kuhusu kazi iliyofanywa na Jeshi la Polisi katika kadhia nyeti kama hiyo. Kamati iliamini kuwa kauli hiyo ni ya wasi wasi wa Serikali na kuchelea kuchukuwa hatua za haraka kwa wahusika muhimu wa tukio la wizi wa nyaraka.

Kamati ilipata shaka kuamini kuwa Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais haifahamu hatua za uchunguzi zilipofikiwa kwa vile ilipata taarifa ya Polisi kuhusu hatua za upelelezi huo mbayo ilipelekwa kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais na Utumishi wa Umma na anuani ya taarifa hiyo ikionesha kuwa alipewa Katibu wa Rais, Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora.

Kamati inaamini kuwa Serikali katika ngazi za juu inajuwa hatua ya uchuguzi ilipofikiwa na kwa hivyo, ilijuwa kuwa Jeshi la Polisi lilitoa ushauri kwa Serikali ambao haukupata mrejesho wowote. Rejea Kiambatanisho KTN 23, kuhusu barua ya Kamishna wa Polisi kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais na Utumishi wa Umma na Katibu Mkuu wa Rais, AR Ikulu na Utawala Bora.

Katika hoja ya nne ya suala la Humoud, Kamati ilitaka kujiridhisha kutokana na vielelezo na maelezo iliyoyapata kuhusu Humoud kama wakati akifanyakazi kama mwanadiplomasia alizingatia na kufuata masharti ya Sheria namba 5 ya mwaka 1986 na Mikataba ya Kimataifa inayoratibu Mahusiano ya diplomasia na Kikonsula. Rejea Kiambatanisho namba KTN 29, kuhusu Sheria namba 5 ya mwaka 1986 ikijumuisha jadweli zenye Mikataba ya Kimataifa ya *VCDR 1961* na *VCCR 1963.(Makofi)*

Katika hoja hii Kamati ilipitia na kuichambua mikataba hiyo na kupima matendo ya Humoud kama yalikuwa yanafuata masharti ya sheria na mikataba hiyo. Hata hivyo, Kamati ilipochambua sheria na mikataba hiyo imegunduwa kuwa Mkataba unaohusu kinga ya Humoud ni mkataba wa Kimataifa wa Mahusiano ya Kikonsula wa mwaka 1963, *Vienna Convention on Consular Realations 1963 (VCCR 1963)* na siyo mkataba wa Kimataifa wa Mahusiano ya Kidiplomasia wa mwaka 1961 *(Vienna Convention on Diplomatic Relations 1961)* kama ilivyoelezwa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa wakati wakijibu barua ya Jeshi la Polisi kupitia Idara ya Mambo ya Nje Zanzibar.

Katika mkataba wa Kimataifa Kuhusu Mahusiano ya Kikonsula wa mwaka 1963 ambao ndiyo makubaliano ya Kimataifa yanayoratibu shughuli za Balozi ndogo za nchi umegawanya majukumu tofauti

na yale ya Mkataba wa Kimataifa Kuhusu Mahusiano ya Kidiplomasia wa mwaka 1961 ambao Idara ya Mambo ya Nje ilihusisha kinga ya Humoud.

Kwa mujibu wa Mkataba huo wa mwaka 1963, jukumu kubwa la Balozi ndogo ni kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 5, kwamba Balozi ndogo zitakuwa na jukumu la kulinda maslahi ya nchi yake kwenye nchi ambayo ubalozi huo mdogo upo, lakini msisitizo wa kazi zao unajikita zaidi katika masuala ya kiutawala na kiufundi na wala haujihusishi na masuala makuu ya kimahusiano kama vile ya ngazi za juu za kiutawala ambayo ubalozi mkuu unahusika kwa mujibu wa Mkataba wa Kidiplomasia wa mwaka 1961 (*VCDR*).

Aidha, Mikataba yote hiyo, pamoja na kutoa fursa na kinga nyengine, pia imetoa kinga ya kutoshitakiwa, kusachiwa na kuhojiwa na vyombo vya usalama kwa makosa watakayofanya wanadiplomasia, wakiwa na hadhi ya kidiplomasia au wakiwa wanatekeleza kazi za kidimplomasia kwa mujibu wa mkataba wa kidiplomasia kwa mabalozi wadogo na maafisa wao.

Hata hivyo, mkataba wa mwaka 1963 pia umeweka wajibu wa mabalozi wadogo na maafisa wao, wakiwa katika nchi wanazofanyia kazi na wakiwa wanapata fursa na kinga kutokana na kazi zao, basi waheshimu Sheria na Kanuni za nchi waliyofikia pamoja na wajibu wa kutoingilia mambo ya ndani ya nchi hiyo.

Katika kutazama kadhia ya Humoud ambaye alikuwa ni mfanyakazi wa ubalozi mdogo, pamoja na masharti yaliyowekwa katika kifungu cha 55 cha Mkataba wa Mahusiano ya Kikonsula (*VCCR*) wa mwaka 1963, Kamati imegunduwa yafuatayo:-

i. Humoud amevunja masharti ya kifungu cha 55 cha mkataba wa mwaka 1963 kwa kushindwa kuheshimu Sheria na Kanuni za nchi iliyompokea ambayo imeweka sharti katika sheria zake kuwa kuiba au kusaidia kuiba Nyaraka za Serikali ni kosa la jinai ambalo yeye amejihusisha nalo.

ii. Humoud amekwenda kinyume na hadhi ya nafasi yake, kwa kujihusisha kwake katika matendo yanayodhalilisha hadhi ya nafasi yake kama afisa wa ubalozi mdogo, na

iii. Humoud amedhalilisha nchi yake ambayo kwa wakati wote na mpaka hivi sasa imekuwa ikiendesha mahusiano yake na Zanzibar kwa uadilifu, haki na heshima.

Kwa hivyo basi, katika hoja hii ya Kamati kama masharti ya sheria zilizomuweka Humoud nchini yamevunjwa, jibu la Kamati ni kuwa masharti hayo siyo yamevunjwa na Humoud, lakini pia yamevurugwa kwa kiasi cha kuaibisha nchi yake na nchi zetu ambazo zimeshaanzisha namna nzuri ya kushirikiana katika suala zima la kubadilishana na kuhifadhi nyaraka na mengineyo.

Kamati ilifikiria hoja ya tano kuhusu shufaa kwa nchi iliyoathirika na kuvunjwa kwa sheria zake na kitendo cha kihalifu kilichoathiri maslahi ya nchi. Katika hili Kamati ilirejea kwenye ushauri waliopatiwa Polisi na Idara ya Mambo ya Nje katika Afisi ya Zanzibar.

Katika ushauri wao walisema kwa mujibu wa Mkataba wa *VCDR* 1961 na sheria namba 5 ya mwaka 1986, ni kuwa Humoud hawezi kuhojiwa wala kushitakiwa kwa kosa la jinai kutokana na kinga anayopata kama mwanadiplomasia.

Katika ushauri huo ambao *RCO* alipohojiwa na Kamati alidhihirisha kutoridhishwa na namna ulivyokuwa mwepesi na kukosa ufafanuzi wa kina, Kamati nayo iliutafakari, ingawa Jeshi la Polisi liliwasilisha ombi lake serikalini kutaka iombe kuondolewa kwa kinga ya Humoud ili ashitakiwe. Rejea Kiambatanisho namba KTN 24, Barua ya Idara ya Mambo ya Nje, Afisi ya Zanzibar kwa Jeshi la Polisi.

Ingawa jambo hilo halijafanyika lakini Kamati kwa kuzingatia maslahi ya nchi na uzito wa tukio lenyewe na hasara ambayo nchi imepata, ambayo haiwezi kurejeshwa kwa thamani nyengine imeuchambuwa na kubaini kuwa:-

i. Majibu ya Idara ya Mambo ya Nje hayakufafanuwa kwa uwazi kuhusu kinga ya Humoud inayolindwa na Mkataba upi kati ya *VDCR 1961, VCCR 1963* na kifungu kipi cha Sheria ya mwaka Na.5 ya 1986.

ii. Kamati imegunduwa kuwa mkataba unaompa kinga Humoud ni wa mwaka 1963 ambao nao umetoa kinga ya kutoshitakiwa kwa Afisa wa Konsula, isipokuwa Afisa huyo anaweza kushitakiwa iwapo atafanya kosa la jinai lililopindukia mipaka '*grave crime'* na chombo cha Mahakama kitowe maamuzi hayo. Rejea kifungu cha 41 (1) cha *VCCR 1963*) katika Kiambatanisho namba KTN 29, uk. 15 wa kiambaanisho hicho.

iii. Idara ya Mambo ya Nje imeiaminisha Polisi kuwa Sheria namba 5 ya mwaka 1986 na Mkataba wa mwaka 1961, yote inampa kinga Humoud, bila kufafanuwa kwa kina mazingira yote kuhusu kinga yake kwa mujibu wa sheria, jambo ambalo halikuwa sawa katika kukishauri chombo kikubwa cha upelelezi kama Polisi.

iv. Kamati pia imebaini kuwa katika suala la kinga na fursa za kidiplomasia kuna tofauti baina ya Mkataba wa Mwaka 1961 kwa Wanadiplomasia na ule wa mwaka 1963, kwa Makonsula (mabalozi wadogo na maafisa wao) ambapo Mkataba wa mwaka 1963 umepunguza masharti ya fursa na kinga hizo kwa mabalozi wadogo na kwamba wanaweza kukamatwa na kushitakiwa iwapo watafanyaka kosa kubwa bila kujali kinga waliyonayo.

v. Katika kufafanuwa kipengele cha 41 (1) cha mkataba wa *VCCR 1963* Kamati imefahamu kuwa ingawa mabalozi wadogo na maafisa wao wanapata kinga ya kutoshitakiwa, lakini imewekwa *'exception'* kuwa wanaweza kushitakiwa iwapo watatenda kosa kubwa (*grave crime)* na mamlaka zenye uwezo za kisheria kutoa maamuzi hayo.

Katika uchambuzi wa ni lipi hasa kosa lililopindukia mipaka *'grave crime'*, Mkataba wa *VCCR 1963* haukutoa tafsiri, wala sheria Namba 5 ya mwaka 1986 haina tafsiri hiyo. Katika sheria za nchi za Jumuiya ya Madola ambazo Zanzibar ni sehemu yake, Kamati ilitazama mfano wa Sheria ya Uingereza ya Mahusiano ya Kikonsuli ya mwaka 1963 (*UK Consular Relations Act* 1968) katika Kifungu cha 1 (2) kinachosomeka katika tafsiri ifuatayo:-

> "Kosa lililopindukia mipaka *'grave crime'* maana yake ni kosa lolote la jinai ambalo adhabu yake ni kifungo kinachopindukia miaka mitano jela".

Kwa tafsiri hiyo, maana yake ni kuwa iwapo Balozi mdogo au Afisa wa ubalozi mdogo atafanya kosa kubwa lililopindukia mipaka katika nchi anayofanyiakazi, basi anaweza kukamatwa na kushitakiwa kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa, unaoratibu Mahusiano ya Kikonsula wa mwaka 1963, ambao umeridhiwa kwa mujibu wa Sheria namba 5 ya mwaka 1986 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayotumika mpaka Zanzibar.

Kwa hivyo basi, Kamati inaeleza kuwa tafsiri ya Kinga ya Humoud kuhusishwa na Mkataba wa Kidiplomasia wa mwaka 1961 ambao haumpi kinga hiyo siyo sawa. Kamati imeona kuwa kama masharti ya sheria hii yangefafanuliwa vizuri kwa Jeshi la Polisi, basi hatua stahiki zingeweza kuchukuliwa mapema kwa Humoud kukamatwa na kuhojiwa na hata kupekuliwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 4 na 11 juu ya sheria Namba 5 ya mwaka 1986.

Katika kujiridhisha na tafsiri hiyo, Kamati ilitazama mfano wa katika kesi mbili za kidiplomasia zilizohusisha matumizi mabaya ya kinga za kikonsula kwa mujibu wa mkataba wa mwaka 1963. Kesi ya kwanza ni ile ya *United States V Khobragade, 14 CR 008, NYLJ* (2014) ambapo mnamo mwezi Disemba, 2013, Afisa wa ubalozi mdogo wa India nchini Marekani alikamatwa na kushitakiwa kwa kosa la kughushi hati ya kusafiria pamoja na unyanyasaji wa mfanyakazi wake wa ndani kosa ambalo alipatikana na hatia.

Katika kesi nyengine ya *United States V Chindawongse, (771 F.2d 840-41 (4th Cir.1985)* ambayo afisa wa ubalozi mdogo wa Thailand nchini Marekani alikamatwa na kupekuliwa na kupatikana na madawa ya kulevya aina ya *Heroin*, alihukumiwa kifungo jela. Katika kesi zote mbili washitakiwa katika kujitetea walidai kinga ya kidiplomasia kwa mujibu wa mkataba wa *VCCR 1963.*

Hata hivyo, tafsiri iliyotolewa na Mahakama ni kwamba mkataba huo hauwapi maafisa wa balozi ndogo kinga kamili (*absolute*) kama ile wanayopewa mabalozi katika mkataba wa kidiplomasia (*VCDR*) wa 1961. Kadhalika, hukumu hizo zimebainisha kuwa mabalozi wadogo na maafisa wao hawapati kinga ya kikonsula kwa matendo yao binafsi, kwa mujibu wa Makubaliano ya Kimataifa ya Mahusiano ya Kikonsula (*VCCR,* 1963).

Katika hoja ya sita ya Kamati, kama hatua zinawezekana kuchukuliwa dhidi ya Humud bila ya kuharibu uhusiano wa Zanzibar na Oman.

Mtazamo wa Kamati katika hili ulishakuwa wazi tokea mwanzoni mwa ripoti hii kuwa, katika kadhia hii nchi zetu zimekuwa katika mahusiano mazuri yanayongozwa katika misingi ya uadilifu, haki na kuheshimiana ambayo imeshikiliwa na historia ndefu ya nchi hizi mbili kwa karne nyingi.

Hivyo, uhusiano huu hauwezi kuvunjika kwa kuchukuliwa hatua za kisheria kitendo cha ubinafsi wa mtu mmoja au wawili ambao matendo yao hayana baraka ya nchi zetu. Kamati inaamini kuwa Humoud kwa vyovyote apojihusisha na kitendo hicho, basi alitanguliza ubinafsi wake na siyo maslahi ya nchi yake wala maslahi ya mahusiano ya nchi zetu. Hivyo, kama hatua za kuchukuliwa zitafuata mashariti ya sheria, basi suala hilo linawezekana likafanyika bila ya nchi zetu mbili kuingia katika mgogoro.

**d. Mambo yaliyopelekea au yaliyorahisisha suala la wizi au upotevu wa nyaraka katika taasisi ya nyaraka.**

Kadhia ya upotevu wa nyaraka katika Taasisi ya Nyaraka na kumbukumbu za Taifa, limesababishwa na mambo mbali mbali. Katika ripoti hii Kamati itaanisha baadhi ya mambo hayo. Kamati katika uchambuzi wake wa maelezo na vielelezo mbali mbali ilivyopata kutoka katika vyanzo tofauti, imeona mambo yafuatayo yamerahisisha kutokea kwa tukio la wizi na upotevu wa nyaraka:-

i. Uzembe na kutojali (*negligence and recklessness)*

ii. Kutokuwepo na mpango imara wa udhibiti wa usalama wa nyumba ya nyaraka.

iii. Usimamizi na uendeshaji mbovu wa Taasisi ya Nyaraka.

iv. Kutokuchukuliwa kwa hatua zinazostahiki kwa matukio ya wizi wa nyaraka yaliyokuwa yakitokea kwa muda mrefu.

v. Taasisi ya nyaraka kutopewa umuhimu unaostahiki kwa muda mrefu.

vi. Kutokuwepo kwa mpango wa ukaguzi wa muda mrefu na muda mfupi.

vii. Ukosefu wa vifaa vya kiusalama kwa muda mrefu.

viii. Ukosefu wa Taaluma ya elimu ya uhifadhi wa nyaraka kwa baadhi ya watendaji wa Taasisi ya Nyaraka, na

ix. Ukosefu wa wataalamu wakutosha katika eneo la uhifadhi wa nyaraka.

Maelezo na ufafanuzi wa kila moja ni kama ifuatavyo:-

**i. Uzembe na kutojali (*negligence and recklessness)***

Taasisi hii, inaongozwa na Mkurugenzi ambaye ndiye msimamizi mkuu wa shughuli zote za kikazi zinazohusiana na taasisi hii. Chini ya Mkurugenzi kuna wasaidizi wake ambao wanatakiwa wamsaidie katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi hiyo. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba katika uendeshaji wa shughuli za afisi hii kuna uzembe umetendeka na ni hali inayoendelea katika taasisi hii.

Kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011 na Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa Nam. 3 ya mwaka 2008, Mkuu wa Taasisi anatakiwa afuatilie utendaji wa taasisi yake na kujua utekelezaji wa majukumu unavyofanyika kwa kila mfanyakazi, jambo ambalo linaonekana halipo kwa kiwango cha kuridhisha katika taasisi hii.

Kutokuwepo kwa ufuatiliaji wa kazi zinavyofanyika ni moja wapo ya hali inayoelezwa hapo juu, Kamati wakati inawahoji watendaji wa taasisi waliieleza kwamba mtuhumiwa wa wizi wa Nyaraka ndugu Mwanakombo Ali Haji ambaye ni mfanyakazi wa chumba cha kuhifadhia nyaraka, pamoja na mfanyakazi mwengine ambaye siye muhusika wa chumba hicho ndugu Mwanahawa Abdalla Ali, walikuwa na kawaida ya kuingia katika chumba hicho bila ya kuwa na kazi maalum, walifikia hatua ya kufanya shughuli zao binafsi kama vile kusukana kinyume na utaratibu wa kazi. *(Makofi)*

Vile vile, Kamati ilielezwa kuwa Ndugu Mwanakombo pia alikuwa na kawaida ya kuingia na mikoba na kutoka na vitu katika chumba cha kuhifadhia nyaraka wakati wa kazi, kitendo ambacho pia hakiruhusiwi kwa mujibu wa taratibu za ofisi.

Kamati inajiuliza wakati haya yote yakitendeka wasimamisi wa taasisi hii walikuwa wapi? Na kwa nini wahusika hawa wasichukuliwe hatua za kinidhamu na kisheria, kwa tabia zao za kukiuka taratibu za kazi.

Kamati imeona kwamba watu waliopewa dhamana ya kusimamia taasisi hii walishindwa kutekeleza wajibu wao kutokana na kushindwa kutekeleza wajibu wao, hatimae kutoa mwanya kwa mutukio ya wizi na hujuma kufanyika.

Wakati Kamati inafanya ukaguzi wa nyaraka zilizopo katika chumba cha kuhifadhia nyaraka, ilielezwa na watendaji, kwamba baadhi ya masanduku yanayohifadhiwa nyaraka zinazohusiana na vitabu vya zamani vya dawa za asili hayajafunguliwa kwa zaidi ya miaka 10 iliyopita na funguo za masanduku hayo anazo Mkurugenzi peke yake, hakuna mtendaji mwengine anaeruhusiwa kuwa nazo. Jambo la kushangaza ni kwamba wakati wa ukaguzi Kamati ilipoomba kupatiwa funguo za masanduku hayo Mkurugenzi alikuwa anasita sita na hatimaye aliwasilisha funguo hizo kwa Kamati.

Baada ya Kamati kusisitiza kupatiwa funguo hizo, Mkurugenzi baada ya kitambo kupita aliamua kuzitoa funguo hizo. Katika ukaguzi uliofanywa na Kamati, baadae Kamati iligundua kwamba, vitabu vingi havimo katika masanduku hayo. Kamati iliona kwamba, vitabu hivyo vimeibiwa kwa sababu vilikuwa havipo.

Kamati ilipomuuliza Mkurugenzi kwa nini amefungia vitabu hivyo na funguo kubaki nazo yeye, alisema kuwa alifanya hivyo kwa kuwa matukio ya wizi yamekuwapo muda mrefu, hivyo, alihofia kuziacha funguo za makabati hayo kwa kila mtu kungesababisha kupotea nyaraka hizo muhimu.

Kamati ilipokaguwa katika masanduku hayo, ilibaini nyaraka muhimu hazipo na maelezo ya wapi zilipo hayakupatikana.

Katika hali ya kushangaza, Kamati pia imebaini kuwa wakati Mkurugenzi wa Nyaraka hayupo ofisini kutokana na ugonjwa, wasaidizi wake walishindwa kuchukuwa hatua za mara moja wakati wafanyakazi wanaotuhumiwa wakitoka na vitu kwenye mikoba kutoka chumba cha uhifadhi.

**ii. Kutokuwepo na mpango imara wa uhifadhi na udhibiti wa usalama wa nyumba ya Nyaraka.**

Hakuna shaka kuwa, kuna nyaraka za Zanzibar zina umuhimu mkubwa katika uhai wa Taifa, ni hazina ya urithi kwa kizazi kinajacho na kilichopo sasa. Watu mbali mbali wakiwemo wataalamu, watafiti, wasomi wa fani mbali mbali na tofauti na wengineo, hupata fursa ya kuzitumia nyaraka zilizopo katika nyumba ya Nyaraka ya Kilimani.

Lakini, jambo la kusikitisha ni kwamba, jengo hili ambalo linahifadhi nyaraka hizo ya zaidi ya miaka mia moja sasa, halina udhibiti wa kutosha wa usalama.

Jengo hili halina utaratibu unaofaa wa kukaguliwa wageni wanaoingia ndani, ili kujua walichokibeba. Kamati imebaini kuwa utaratibu wa kudhibiti funguo muhimu za kuingilia katika chumba cha kuhifadhia Nyaraka *(repository room)* pia haupo vizuri, ambapo Kamati ilielezwa na watendaji kwamba, kikawaida ufunguo wa kuingia katika chumba hicho unawekwa chini ya buku lililopo katika meza na mfanyakazi anaewahi kuja mwanzo anachukuwa ufunguo na kufungua. *(Makofi)*

Wakati Kamati ikiendelea na kazi za ukaguzi katika taasisi ya Nyaraka, iliweza kugundua kwamba jengo hilo halina askari wa ulinzi wenye silaha, ambapo kwa sasa jengo linalindwa usiku na walinzi ambao wanatumia silaha za kienyeji, kama marungu. Hali hii inaweza kupelekea uhalifu ukafanyika na walinzi wakashindwa kujitetea na kujihami kwa kuwa hawana silaha madhubuti.

Vile vile, kuwepo kwa nyumba ya mtu binafsi katika Jumba la Nyaraka ambaye anatumia mlango mmoja na Taasisi hiyo ni suala ambalo linahatarisha usalama wa ofisi hiyo, kwa sababu hii inatoa fursa ya kuingia watu mbali mbali wanaokuja kutembea katika nyumba hiyo.

**Usimamizi na Uendeshaji wa Ofisi ya Nyaraka:**

Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu Nam. 3 ya mwaka 2008 na utaratibu wa kuendesha kazi za Taasisi hii umeelezwa kwa urefu katika Sheria hiyo. Kwa mujibu wa kifungu cha 12 cha Sheria hiyo Mkurugenzi ndiye msimamizi mkuu wa shughuli za Taasisi hiyo juu yake kukiwa na Bodi ya Ushauri inayoteuliwa na Waziri chini ya Kifungu Namba 8 cha Sheria hiyo.

Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba kuna ukiukaji mkubwa wa utaratibu wa usimamizi na uendeshaji wa Taasisi uliowekwa na Sheria hii, hasa kwa upande wa uongozi.

Kushindwa kwa Mkurugenzi kutekeleza majukumu yake kama yalivyoelezwa katika kifungu cha 12 cha Sheria ya Taasisi hiyo, kumepelekea kutokuwepo kwa umakini wa kazi kwa waliobakia kazini hapo. Hasa

ukizingatia kwamba hakukuwa na msimamizi aliyewekwa kwa mujibu wa taratibu za Ofisi kukaimu nafasi hiyo, mtu ambaye angekuwa masuuli kwa mambo yote yanayotendeka katika Taasisi hiyo wakati Mkurugenzi akiwa hayupo Ofisini.

Vile vile, ukosefu wa vikao vya ndani ya ofisi vya kila baada ya muda nao ni tatizo, vikao ni muhimu kwa ajili ya kutathmini utendaji wa Taasisi nzima unavyoendelea. Kamati wakati inawahoji watendaji waeleze ni vipi majukumu ya Afisi yanavyoratibiwa, waliieleza Kamati kwamba hakuna ufuatiliaji unaofanyika kwa kuwa hakuna mikutano ya kiofisi inayofanyika kutathmini utendaji wa kazi za Taasisi.

Kamati inashawishika kusema kwamba, Taasisi hii kwa muda mrefu imekosa uangalizi wa karibu wa kuisimamia kazi zake za kila siku na ndio moja ya sababu za tukio la wizi wa nyaraka katika taasisi hii. Kwa kukosekana usimamizi huo wa karibu, baadhi ya watendaji wamekuwa wakifanya kazi kwa mazowea wakijuwa kwamba hakuna anaewauliza wala kuwaonya kwa tabia hiyo.

Sheria ya Kuanzisha Taasisi hii katika kifungu cha 8, imeanzisha Bodi ya Ushauri ambayo kazi yake ni kumshauri Waziri juu ya uendeshaji mzuri wa Taasisi hiyo. Kamati ilitarajia kwamba kuwepo kwa Bodi ya ushauri ya Taasisi hiyo ingesaidia sana katika kuifanya Taasisi hii iwe katika kiwango kizuri cha utendaji.

Hata hivyo, katika hali ya kusikitisha uendeshaji wa Taasisi hiyo na mwenendo wa matuko, ni wazi kuwa Bodi hiyo haikuwa ikimshauri ipasavyo Waziri, kama alivyokiri mwenyewe Waziri mbele ya Kamati.

Vile vile, Kamati imedadisi uwepo wa Bodi hii ya ushauri wakati matukio ya wizi yanaendelea ndani ya Taasisi hiyo kwa muda mrefu. Je, Bodi imechukua hatua gani ya kumshauri Waziri kuhusu matukio hayo au kumuelekeza Mkurugenzi kuchukuwa hatua stahiki.

Aidha, Kamati imejiuliza kwa nini Bodi haikuweza kumshauri Waziri ipasavyo kwamba kutokuwepo kwa Mkurugenzi Ofisini kwa muda mrefu kunasababisha shughuli kuzorota kwa kazi za ofisi, hivyo, kungehitajika mtu wa kukaimu nafasi hiyo.

Katika kupata ufumbuzi wa maswali hayo Kamati iliandika barua ya tarehe 6/01/2015 kwa Bodi hiyo ambayo kwa wakati huo ilipewa wito na Kamati ili iweze kuja, lakini Bodi ilijibu kuwa imeshamaliza muda muda wake tangu tarehe 23/09/2014. Hata hivyo, katika hali ya kusikitisha wajumbe wawili tu waliyokuwa Bodi hiyo ndiyo walifika mbele ya Kamati ambao hawakuwa na uwezo wa kuendelea na kikao kwa niaba ya wenzao na hivyo Kamati kushindwa kuendelea na kikao hicho. Rejea Kiambatanisho namba KTN 30, kuhusu barua ya wito ya Kamati kwa Bodi.

Kitendo hiki cha Bodi kutofika kwa ukamilifu, kilipelekea Kamati kukosa majibu ya maswali yake hadi sasa ambapo taarifa hii inasomwa mbele ya Baraza lako hili tukufu na kama vile Bodi hiyo ilivyoshindwa kumshauri Waziri ipasavyo, imeshindwa pia kufika mbele ya Kamati kutoa maelezo inavyopasa.

**Kutochukuliwa kwa hatua zinazostahiki kwa matukio ya upotevu wa nyaraka kwa muda mrefu:**

Kamati katika uchunguzi wake imebaini kuwa matukio ya wizi wa nyaraka na uvunjwaji wa taratibu za kiofisi yamekuwa yakitokea muda mrefu katika Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa. Imebainika kwamba makosa kama hayo yamewahi kutokea mara kadhaa katika miaka ya nyuma na wahusika hawakuchukuliwa hatua zinazostahiki.

Katika uchunguzi wake huo kupitia mahojiano ya watendaji mbali mbali wa Taasisi ya Nyaraka, Kamati ilipata taarifa za mtumishi aitwae Ashura Mohammed Ahmed aliyewahi kutumikia Taasisi hiyo kuanzia mwaka 1994 hadi mwaka 2005 ambapo alipatiwa uhamisho wa kwenda Skuli ya Vikokotoni.

Mtumishi huyu aliwahi kutuhumiwa kwa kosa la kuiba nyaraka na ndio sababu iliyopelekea kupewa uhamisho kutoka katika Taasisi ya Nyaraka na kuhamishiwa Skuli ya Vikokotoni.

Kamati imearifiwa kuwa mnamo mwaka 2009 ndugu Ashura Mohammed Ahmed aliomba likizo bila ya malipo kwa ajili ya kwenda Dubai kumfuata mzazi wake ambaye yuko huko kwa ajili ya matibabu. Kamati ilipofuatilia habari zake ili imwite na kumuhoji ilielezwa kuwa mfanyakazi huyu hadi leo hajarudi tena kazini wala hajulikani aliko. Rejea Kiambatanisho namba KTN 31, kuhusu barua ya maelezo ya Ashura Mohammed Ahmed kutoka WEMA.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Nyaraka alieleza kuwa wakati wakiwahoji watuhumiwa wa wizi wa nyaraka walipata maelezo kuwa ndugu Ashura Mohammed Ahmed amekuwa anawasiliana na watuhumiwa hao kwa njia ya simu kupitia *"whatssup"* akijisifu kuwa amefanikiwa kusafiri mpaka nchini Marekani kwa sababu ya (kuiba) Nyaraka tu, huku akiwasikitikia wenzake waliobakia hapo kwa kuzubaa.

Kamati imetafakari taarifa hizo na kuona kuwa hiyo ni athari ya kutokuchukuliwa hatua stahiki dhidi ya uhalifu huo, hatimae uhalifu huo unaendelea na wanaofanya wanashawishi wenzao wafanye.

Kamati ilipomuuliza Mkurugenzi kwa nini alimuhamisha Ashura Mohammed Ahmed badala ya kumchukulia hatua za kisheria, alijibu kuwa hakuwa na ushahidi wa kutosha na alimuhamisha kwa kuwa alikuwa si muaminifu tena. Katika taarifa ambazo Kamati ilizopata kutokana na mahojiano na wafanyakazi Kamati imeelezwa kuwa ndugu Mwanakombo, anayedaiwa kuhusika na wizi wa nyaraka, baada ya tukio hilo naye kabla ya hatua zaidi hazijachukuliwa dhidi yake, alihamishwa kutoka chumba cha uhifadhi nyaraka *(repository room)* na kuhamishiwa *'search room'*, ambako bado alikuwa na fursa ya kufika katika chumba cha uhifadhi nyaraka.

Aidha, zipo taarifa kuwa wapo wafanyakazi wengine waliowahi kuhamishwa na kupelekwa Taasisi nyeingeni za Serikali baada ya kuhusishwa na matukio ya wizi.
Kamati haishangazwi na kuendelea kwa matukio ya wizi katika Taasisi hiyo kwa vile watuhumiwa wote wa wizi wamekuwa wakipewa adhabu isiyolingana na makosa yao kwa kuhamishwa kutoka kitengo kimoja na kwenda chengine au kupelekwa katika Taasisi nyengine ya Serikali. Hali hiyo imekuwa ikijirejea mara kwa mara wakati matukio ya wizi wa nyaraka yanapotokea.

**Taasisi ya Nyaraka kutopewa umuhimu unaostahiki kwa muda mrefu:**

Taasisi ya nyaraka imeanzishwa kwa lengo la kutunza na kuhifadhi nyaraka na kumbukumbuku za Kitaifa hili, hazina iliyopo katika Jumba lile ni ya thamani kubwa sana kwa nchi yetu. Hata hivyo, hali yake ilivyo na hazina iliyomo, Kamati imekuwa ikijiuliza kama kweli Taasisi ya Nyaraka inapewa kipaumbele kulingana na thamani ya kilichokuwemo ndani.

Itakumbukwa kuwa kwa muda mrefu wajumbe wa Baraza hili wamepiga kelele za kuwekwa mitambo ya *CCTV Camera* katika jengo la kuhifadhia nyaraka Kilimani, kama wanavyopiga kelele hivi sasa kwa Serikali kutafuta mashine ya vinasaba (*DNA*) katika kesi za udhalilishaji. Hata hivyo, jambo la kusikitisha mitambo hiyo imewekwa baada ya kwisha kutokea uharibifu wa hali ya juu katika Taasisi hiyo, ni sawa na kusema kuwa imetafutwa fimbo baada ya kuumwa na nyoka.

Wajumbe pia wamesema sana kuhusu uhaba wa vitendea kazi kwa sababu vilivyopo vimechakaa na havifai kuwepo katika Taasisi muhimu kama hii. Kamati imeona Ufinyu wa bajeti inayopangwa na kiwango halisi cha fedha kinachoingiziwa Taasisi hii kwa mwaka ni kidogo sana kiasi kwamba haiwezi kukidhi kujipatia mahitaji ya kiofisi.

Kinachoshangaza zaidi ni kuwa mwaka 2008, Baraza hili limepitisha Sheria ya Taasisi ya Nyaraka ambayo imeweka masharti katika kifungu cha 21(2) cha kuanzisha akaunti maalumu ya fedha ambayo itasimamiwa na Mkurugenzi wa Taasisi ya Nyaraka. Hata hivyo, akaunti hiyo haijaanzishwa na fedha za watafiti kutoka nje zinalipwa katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali huku Taasisi ya Nyaraka ikiambuliwa senti chache za kutoa *photocopy.*

Kamati inaamini kuwa endapo akaunti hiyo ingeanzishwa kwa mujibu wa sheria, na fedha za watafiti wa nje zikalipwa moja kwa moja katika Taasisi hiyo na kusimamiwa vizuri, matatizo mengi ya Taasisi hiyo yangelitatuka bila utegemezi wa Serikali.

Kamati imearifiwa pia kuhusu maslahi madogo wanayopatiwa watendaji wa Taasisi hii, pamoja na fursa finyu za kuwaendeleza kielimu, nayo imesababisha watendaji wa Taasisi hii kujihisi wamesahauliwa na kutothaminiwa.

Aidha, Kitendo cha Serikali kukaa muda mrefu bila ya kuipatia Taasisi ya Nyaraka Bodi ya Ushauri ni kitendo kinachoonyesha jinsi gani Taasisi hii ilivyombali ya macho ya kawaida ya Serikali. Kamati imebaini kuwa Bodi iliyoisha muda wake iliteuliwa mnamo tarehe 16/09/2010 na kumaliza wake mnamo tarehe 23/09/2014. Tangu Bodi hiyo imalize muda wake mpaka leo imepita miezi saba mpaka uteuzi wa Mwenyekiti mpya umefanyika bila ya wajumbe wengine kuteuliwa.

Mhe. Haroun Ali Suleiman aliiambia Kamati kuwa haoni wajumbe wa kuwateuwa ambao wanaweza kumshauri. Kamati inaamini kwamba, mambo hayo huchangia kwa kiasi kikubwa usimamizi unaozorota wa Taasisi hiyo ambayo inakosa vyombo vya juu vya ushauri na usimamizi.

**Kutokuwepo kwa mpango endelevu wa ukaguzi wa Nyaraka wa muda mfupi na muda mrefu:**

Kamati imepata maelezo kuwa Taasisi ya Nyaraka hutakiwa kufanya ukaguzi wa Nyaraka kila baada ya miezi sita, lakini kutokana na uchache wa nyenzo na rasilimali fedha muda huo umekuwa unapita bila ya ukaguzi huo kufanyika.

Katika uchunguzi wake Kamati imegunduwa kuwa ukaguzi unaofanywa na wafanyakazi wenyewe ni wa matukio, mfano ukaguzi uliofanyika mara baada ya wizi kutokea umefanyika baada ya chumba cha uhifadhi kuhamishiwa wafanyakazi wengine ambao walifanya ukaguzi wa kujiridhisha wenyewe tu. Rejea **Kiambatanisho namba KTN 1** cha nakala ya taarifa ya ukaguzi ya wafanyakazi kwa Mkurugenzi.

Kamati pia imeoneshwa taarifa ya ukaguzi uliofanywa na wafanyakazi wa Nyaraka mnamo tarehe 22/08/2014, ukaguzi huo ambao umeorodhesha mkusanyiko wa nyaraka 75 zilizohifadhiwa katika makasha ya chuma, kati ya nyaraka hizo, ni nyaraka nne (4) zilizowekwa alama ya vyema ndizo ambazo zimeonekana na kutambuliwa. Rejea Kiambatanisho KTN 32, chenye orodha ya nyaraka hizo.

Katika ukaguzi wa Kamati uliofanywa kwa muda mfupi maeneo maalumu yameonyesha kuwa Nyaraka nyingi zimepotea. Rejea Kiambatanisho namba KTN 3 mpaka 19 cha ripoti hii. Tafsiri ya Kamati ni kuwa kwa vile ukaguzi haufanyiki kwa wakati, kumekuwa na mwanya mkubwa wa matokeo ya wizi wa mara kwa mara kama ilivyobainishwa na kaguzi ilizofanyika katika maeneo machache ya Taasisi hiyo.

**Ukosefu wa taaluma ya uhifadhi wa nyaraka kwa wafanyakazi wengine:**

Uhifadhi, utunzaji na usimamizi wa matumizi ya nyaraka ni suala linalohitaji utaalamu wa hali ya juu. Wahusika wanaofanya kazi hii wanatakiwa kuwa na utaalamu wa masuala ya Nyaraka, hii ni kwa sababu nyaraka hasa zile za muda mrefu zinahitaji kutunzwa kitaalamu.

Uchunguzi wa Kamati umebaini kwamba, watendaji wengi wa Taasisi ya Nyaraka wana utaalamu mdogo sana katika suala la nyaraka, ni watendaji wachache tu ambao ndio wanaotegemewa kwa kuwa na utaalamu huo. Suala hili linachangiwa zaidi na kutokuwepo kwa fursa za kuwaendeleza kielimu watendaji wa Taasisi hii, lakini pia Kamati imebaini kwamba, kwa wale wanaojitolea kujiendeleza kwa gharama zao kumekuwa na vikwazo vingi vya kuwanyima ruhusa kutoka kwa uongozi, hali inayopelekea kudumaa kielimu kwa watendaji hao.

**Ukosefu wa wataalamu wakutosha katika eneo la uhifadhi wa nyaraka:**

Taasisi ya Nyaraka ina watendaji wengi wanaohusika na usimamizi wa chumba kinachohifadhia nyaraka *"repository room/search room",* ambao ndio wanaohusika kwa karibu na suala zima la usimamizi wa nyaraka zilizopo katika Taasisi hii; ikiwemo kupanga nyaraka, kutowa na kuwapatia watafiti wanaokuja kutumia nyaraka hizo katika jengo hilo, kurikodi kilichoazimwa na kilichorejeshwa n.k.

Hata hivyo, kati ya watendaji hao, ni watendaji wachache tu ndio wenye utaalamu wa uhifadhi wa nyaraka. Katika hali hii ni dhahiri kwamba Taasisi hii ina upungufu mkubwa wa wataalamu wa maswala ya Nyaraka hali inayopelekea wengi wao kufanya kazi kwa uzoefu tu.

Hivyo basi, katika uchunguzi wake Kamati imeona kwamba mambo yaliyoelezwa hapo juu, yamechangia au kurahisisha suala la wizi au upotevu wa nyaraka, hii inawezekana watu waliokuwa na nia mbaya ya kuziiba nyaraka za nchi yetu walijuwa udhaifu huo wa Ofisi pamoja na watendaji wake kwa ujumla na ndio maana wakaamua kuwatumia watendaji hao badala ya kutumia njia nyengine kama kuvunja na kuiba.

**Uhifadhi wa Nyaraka Nyengine Katika Taasisi ya Nyaraka:**

Kamati haikuishia katika kuangalia sababu zilizopelekea wizi au upotevu tu, bali ilikwenda mbali zaidi na kuangalia uhifadhi wa nyaraka nyengine ulivyo katika Taasisi hii na katika eneo hili mambo yafuatayo yaligundulika:-

i. Uchakavu wa nyaraka na ukosefu wa vifaa vya kutibu nyaraka;
*ii.* Uhifadhi mbaya wa nyaraka zinazohitaji uhifadhi maalum wa *(AVs);*
*iii.* Upungufu wa vyombo vya uhifadhi *(acid boxes);*
iv. Kutokuwepo kwa mfumo mzuri wa wa kumbukumbu ya Nyaraka zinazochukuliwa na Taasisi nyengine za Serikali;
v. Kutokuwepo kwa uhifadhi mzuri wa nyaraka katika Taasisi nyengine za Serikali (kwa mujibu wa masharti ya Sheria Nam. 3 ya 2008) yanayozitaka Taasisi za Serikali kuhifadhi na kuweka kumbukumbu vizuri kwa ajili ya kuhifadhiwa;
vi. Ukosefu wa vituo vya kukusanyia kumbukumbu kwa ajili ya kuhifadhiwa *(archive centres)* nyaraka nyingi zimepotea au zimewekwa sehemu zisizostahiki (*misplaced*); na
vii. Ufinyu wa jengo la kuhifadhia Nyaraka.

Maelezo ya ufaafanuzi ni kama ifuatavyo:-

**Uchakavu wa nyaraka na ukosefu wa vifaa vya kutibu nyaraka:**

Katika ukaguzi uliofanywa na Kamati imebainika kwamba nyaraka nyingi, hasa zile za zamani zilizopatikana kutoka kwa utawala wa kifalme, zimeharibika na kuchakaa kwa kiasi kikubwa.

Sababu za kuchakaa na kuharibika kwa nyaraka hizo ni kutokuwa na utaratibu wa kawaida wa kuzifungua ili zipate hewa ya kawaida, pia nyaraka hizi ni za muda mrefu na zilihitaji kufanyiwa *binding* na *lamination* ili kuziwezesha karatasi zilizotumika kubakia katika hali ya umadhubuti.

Jambo la kusikitisha ni kwamba nyaraka hizi zilitakiwa zipatiwe madawa kwa ajili ya kuzitibu kutokana na hali ya hewa ya muda mrefu, lakini Taasisi haina dawa hizo wala nyaraka hazijawekwa dawa kwa muda mrefu. Ni dhahiri kwamba kila siku zinavyokwenda mbele hazina hii itadhidi kuharibika ikiwa hatua za haraka hazitochukuliwa.

**Uhifadhi Mbaya wa Nyaraka na Picha Zinazohitaji Uhifadhi Maalum wa (*AVs*):**

Katika eneo hili Kamati imefanya uchunguzi na kugundua zipo nyaraka za picha (*AVs*) ambazo zimehifadhiwa katika masanduku ya bati katika Taasisi ya nyaraka. Kamati imeelezwa kuwa nyaraka hizi zinahusu mambo mbali mbali ya Zanzibar zimeletwa kutoka Uingereza ambako zimehifadhiwa katika Nyumba ya nyaraka. Prof. Abdul Shariff alizipiga picha maalumu na kuzihifadhi na kuzileta katika Nyumba ya Nyaraka Kilimani.

Hata hivyo nyaraka hizo nyingi zinazofika 3000 zimehifadhiwa katika masanduku ya bati na kupata joto na idadi kubwa zimeshaharibika kwa joto kali, hata mashine ya kusomea nyaraka hizo nayo imeshaharibika.

Juhudi kubwa zilifanywa kwa kuzitafuta, kuzikusanya na hatimaye kuzileta Zanzibar, lakini ni bure bure zimepotea kutokana na nyaraka hizo kutokuhifadhiwa vizuri.

**Upungufu wa vyombo vya uhifadhi (*Acid boxes*):**

Baadhi ya nyaraka zimekuwa katika hali hatarishi na kuharibika kutokana na kukosekana kwa maboksi maalumu ya kuzihifadhia kama vile maboksi ya *'acid'* ambayo yanazuia wadudu kuzifikia na kuziharibu. Maboksi hayo ambayo yaliyowahi kutolewa Msaada kutoka Serikali ya Uingereza mwaka 1980 mpaka leo hayajapatikana mengine ya kiwango kama hicho, hivyo kuzifanya nyaraka nyengine kuhifadhiwa kwenye maboksi ya kawaida ambayo hayatoi kinga dhidi ya uharibifu.

**Kutokuwepo kwa mfumo mzuri wa kumbukumbu ya Nyaraka zinazochukuliwa na Taasisi nyengine za Serikali:**

Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa imepewa mamlaka kwa mujibu wa Sheria Nam. 3 ya 2008, kifungu cha 26, kuweza kuwapatia watu mbali mbali zikiwemo Taasisi za Serikali na kutoa huduma ya kutumia kumbukumbu zilizopo katika jengo la nyaraka kwa kufuata utaratibu utakaowekwa na Taasisi hiyo.

Kwa kawaida watu wanaotaka kutumia nyaraka hizo hutakiwa kujisomea ndani ya jengo hilo na ikiwezekana kupatiwa nakala kivuli *(photocopy)* ya nyaraka wanazozihitaji kwa kufuata utaratibu maalum.

Sheria ya kuanzisha Taasisi ya Nyaraka imetoa sharti la kutolewa kopi tu, hata hivyo kuna baadhi ya Taasisi za Serikali kwa mfano Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, kwa kuwa inashughulika na kufuatilia taratibu za Mirathi ya Kiislamu Mahakama imelazimika kutumia Nyaraka halisi. Hivyo basi, kuilazimu Taasisi ya Nyaraka kwa kufuata amri ya Mahakama kutoa nyaraka halisi.

Kamati imebaini kwamba hakuna utaratibu mzuri wa kuweka kumbukumbu za nyaraka zinazotoka kwenda katika Kamisheni ya Wakfu na zile zinazorudishwa baada ya kumalizika mashauri ya Mahakamani.

Kamati imetaarifiwa na Watendaji wa Taasisi ya Nyaraka kwamba, kuna nyaraka nyingi zimechukuliwa na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana na hazijarejeshwa bado. Rejea Kiambatanisho namba KTN 33.

Katika kutaka kujua ukweli wa jambo hilo Kamati ilimwita na kumuhoji Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana na watendaji wake ili kupata ufafanuzi juu ya kadhia hiyo. Katika hali ya kushangaza Kamisheni hiyo ilitoa orodha ya nyaraka walizowahi kuazima na ambazo bado hawajazirejeshwa. Rejea Kiambatanisho namba KTN 34.

Uongozi wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ilionesha wasiwasi wake baadae katika utaratibu unaotumika kuweka kumbukumbu za nyaraka hizo kuwa sio mzuri sana, ambapo baadhi ya orodha ya nyaraka zilizoorodheshwa kwamba zimechukuliwa na Kamisheni hazijawahi kuazimwa kwa mfano nyaraka zinazohusu mirathi ya wasiokuwa waislamu, Kamisheni imesema kwamba haihusiki na mambo ya dini nyengine na Kamisheni zimejumuishwa katika orodha hiyo ya nyaraka zilizopotea. Rejea Kiambatanisho namba 33.

Kamisheni imeleza zaidi Kamati kwamba, inaonekana watu binafsi kwa kutumia njia zao wenyewe wana uwezo wa kupata nyaraka zinazohusu mirathi yao. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, ilishawahi kutokea wahusika walitaka kufungua kesi ya mirathi katika Kamisheni, lakini zilipotafutwa kumbukumbu zinazohusu mirathi hiyo kutoka katika Taasisi ya Nyaraka hazikuwepo na badala yake kumbukumbu hizo walikuwanazo wahusika wenyewe, jambo ambalo ni kinyume na utaratibu na inaonekana ni dhahiri kwamba walizipata kutoka katika Taasisi ya Nyaraka ambayo ndiyo Ofisi pekee iliyotakiwa kuhifadhi nyaraka hizo.

Kamati imebaini kwamba kuna mkanganyiko mkubwa katika kuweka kumbukumbu za Nyaraka katika Taasisi ya Nyaraka, hasa baada ya kupata fursa ya kulikaguwa buku linalowekwa kumbukumbu hizo. Inaonekana kwamba, hakuna utaratibu wa mtu maalum kufanya kazi hiyo, hali inayopelekea kutokuwa na uhakika nyaraka gani ilitolewa na kupokewa na nani. Lakini pia, baadhi ya wahusika hawaelewi hata hicho walichokirikodi kutokana na uwelewa mdogo wa lugha ya kigeni inayotumika kurikodia buku hilo yaani lugha ya Kiengereza.

**Kutokuwepo kwa uhifadhi mzuri wa nyaraka katika Taasisi nyengine za Serikali:**

Kwa mujibu wa masharti ya Sheria Nam. 3 ya 2008) yanayozitaka Taasisi za Serikali kuhifadhi na kuweka kumbukumbu vizuri kwa ajili ya kuhifadhiwa. Katika kifungu cha 13 cha Sheria Nam. 3 ya mwaka 2008 na Kifungu cha 95 cha Sheria ya Utumishi wa Umma namba 2 ya mwaka 2011 na Kanuni ya 52 ya Kanuni za Utumishi wa Umma mwaka 2014 ambapo inaelezwa kuwa Taasisi zote za Serikali zinawajibika kuwa na utaratibu wa kutunza kumbukumbu za shughuli zinazofanyika kikawaida katika taasisi hizo.

Hii ni kwa sababu Sheria inazichukulia kumbukumbu hizo kuwa ni siri hadi itakapotimia miaka 30 toka kuandikwa kwa kukumbuku hizo. Baada ya kipindi hicho kumbukumbu hizo hutakiwa kuhamishiwa katika Jumba la Nyaraka kwa ajili ya kuhifadhiwa na kuweza kutumika kama ni rejea kwa wataalamu na utafiti wa nchi za nje.

Utaratibu huu unawezesha, kuzitumia nyaraka kwa ajili ya matumizi ya kizazi kijacho. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba Taasisi nyingi za Serikali hazina utaratibu mzuri wa kuzihifadhi nyaraka hizo,

hali inayopelekea kukosekana kwa kumbukumbu nyinyi za miaka ya karibuni hususan baada ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kamati ilipata taarifa kwamba kuna kumbukumbu za sauti za matukio ya wakati wa Mapinduzi ya mwaka 1964 ambazo zinahifadhiwa katika *ZBC Radio*, lakini Kamati imeelezwa kuwa kumbukumbu hizo haziko katika hali nzuri na kwa mujibu wa Sheria zilitakiwa ziwe zimehamishiwa katika Jumba la Nyaraka lililopo Kilimani.

Kamati katika kutaka kujua ukweli wa suala hilo Kamati ilifanya ziara katika ofisi *ZBC Radio* na kuelezwa kuwa kumbukumbu hizo hazipo. Kamati ilitaka kujua kumbukumbu nyengine zinazohusu kuanzishwa redio tokea mwaka 1951 nazo pia imeelezwa kuwa hazipo, badala yake kumbukumbu zilizokuwapo ni kuanzia mwaka 1964 ambapo Kamati imeona kuwa siyo kipindi ambacho redio hiyo imeanzishwa ingawa kumbukumbu hizo ni muhimu.

**Ukosefu wa vituo vya kukusanyia kumbukumbu kwa ajili ya kuhifadhiwa** (***Archive centres***)***:***

Kutokana na ukosefu wa vituo vya kukusanya nyaraka ambazo hazijafika muda wa kuhifadhiwa, Kamati imeona kuwa nyaraka nyingi zinapotea au zinawekwa sehemu zisizostahiki *(misplaced).* Nyaraka kama hizo Kamati imeona zimewekwa kwenye kontena nyuma ya jengo la Afisi ya Nyaraka, ambapo wadudu kama panya n.k. wanaziharibu.

Kwa kuwa kumbukumbu za Taifa zinatokana na shughuli mbali mbali za kila siku zinazofanywa katika Taasisi za Serikali, ni dhahiri kwamba kila taasisi ina uwezo wa kuzalisha kumbukumbu nyingi na muhimu kwa ajili ya Taifa letu.

Hivyo basi, ukweli kwamba kumbukumbu za Taifa hili ni nyingi kwa sasa hauwezi kupingika, hasa kwa kuwa shughuli za kiserikali zinatanuka kwa kiasi kikubwa ndani na nje ya nchi, ikilinganisha na kipindi cha miaka ya 50 kabla ya Mapinduzi ya mwaka 1964.

Nchi imekuwa ikifanya maingiliano ya kitaifa na kimataifa, mikataba inayofungwa baina ya nchi yetu na nchi nyengine imekuwa ni mingi, lakini pia matukio ya kisiasa nayo yamekuwa mengi zaidi. Haya yote yanasababisha kuwepo kwa kumbukumbu nyingi ambazo kwa ukweli kuna haja ya kutafutiwa utaratibu mzuri wa kuhifadhi zaidi na kulitumia Jumba la Nyaraka lililopo sasa ambalo kwa kweli linaonesha kuzidiwa.

Kwa mujibu wa kifungu cha 19 cha Sheria namba 3 ya mwaka 2008, Mhe. Waziri amepewa Mamlaka ya kuanzisha baada ya kushauriana na Bodi ya Taasisi ya Nyaraka anaweza kuanzisha vituo vyengine vya kuhifadhia nyaraka nje ya Jumba la Nyaraka.

Hii itasaidia kuweza kuweka kumbukumbu nyingi ambazo kwa sasa zinaonekana kuzagaa katika maofisi mbali mbali bila ya kuwa na uangalizi mzuri wa kitaalamu. Hata hivyo, tokea kupitishwa kwa Sheria hii mwaka 2008, hakuna kituo kilichofunguliwa kwa malengo hayo. Kamati inaamini kwamba umuhimu wa kufungua vituo hivyo upo, ambapo vingeliweza pia kutumika kwa kuhifadhi zile nyaraka muhimu zaidi na nyeti kwa ajili ya Taifa na ingelikuwa ni vigumu watu wenye nia mbaya kuweza kuzifikia kiurahisi.

Pia, Kamati ilipewa taarifa ya kuwepo kumbukumbu ambazo zipo katika hali mbaya katika jengo la Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Elimu Amali, lakini kutokana na ufinyu wa muda haikuweza kufika katika eneo hilo.

**Ufinyu wa jengo la kuhifadhia Nyaraka:**

Kama ilivyoelezwa awali kwamba jengo la Kuhifadhia Nyaraka lilianzishwa miaka mingi iliyopita. Na ni dhahiri kwamba kwa wakati huo jengo lile lilikuwa la kutosheleza kutokana na mahitaji yaliyokuwepo wakati huo. Hata hivyo, kutokana na kukuwa kwa maendeleo ya nchi, kukuwa kwa Shughuli za kiserikali, imepelekea kuzalishwa kwa kumbukumbu nyingi ambazo zinahitaji kuhifadhiwa.

Vile vile, kwa kuwa historia ya Zanzibar ina nafasi kubwa katika ulimwengu, nyaraka zilizokuwepo katika jumba lile limepelekea kupatikana kwa umaarufu kutika sehemu mbali mbali zilizopo nje ya Zanzibar, wataalamu na watafiti kutoka ndani na nje wamekuwa wakifika kwa ajili ya kuzitumia kumbukumbu hizo, hali hii pia imechangia kulifanya jengo lile kuhitaji nafasi kubwa kwa ajili ya kuwapa wasaa mzuri wataalamu hao.

Kamati ilipomuhoji Prof. Abdul Shariff kwa nafasi yake ya utaalamu aliiambia Kamati kwamba nyaraka za Zanzibar ni za zamani zaidi kwa Kanda ya Afrika Mashariki na Kati ambapo nchi nyengine zimeanza kuhifadhi nyaraka za kuanzia miaka ya 1890 wakati za Zanzibar imeanza kuhifadhi nyaraka mwaka 1840. Samahani 1890 ndipo ilipoanza Afrika Mashariki na Kati, lakini Zanzibar imeanza 1840, naweka *Hansard* sawa.

Sio hilo tu, bali hata chumba kinachotumika kuhifadhia nyaraka ni kidogo hali ilinayosababisha mrundikano wa nyaraka nyingi sana katika sehemu moja. Hali hii ni hatari kwa ubora wa nyaraka hizo.

Vile vile, eneo ambalo Jumba la Nyaraka lipo, pia haliendani na hadhi ya Taasisi hiyo, Kamati imebaini kuwa jengo hilo linatumia mlango mmoja tu wa kuingilia kutokea na vile vile mna nyumba ya mtu binafsi, hali ambayo si salama kwa hazina iliyomo ndani ya jumba lilo.

**HADIDU REJEA YA PILI**

**KUPENDEKEZA NJIA MBALI MBALI MUAFAKA AMBAZO NYARAKA NYENGINE ZITAKUWA SALAMA**

Katika hadidu rejea ya pili, Kamati imejielekeza katika kuchambua na kupendekeza njia mbali mbali ambazo zinaweza kufanywa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba nyaraka nyengine ziltakuwa salama kwa ajili ya manufaa ya Taifa hili.

Katika uchambuzi wa hadidu rejea hii, Kamati inapendekeza kuzigawa njia hizo za kuzihifadhi nyaraka katika makundi mawili kama ifuatavyo:

a. Nji za kuzihifadhi nyaraka dhidi ya wizi na upotevu.

b. Njia za kuzihifadhi nyaraka dhidi ya uharibifu.

**a. Njia za kuzihifadhi nyaraka dhidi ya wizi na upotevu:**

Katika kufafanua njia hizi Kamati imejikita zaidi katika kupendekeza njia ambazo zitaweza kusaidia kuziepusha nyaraka zilizopo dhidi ya wizi na upotevu usije ukatokezea tena. Njia hizo zitasaidia kuweza kuhakikisha kwamba nyaraka zilizobakia zinakuwa salama wakati wote. Njia hizo ni kama ifuatazo:

**Uwepo wa uwajibikaji kwa watendaji wote wa Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa:**

Kwa kuwa suala la wizi wa nyaraka uliotokea katika Taasisi hii, umesababishwa kwa kiwango kikubwa na uzembe uliofanywa na baadhi ya watendaji waliotakiwa kusimamia majukumu yao kila siku ya

kuendesha Taasisi hii, hivyo, suala la uwajibikaji kwa watendaji litasaidia kwa kiasi kikubwa kuepusha matendo maovu kama hayo.

Suala la uwajibikaji lina maana ya kuhakikisha kwamba kila mmoja katika Taasisi anawajibika kutekeleza majukumu yake aliyopangiwa kwa mujibu wa taratibu za kiofisi. Hivyo basi, viongozi wanatakiwa kufanya kazi yao ya uongozi na usimamizi dhidi ya wale waliotakiwa kuwaongoza na kuwasimamia.

Na watendaji wenye dhamana nyenginezo wanatakiwa kuzitekeleza dhamana zao kwa kufuata taratibu zilizowekwa. Kutokuwajibika kumepelekea maafa makubwa ambayo yameisababishia hasara kubwa Serikali na Taifa kwa ujumla, mfano mzuri ni tukio ambalo Kamati imetaarifiwa na baadhi ya watendaji kwamba watendaji wa Taasisi hii walimuona mshukiwa wa wizi Ndugu Mwanakombo Ali Haji akitoka na vitu ndani ya chumba cha kuhifadhia nyaraka, lakini kutokana na wasimamizi wa chumba hichi kutokuwajibika, walimuacha kutoka na hatimaye kupoteza ushahidi wa tukio hilo.

**Uimarishaji wa usalama katika Taasisi ya Nyaraka:**

Uimarishaji wa usalama katika maeneo yanayolizunguka Jumba la Nyaraka ni suala la msingi. Uimarishaji huu uelekezwe katika chumba cha uhifadhi nyaraka na eneo lote la Taasisi. Kamati ilipongeza hatua ya kuweka mitambo ya *CCTV camera* ambayo itasaidia kugundua wahalifu, lakini inasisitiza kuhakikishwa kwamba watumishi watakaowekwa kuisimamia mitambo hiyo wawe ni wenye utaalamu na uadilifu wa hali ya juu.

Inapendekezwa pia kuwa, kuwekwa mitambo ya kutumia vitambulisho maalum kwa wale wote watakaokuwa na dhamana ya kuingia katika chumba cha kuhifadhia nyaraka, hii itasaidia kuepusha wasiohusika kuweza kuingia na kufanya uharibifu.

Suala la usalama pia linatakiwa liimarishwe kuanzia mlangoni, imefikia wakati sasa mlango wa kuingilia Taasisi hiyo uwe na mitambo maalum wa kukagua watu wanaoingia na kutoka, hatua hii itasaidia kupunguza uhalifu.

Pia, Kamati inaitaka Serikali kuweka askari wenye silaha kwa lengo la kuweka ulinzi wa kutosha katika maeneo hayo, hii ni kwa sababu watu wenye nia ovu ya kuziiba nyaraka za nchi hii wanaweza kutumia njia mbadala ya kuvunja ikiwa watakosa njia ya kuwatumia watumishi wa Taasisi kama wanavyofanya sasa hivi.

Vile vile, katika jumba hilo bado kuna nyaraka nyingi muhimu zimebakia nazo pia zinahitaji kulindwa zisije zikapata athari ya kuibiwa.

**Marekebisho ya kimuundo wa Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa:**

Muundo wa utumishi wa Taasisi hiyo ndio unaotoa muundo wa Taasisi yote kwa ujumla pamoja na Bodi kwa mujibu wa Kifungu cha 4 na 8 cha Sheria namba 3 ya 2008.

Kwa mujibu wa maelezo ya watendaji wa Taasisi hiyo waliyoyatoa mbele ya Kamati, walieleza kwamba, Taasisi hii inatakiwa iwe na Idara zinazoongozwa na wakuu wa Idara, pamoja na vitengo vinavyoongozwa na wakuu wa vitengo hivyo.

Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kurekebisha Muundo wa Taasisi hii ili iweze kufanya kazi vizuri na kumuwezesha kila mtendaji kujua nafasi yake, cheo chake na majukumu yake. Hatua hii itasaidia wakati wa kuwawajibisha wahusika waliopewa dhamana wakati wanaposhindwa kutekeleza dhamana zao. Hali

ilivyo sasa katika Taasisi hii ni kwamba watendaji waliopo wanafanya majukumu yao kwa mazowea tu sio kwa kuelewa na kwa kufuata utaratibu.

Kamati imeelezwa kwamba, muhusika aliyeachiwa kusimamia Ofisi wakati Mkurugenzi hayupo ambaye ni ndugu Moza Zahran hakupewa mamlaka hayo kwa barua, alipewa tu kwa mdomo kiasi kwamba hata hakuwa na nguvu na amri kwa watendaji wenzake juu ya kazi anayoifanya. Kamati inasisitiza hapa kuwa muundo wa Taasisi hiyo urekebishwe kwa kuwepo nafasi ya Mkurugenzi Msaidizi.

**Kufanywa marekebisho ya Sheria ya kuanzisha Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa Nam. 3 ya mwaka 2008:**

Sheria ya kuanzisha Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa Nam. 3 ya mwaka 2008, ilianzishwa kwa malengo ya kuweka utaratibu mzima wa kuendesha Jumba la Nyaraka.

Hata hivyo, Sheria hii imeelezwa kuwepo kwa Mkurugenzi wa Taasisi hiyo ambaye ndiye atakaekuwa msimamizi wa shughuli zote za Taasisi hii. Kamati katika uchunguzi wake imebaini kwamba, licha ya kuwepo kwa matukio ya kupotea na kuibiwa kwa nyaraka kwa muda mrefu, lakini tukio la wizi wa nyaraka uliotokezea hivi karibuni umechangiwa sana na kutokuwepo kwa Mkurugenzi Ofisini kwa muda mrefu.

Kwa kuwa, hali ya ugonjwa aliokuwa nao Mkurugenzi ilimsababishi kutoweza kufika Ofisini, ilipelekea Taasisi hiyo kubakia muda mrefu bila ya kuwa na kiongozi na kwa kuwa hakuna mtu aliyeteuliwa rasmi kukaimu nafasi hiyo, ilipelekea baadhi ya watendaji kufanya kazi kwa utashi wao wenyewe na kuigeuza Taasisi hii kuwa shamba la bibi.

Kamati imeshawishika kusema kwamba kuna haja ya msingi ya kufanywa marekebisho ya Sheria hii ili iweze kuanzisha nafasi ya Naibu Mkurugenzi wa Taasisi hii kama ilivyotangulia kulezwa, ambaye atakuwa msaidizi mkuu wa Mkurugenzi.

Hadi hivi sasa, wakati ripoti hii inasomwa mbele ya Baraza hili tukufu ni kwamba Mkurugenzi hawezi kuhudhuria kazini ipasavyo. Kamati inaamini kwamba, si ugonjwa tu bali hata umri mkubwa alionao Mkurugenzi unamtaka kwa sasa aweze kupumzika na aweze kuwa mshauri na kuwaachia wengine waendelea jukumu hilo.

Kamati wakati inahitaji kufanya ukaguzi wa nyaraka ilikusudia kumshirikisha Mkurugenzi katika kila hatua ya ukaguzi huo, kwa sababu ingekuwa rahisi kupata majibu ya maelezo ambayo yangeibuka wakati wa ukaguzi ulipokuwa ukiendelea. Hata hivyo, kutokana na hali yake ya afya hakuweza kushiriki hata kidogo katika shughuli hiyo.

Si hilo tu lakini pia sheria hii ina ulazima wa kufanyiwa marekebisho katika eneo la adhabu inayotolewa dhidi ya mtu anayetiwa hatiani kwa kosa la kuharibu, kuiba au kuchana nyaraka na kadhalika. Kwa mujibu wa kifungu cha 24 cha Sheria ya Nyaraka kinaeleza kwamba ni kosa kwa mtu yeyote kuhamisha, kutoa, kuchana au kuharibu kwa makusudi kumbukumbu au nyaraka bila ya kuwa na ruhusa ya Mkurugenzi na mtu atakaebainika kutenda kosa hilo atahukumiwa kulipa faini isiyopunguwa shilingi laki tano au kifungo kisichopunguwa miezi kumi na mbili.

Kamati inaona kwamba kiwango cha chini cha adhabu kilichowekwa ni kidogo, kwa kulinganisha na thamani ya nyaraka zilizomo katika Jumba la Nyaraka. Nyaraka ambazo ni za awali zaidi katika ukanda mzima wa Afrika Mashariki na Kati, lakini pia baadhi ya nyaraka hizi zinapatikana Zanzibar tu. Vile vile, inaonekana kwamba watu wanaozinunua nyaraka hizi kutoka kwa watumishi wa taasisi hii, wanazinunua kwa pesa nyingi sana. Kama Kamati ilivyoelezwa na Ndugu Fuad Abdulla ambaye ni mtendaji wa Taasisi

ya Naraka kwamba,  muhusika wa ushawishi wa kuibiwa kwa nyaraka hizi Humoud aliwaambia kwamba ikiwa watakubali kumpatia nyaraka anazozitaka atawabadilishia maisha yao na kuwa mazuri kama walivyo wenzao.

ii. **Uimarishwaji wa Ofisi ya Nyaraka:**

Ili Taasisi ya Nyaraka iweze kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa na kuepusha matukio ya tamaa kama yaliyofanyika katika miaka mingi iliyopita, kuna haja ya makusudi ya kuiimarisha taasisi hii ili iendane na hadhi na umuhimu wa nyaraka zinazohifadhiwa pale. Uimarishaji huo unatakiwa uelekezwe katika maeneo mengi kama vile kuongezewa wataalamu watakaokuwa na ujuzi wa kuzitunza na kuzihifadhi nyaraka zilizopo. Pia, wataalamu ambao kwa kiasi kikubwa watakuwa na uelewa wa thamani ya nyaraka zilizopo katika taasisi hii.

Vile vile, uimarishaji wa ofisi ujielekeze katika kuipatia taasisi vitendea kazi, kama kompyuta, viti, meza, *stationaries*, usafiri wa watendaji, eneo la kutosha la kuhifadhia nyaraka na la kufanyia kazi watendaji wenyewe. Pia, maslahi ya wafanyakazi ni suala la msingi sana kutiliwa maanani, kwa sababu ni dhahiri kwamba tamaa ya watendaji walioshiriki katika kufanya uhalifu huu imechangiwa sana na maslahi duni wanayoyapata. Jambo muhimu zaidi ya yote ni bajeti ya taasisi, kutokana na mapendekezo yaliyotolewa hapo juu yanakwenda sambamba na marekebisho ya bajeti inayotengwa kwa ajili ya taasisi hii, ni lazima iongezeke ili kukidhi mahitaji ya kuiimarisha taasisi hii. Pia, uingizwaji wa fedha zilizoidhinishwa ni lazima ziingiwe zote na kwa wakati ili taasisi iweze kujiendesha kisasa.

Kamati inapendekeza kwamba ipatiwe fungu lake la bajeti ambayo itaiwezesha kuidhinishiwa fedha zake na Baraza la Wawakilishi kuliko kuiwacha ikawa kama Idara ya Wizara jambo ambalo linasababisha kukosa fedha za kutosha kwa ajili ya kazi zake.

iii. **Kuwepo kwa Mpango wa Kawaida wa Ukaguzi wa Nyaraka:**

Ukaguzi wa nyaraka ni jambo muhimu sana, kwa sababu ndio utakaopelekea kujua nyaraka zipi zipo na zipi hazipo, kama ingekuwa kuna utaratibu wa kawaida ni dhahiri kwamba tukio la wizi lingegundulika mapema na pengine lisingetokea kwa kiasi kikubwa. Kamati inapendekeza kuwepo utaratibu wa kufanywa ukaguzi wa nyaraka kwa kila robo ya mwaka na ripoti ya ukaguzi huo iwasilishwe katika Kamati ya Kisekta ya Baraza la Wawakilishi, wakati inapofanya ukaguzi wa kila robo mwaka

iv. **Ujenzi wa Vituo vya Kuhifadhiwa Nyaraka (*Archive Centre's*):**

Maendeleo ya Taasisi za Serikali yamepelekea kuanzishiwa kwa kumbukumbu nyingi katika taasisi hizo ambazo kwa kiasi kikubwa zimekuwa zikizagaa maeneo mbali mbali ya taasisi hizo. Kwa kuwa kumbukumbu hizo nyingi huwa hazijafikia muda wa kupelekwa katika Jumba la Nyaraka, hulazimika kubakia katika taaisisi husika zikisubiria kufikiwa muda wake. Katika hali ya kusikitisha taasisi nyingi hazina maeneo maalumu yaliyojengwa kwa ajili ya kuhifandia kumbukumbu zao ili ziweze kutunzwa hadi pale zitakapofikia muda wa kupelekwa katika Jumba la Nyaraka. Hali hii hupelekea kumbukumbu nyingi kupotea au kuharibika kutokana na kukosa uangalifu mzuri.

v. **Kuwaendeleza Watendaji wa Taasisi ya Nyaraka:**

Watendaji wa taasisi hii ni watumishi walioitumikia taasisi hii kwa muda mrefu na nidhahiri kwamba kwa sasa kiwango chao cha elimu hakiendani na mabadiliko ya ulimwengu ya matumizi ya Sayansi na Teknolojia. Imefika wakati sasa shughuli za kutoa taaluma zinazohusu masuala ya nyaraka zifanywe kwa njia za teknolojia mfano, kuweka kumbukumbu za wanaochukua na kurejesha nyaraka kwa kutumia mtandao maalum wa kompyuta, hii itasaidia kuweka kumbukumbu vizuri kusema hivyo, Kamati

inamaanisha kwamba kwa sasa utaratibu wa kuweka kumbukumbu kwa kutumia kalamu na karatasi kidogo haurahisishi utendaji.

v. **Njia za Kuhifadhi Nyaraka Dhidi ya Uharibifu:**

Katika sehemu hii Kamati inatoa mapendekezo haya kwa ajili ya kuisadia Serikali kuchukua hatua za mara moja kuzuia uharibifu wa nyaraka usiendelee. Uhabaribifu huo kama ulivyokwishaelezwa katika taarifa hii ukiachwa uendelee utasababisha dhana nzima ya uhifadhi isiwe na maana yoyote, kwa sababu huwezi kuhifadhi kitu halafu kinaharibika huku kikitazamwa tu. Hivyo, Kamati inaona zipo njia zikitumika kwa dhati basi zitasaidia kuhifadhi nyaraka hizo zisiendelee kuharibika:-

1. Kutafutwe vifaa vya kutibu nyaraka na vifaa hivyo viwepo muda wote. Aidha, Kitengo cha Utibabu wa Nyaraka (*conservation unit*) kipatiwe vifaa vya kisasa na dawa za kutibu nyaraka zinazoharibika. Kitengo hiki kwa sasa hakina vifaa wala madawa ya kutibu nyaraka ambazo nyingi zinaendelea kuharibika.

2. Kuwepo na hifadhi maalumu ya nyaraka za picha (*micro film*). Vile vile, Kamati inaitaka Serikali kuzichapisha nyaraka hizo ambazo zipo katika ukanda maalumu wa picha ambao unahitaji kifaa maalumu cha kusomea, kwa kuwa kifaa cha kusomea kilichopo kimeshaharibika kwa kukaa muda mrefu bila ya kutumika.

3. Mfumo wa uwekaji kumbukumbu za kuazima nyaraka ubadilishwe kwa taarifa za anayeazima na muhusika anayeazimisha kuwekwa vizuri kwenye daftari.

4. Kuwepo kwa utaratibu wa kuazimisha kopi za nyaraka zilizoprintiwa ambazo zimethibitishwa kuwa ni kopi za nakala halisi, ili kuepusha kuharibiwa au kuibiwa kwa nyaraka halisi. Vile vile, kwa watendaji kufuata utaratibu wa kuazimisha nyaraka utakaowekwa na taasisi hii.

5. Nyaraka zote ambazo hazikuwekea nambari za faharisi vizuri na kusababisha kutotambulika idadi yake (mfano kundi la nyaraka za *AA5 za Arabic Correspondents*) kwa kila barua iliyomo kwenye *volume* na nyaraka za picha za viongozi na matukio ya nchi, ziwekwe nambari za utambuzi.

6. Kufanya utaratibu wa makusudi wa kuzi *scan,* nyaraka zote ili ziwe katika *soft copy* ambazo zitatumika iwapo *hardcopy* itapotea au kuibiwa na kuzifanyia *binding* nyaraka zote ambazo zimeshakuwa za siku nyingi na zimeanza kuwa katika hali mbaya, ili kuzinusuru kuharibika moja kwa moja.

7. Kuwapo vituo vya kukusanyia nyaraka (*archive centers*), ambazo hazifanyi kazi kwa muda na kuzihifadhi ambapo zaidi ya miaka 30 zilikuwa zikikaa katika maeneo mengine.

8. Taasisi zote za Serikali ziwe na mpango wa kumbukumbu zitakazoratibiwa na masjala na vitengo hivyo viwe vinatoa taarifa ya ukusanyaji na uhifadhi kama inavyoelekezwa na masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, na

9. Sheria Nam. 3 ya 2008 na Sheria Nam. 2 ya 2011 itekelezwe kikamilifu katika utekelezaji wa kazi za Taasisi ya Nyaraka.

**HITIMISHO**

**MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

Kwa kuwa Kamati imeshabainisha kwa ujumla matokeo ya kadhia nzima ya wizi na kupendekeza njia mbali mbali muafaka za kuzuia tukio hilo lisijitokeze tena, aidha, mapendekezo kadhaa ya kuzuia uharibifu wa nyaraka usiendelee tena. Kamati inapenda kuweka mapendekezo mahasusi na mapendekezo ya jumla kwa serikali kuchukua hatua ili kuwepo utunzaji mzuri na endelevu wa nyaraka za Zanzibar.

**MAONI NA MAPENDEKEZO MAHUSUSI YA HATUA ZA KUCHUKULIWA**

Katika maoni na mapendekezo mahususi ya hatua za kuchukuliwa, Kamati inaelekeza yafuatayo kwa ajili ya kufanyiwa kazi:-

1. Hatua zichukuliwe ili nyaraka zilizoibiwa zipatikanwe. Kamati inapendekeza hapa kuwa mbali na majibu ya Idara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Zanzibar kutoka Makao Makuu ya Wizari kwa Jeshi la Polisi, majibu ambayo Kamati imeona hayakuwa sahihi kwa sababu zilizoelezwa hapo juu Jeshi la Polisi lichukue hatua ya kumpata Humoud kwa mujibu wa Sheria Nam. 5 ya mwaka 1986 na Mkataba wa Kimataifa kuhusu Mahusiano ya Kikonsula ya mwaka 1963.

2. Nyaraka zilizoibiwa zitangazwe katika mitandao ya Kimataifa popote pale zitakapopelekwa ijulikane kuwa nyaraka hizo zimeibiwa Zanzibar. Aidha, vyombo vya Kimataifa vya ufuatiliaji wa mali za urithi vitumike kusaidia kutafuta nyaraka hizo. Sambamba na hilo, Kamati inaitaka Serikali kuufanyia kazi ushauri uliotolewa na wataalamu wa Taasisi ya Nyaraka wa namna ya kufanya ili nyaraka zilizoibiwa zipatikane. Rejea ushauri huo katika Kiambatanisho namba KTN 35, barua ya Taasisi ya Nyaraka kwa Serikali ya tarehe 6 October, 2014.

3. Kwa kuwa Kamati imefanya kazi katika muda finyu sana, hivyo haikuweza kupata fursa ya kukagua sehemu zote zilizopo katika Taasisi ya Nyaraka. Hivyo basi, Kamati inapendekeza kwamba Serikali iunde Tume Maalumu itakayojumuisha wataalamu wa mihimili yote mitatu ya nchi ambayo ni Baraza la Wawakilishi, Mahakama na Serikali kwenda kufanya ukaguzi wa nyaraka zote zilizopo katika Jumba la Nyaraka na kuja na ripoti, ambayo itawasilishwa serikalini na hatimaye Barazani.

4. Kamati inapendekeza kwamba kupigwa muhuri wa moto nyaraka zote za chumba cha uhifadhi *(repository room)* ili kuwa na kielelezo cha ushahidi kamili wa umiliki wa Serikali. Vile vile, Kamati inaamini kwamba kwa kufanya hivyo Nyaraka za Zanzibar zitakuwa na alama maalumu ambayo popote itakapopelekwa itakuwa ni kielelezo cha kujitegemea kuwa nyaraka hiyo ni mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Jambo hili ni muhimu kwa kuwa nyaraka zilizopo sasa katika Jumba la Nyaraka hazina muhuri maalumu wa Serikali ambao unaonyesha umiliki wa nyaraka hizo.

5. Taasisi ya Nyaraka iweke Kanuni maalumu za matumizi ya nyaraka kwa watumiaji mbali mbali wanaofika hapo. Kanuni hizo ziweke masharti ambayo mtu yeyote atapewa asome kabla ya kutumia nyaraka hizo. Mfano, kutoruhusiwa kwa mtu yeyote kupewa nyaraka kongwe zilizokuwa halisi na badala yake mtu apatiwe kopi iliyothibitishwa na kadhalika.

6. Taasisi ya Nyaraka ipatiwe walinzi wa kudumu kutoka Jeshi la Polisi au Vikosi vya Idara Maalumu za SMZ, kama vile zinavyolindwa Taasisi nyengine za Serikali.

7. Kamati inapendekeza kurekebishwa mfumo wa uhifadhi wa nyaraka kwa kutafutwa *mobile shelf* ambazo ni salama zaidi na kuweza kuhifadhi nyaraka nyingi katika sehemu ndogo na kupunguza tatizo la ufinyu wa chumba cha kuhifadhia nyaraka kilichopo mamlaka ya nyaraka, na

8. Kamati inapendekeza kuwepo utaratibu wa mara kwa mara wa kuwapima afya wafanyakazi wa nyaraka ambao wanafanyakazi katika mazingira hatarishi kiafya ambayo ni ya vumbi la karatasi za zamani na dawa za kemikali za kutibu karatasi.

**MAONI NA MAPENDEKEZO YA JUMLA YA HATUA ZA KUCHUKULIWA**

Kamati inaelekeza maoni na mapendekezo yafuatayo kwa ajili ya kufanyiwa kazi:-

1. Sheria Nam. 3 ya mwaka 2008 ifanyiwe marekebisho kwa kuwekwa nafasi ya Mkurugenzi Msaidizi, kuongezwa kwa adhabu kali kwa uharibifu, wizi, uhamishaji kinyume na Sheria ya nyaraka na kadhalika. Aidha, marekebisho mengine ya sheria hiyo yazingatie maoni mbali mbali ya Kamati katika ripoti hii.

2. Serikali ifanye marekebisho ya uongozi wa Taasisi ya Nyaraka, kwanza kwa kuteua Bodi mpya ya Ushauri itakayokuwa na wataalamu wenye elimu na uzoefu wa Mambo ya Nyaraka mara baada ya kumalizika kwa muda Bodi iliyopo. Aidha, Serikali isichukuwe muda mrefu kuteua bodi nyengine, pili kuwepo Mkurugenzi Mkuu ambaye ataweza kutekeleza kazi zake kwa mujibu wa masharti ya Sheria Nam. 3 ya mwaka 2008.

3. Mapendekezo ya kuzitafuta nyaraka za Serikali kwa utaratibu wa Sheria za Kimataifa yafuate kama yalivyopendekezwa na wataalamu. Rejea Kiambatanisho namba KTN 35.

4. Uajiri wa wafanyakazi katika Taasisi ya Nyaraka ufuatiwe na uchunguzi wa kina kwa anayeajiriwa (*vetting*) ili kubaini taarifa za mwajiriwa kabla ya kuajiriwa.

5. Maslahi ya wafanyakazi yaimarishwe, Kamati imebaini kuwa maslahi madogo ya wafanyakazi ni moja kati ya sababu kuu zinazopelekea washawishike kirahisi kuiba nyaraka ambazo thamani yake ni kubwa, na

6. Taasisi ya Nyaraka ipatiwe fungu lake la bajeti (*vote*) badala ya kutegemea kasma kutoka Wizarani ambayo inaitazama Taasisi ya Nyaraka kama idara ya kawaida na kutokuona umuhimu wake kwa ukaribu.

Kamati inakiri kuwa licha ya kutumia muda mfupi na nguvu nyingi katika uchunguzi na kuja na mapendekezo hayo, haina maana kuwa uchunguzi huu umemaliza kila kitu isipokuwa yaliyogundulikana ni kwa mujibu wa muda na nyenzo ambazo Kamati hii imepewa kwa muda mfupi.

Katika kufanyakazi ya uchunguzi wa nyaraka zilizopo na zilizopotea, Kamati ilifanyakazi kubwa ya kutwa nzima ikisaidiana na Mtaalamu wa Kumbukumbu na Nyaraka kutoka Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, ndugu Abas Ibarahim Sanya ambaye amewahi pia kuwa mfanyakazi wa Taasisi ya Nyaraka kwa kipindi kirefu. Kamati iliafanya nae kazi ndugu Ibrahim Sanya kwa kipindi cha wiki nzima katika taasisi hii.

Lakini pia Kamati ilifanya kazi kwa kipindi cha wiki nzima pia na Mhe. Abdalla Mohammed Ali kwa kazi ya kutambua lugha ya Kiarabu ambayo ilikuwemo katika baadhi ya nyaraka na Mhe. Aballa Mohammed Ali yeye ni Mjumbe wa Baraza hili alifanya kazi ya kutafsiri na alisaidia sana Kamati. (*Makofi*)

Kamati pia ilitumia mtaalamu wa Taasisi ya Nyaraka, ndugu Omar Shehe Khamis ambaye nae pia alifanya kazi kubwa na alisaidiana na Kamati katika kupekuwa nyaraka mbali mbali. Kazi hiyo yote ilifanyika kwa wiki nzima na imegusa baadhi ya maeneo mengi (*sampling*) ambayo ilitosha kuonesha picha ya mapungufu kadhaa ya uwepo wa nyaraka zetu.

Katika kuhitimisha maelezo haya kamati napenda kusisitiza tena kuwa uchunguzi kamili ufanyike wa kuziorodhesha nyaraka zote na kuzitambua zilizopo na ambazo hazipo pamoja na kuweka faharisi kwenye *digital* ili ziweze kuhifadhiwa vizuri. Wakati wa uchunguzi Kamati iliweza kufika maeneo mbali mbali na ingeliwezekana kufika maeneo yote kama muda na nyenzo zingekuwa za kutosha. Kamati pia inapendekeza kwa Serikali kuwezesha uchunguzi huo ufanyike kwa jumba lote na vielelezo vyote viweze kupatikana ambavyo vitaweza kupatiwa wataalamu na hatimae kuweza kuwasilishwa katika maeneo husika.

Kamati inachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi ambaye muda wote hususan kwangu mimi kama Mwenyekiti wa Kamati ilikuwa tunakutana na kushauriana na hatimae kuweza kutoa maelezo pamoja na kuweza kufikia mustakabal wa mambo ambayo yalikuwa Kamati inawataza

Vile vile, tunawashukuru sana Katibu Mkuu wa Baraza la Wawakilishi ndugu Yahya Khamis Hamad kwa kazi kubwa kwa kusaidiana na wasaidizi wake ambaye alikuwa akiisaidia Kamati kuhakikisha kwamba inawapatia misaada kwa hali na mali katika kuthibitisha kuhakikisha kwamba Kamati na watendaji wake wanafanikisha kazi hii kwa ajili ya kuhakikisha kuwa kazi hii inafanyika kwa ufanisi mkubwa.

Na vile vile tunamshukuru sana Katibu Yahya kwa msaada wa kitaalamu, fikra na ushauri kwa muda wote mpaka ripoti hii ikawezwa kuletwa mbele ya Baraza hili.

Kamati inapenda kutoa shukurani za pekee kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote waliosaidia Kamati kwa kutoa taarifa mbali mbali na kwa umuhimu mkubwa, Kamati imepokea mchango mkubwa na wa aina yake ambao umetolewa na aliyekuwa Mwakilishi Jimbo la Magomeni Mhe. Salmin Awadh Salmin, ambaye amefariki kabla ripoiti hii kukamilika na kuwasilishwa Barazani. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahala pema peponi, *Amin*.

Kutokana na mchango wake mbele ya Kamati mnamo mwezi wa Januari, 2015 kamati imeweza kupata pakuanzia kutoka vyanzo muhimu vya taarifa ambavyo alishauri Kamati kama ambavyo tulikwisha kusema hapo mwanzoni. Ripoti hii isingelikamilika bila ya msaada mkubwa uliotolewa na Mkurugenzi

wa Taasisi ya Nyaraka pamoja na watendaji wake ambao walisaidia taarifa mbali mbali, naye tunamshukuru.

Kamati inatoa shukurani kwa mawaziri ambao walikubali kutoa maelezo mbele ya Kamati kuwezesha taarifa mbali mbali kupatikana. Lakini pia nikushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa mimi fursa ya kuweza kusoma taarifa hii leo mbele yako na wajumbe wote wakaweza kuisikia na wananchi wote kwa ujumla. Bila ya kusahau napenda kumshukuru Naibu Katibu Mkuu Afisi ya Rais, Kazi na Utawala Bora kwa kuipokea Kamati siku ya mwanzo ilipoanza kazi yake ya uchunguzi na kwa uzalendo wake wa kufatilia kadhia hii mpaka hapa ilipofika…

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa malizia muda unakwisha, malizia.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa (Mwenyekiti Kamati Teule ya Kuchunguza Upotevu wa Nyaraka):** Kazi hii ya kuchunguza imepita katika maeneo mengi ambayo kutokana na ufinyu wa muda na nafasi hii niliyonayo haitawezekana kutaja na kuwashukuru wote. Kamati inapenda kuwashukuru wale wote waliotoa mchango wa hali na mali kwa Kamati hii ambayo michango yao muhimu itakumbukwa milele kwa kufanikisha kazi hii.

Mwisho, shukurani za mwisho kabisa zimuendee Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye Kamati imepata taarifa kuwa ameahidi Serikali yake itachukua hatua ya kuzifanyia kazi ripoti hizi popote pale zitakapowasilishwa. Kamati inampongeza kwa hatua hiyo na kumtaka katika kuchukua hatua atafakari na kuyazingatia mapendekezo ya Kamati hii kwa maslahi ya nchi hii na vizazi vijavyo. Historia itamkumbukwa kwa uzalendo wake na uongozi wake wa kujali maslahi ya nchi yake kwanza.

Baada ya maelekezo hayo sasa kwa aina maalum Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana na kumpongeza sana Katibu wetu wa Kamati ndugu Khamis ambaye kwa leo amekuwa Katibu wa Baraza hapa kwa namna ambavyo alikuwa akinistahamilia na kunivumilia mimi pamoja na Kamati bila ya kumsahau Katibu wetu Latifa ambaye nae pamoja na kazi nyingi alizonazo alidiriki kuacha shughuli zake na kuungana nasi, kufanya kazi yetu kwa pamoja, lakini bwana Khamis namshukuru zaidi. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa stamina ulionesha kwa sababu muda wote wa jioni umeuchukua wewe. Waheshimiwa Wajumbe, niwashukuru na nyie kwa kusikiliza mawasilisho hayo naomba nitoe taarifa mbili;

Taarifa ya kwanza tunategemea kesho tukijaaliwa tuje tuanze kuchangia mpaka mchana, tukimaliza mchana tusali, tule tuingie kwenye semina ambao wenzetu kutoka Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania watatoa semina juu ya Mswada wa Miamala ya *Electronic* na Uhalifu wa Mtandano. Nashukuru kwamba semina mbili za nyuma mlishiriki kikamilifu.

Kwa hivyo, naomba na hii tuwatie moyo wenzetu tuje kwa wingi, tumalize mchana tuingie kwenye semina. Na huku juu mpaka hivi sasa nimepata wachangiaji wawili tukijaaliwa roho kufika ataanza Mhe. Prof. Makame Mshimba Mbarouk na baadae atafuatia Dkt. Hamza Hassan Juma, na wale wanaotarajia kuchangia wakasome asubuhi walete majina kwa sababu hatuanzi kwa maswali. Baada ya maelezo hayo sasa naahirisha kikao chetu hadi kesho siku ya Jumamosi tarehe 28/03/2015, saa 3:00 asubuhi. (*Makofi*)

*(Saa 1:42 usiku Baraza liliakhirisha mpaka tarehe 28/03/2015 saa 3:00 asubuhi)*